KANISA LA YESU KRISTO LA WATAKATIFU WA SIKU ZA MWISHO • APRILI 2015

Liahona

Kuelewa Dhabihu Takatifu ya Mwokozi, p. 34

Kwa Nini Kuwa Dhaifu Si Dhambi, p. 20

Jinsi ya Kufaulu katika Jioni ya Familia Nyumbani, pp. 10, 80

"Ni nani kwenu, mwenye kondoo mia, akipotewa na mmojawapo, asiyewaacha wale tisini na kwenda nyikani, aende kumtafuta yule aliyepotea hata amwone? . . .
"Naye akiisha kumpata, kwa furaha humbeba mabegani mwake."

Luka 15:4–5

Picha hii iliyopigwa Israeli Aprili 2010, inaonyesha hatari za mchungaji akinusuru kondoo wake.

Liahona, Aprili 2015

7

UJUMBE

4 **Ujumbe wa Urais wa Kwanza: Rais Monson Ahimiza Ujasiri**
Na Rais Thomas S. Monson

7 **Ujumbe wa Mwalimu Mtembeleaji: Sifa za Yesu Kristo—Bila Hila ama Unafiki**

MAKALA YA HABARI MAALUMU

14 **Ushawishi wa Kiroho wa Wanawake**
Na Starla Awerkamp Butler
Ushawishi wako kama mwanamke unafikia mbali zaidi ya kile kinachoweza kuonekana.

20 **Si dhambi kuwa Mdhaifu**
Na Wendy Ulrich
Jifunze jinsi ya kutofautisha kati ya dhambi na udhaifu na jinsi ya kubadilisha udhaifu kuwa nguvu.

26 **Dini Safi**
Na Mzee W. Christopher Waddell
Soma hatua hizi tatu zinazokuelekeza katika huduma isiyo na ubinafsi.

30 **Nina Haja Nawe Kila Saa**
Na Jonathan H. Westover
Kuimba wimbo kulifanya mabadiliko yote kwa familia hii ya Kikorea iliyokuwa inachunguza Kanisa.

34 **Dhabihu Takatifu ya Mwokozi Isiyo na Ubinafsi**
Na Rais Boyd K. Packer
Kupitia Upatanisho wa Mwokozi tunaweza kulipia akaunti zetu za kiroho za dhambi na hatia.

80 **Miaka 100 ya Jioni ya Familia Nyumbani**
Mnamo 1915 Rais Joseph F. Smith na washauri wake waliwaalika waumini kuanza kufanya jioni ya familia nyumbani, wakielezea utaratibu, malengo, na baraka zake.

IDARA

8 **Tunazungumza Kuhusu Kristo: Nguvu ya Imani**
Na Amber Barlow Dahl

10 **Nyumba Zetu, Familia Zetu: Jioni ya Familia Nyumbani—Mnaweza Kuifanya!**

12 **Fasihi za Injili: Amefufuka**
Na Rais David O. McKay

40 **Sauti za Watakatifu wa Siku za Mwisho**

KWENYE JALADA
Mbele: *Barabara ya Emau,* na Liz Lemon Swindle, isinakiliwe. Ndani ya jalada la mbele: Picha na Jim Jeffery. Ndani ya jalada la nyuma: Picha kielelezo na Cody Bell.

VIJANA WAZIMA



44 **Endeleeni kwa Imani**
Na Mzee Anthony D. Perkins
Jifunze kutoka kwa Nefi nini cha kufanya unapokabiliwa na maamuzi muhimu.

Ona kama unaweza kupata Liahona iliyofichwa katika toleo hili. Dokezo: Je ni wapi unaweza kuwasha mshumaa?

VIJANA

49 **Bango: Mtafute Yeye**

50 **Kwa Sababu ya Joseph**
Na Ted Barnes
Kwa uchache kuna karibu njia hizi sita ambazo kwazo, maisha yako yamekuwa tofauti kwa sababu ya Nabii Joseph Smith

53 **Nabii Aliye Hai**
Na Rais Ezra Taft Benson
Adamu? Nefi? Musa? Huenda ukashangazwa kujifunza ni nabii gani aliye muhimu zaidi

54 **Mfano wa Mwokozi wa Utiifu**
Namna tisa ambazo Yesu Kristo alituwekea njia tufuate.

58 **Nafasi Yetu**

60 **Jinsi ya Kuwa na Hekima**
Na Mzee Neil L. Andersen
Nini tofauti kati ya hekima ya ulimwengu na hekima ya Mungu?

61 **Kwa Ufahamu**

62 **Kundi Moja na Mchungaji Mmoja**
Kuelewa kila kitu kwa ukamilifu juu ya kazi ya mchungaji kunaweza kutuleta karibu na Mwokozi.

64 **Maswali na Majibu**
Ninawezaje kupata urahisi wa kuzungumza na askofu wangu kuhusu hojaama matatizo yangu?

WATOTO

66 **Ni Nani Shujaa Wako?**
Na Charlotte Mae Sheppard
Ellie alikuwa na uoga wa kuliambia darasa nani aliyekuwa shujaa wake wa kweli.

68 **Sala na Makanisa Makuu**
Na McKelle George
Wakati Dani alipotembelea kanisa kuu kule Uingereza, alijifunza somo muhimu kuhusu sala.

70 **Shahidi Maalum: Ni kwa nini kuwa mtiifu ni muhimu sana?**
Na Mzee Russell M. Nelson

71 **Wazo Zuri**

72 **Wakati wa Maandiko: Yesu amponya Mwenye Ukoma**
Na Erin Sanderson

74 **Michoro ya Maandiko: Yesu Awaponya Wagonjwa**

75 **Njia Sahihi**
Na Elder Claudio D. Zivic
Kufuata njia sahihi kunaleta mabadiliko yote.

76 **Kwa Watoto Wadogo: Ninajua Kwamba Yesu Ananipenda**
Na Jane McBride Choate

APRILI 2015 VOL. 2 NO. 1
LIAHONA 12564 743

Gazeti la kimataifa la Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho

Urais wa Kwanza : Thomas S. Monson, Henry B. Eyring, Dieter F. Uchtdorf
Akidi ya Mitume Kumi na Wawili: Boyd K. Packer, L. Tom Perry, Russell M. Nelson, Dallin H. Oaks, M. Russell Ballard, Richard G. Scott, Robert D. Hales, Jeffrey R. Holland, David A. Bednar, Quentin L. Cook, D. Todd Christofferson, Neil L. Andersen

Mhariri: Craig A. Cardon
Washauri: Mervyn B. Arnold, Christoffel Golden, Larry R. Lawrence, James B. Martino, Joseph W. Sitati

Mkurugenzi Mkuu: David T. Warner
Mkurugenzi wa Utendaji: Vincent A. Vaughn
Mkurugenzi wa Magazeti ya Kanisa: Allan R. Loyborg
Meneja wa Biashara: Garff Cannon

Mhariri Mtendaji: R. Val Johnson
Meneja Msaidizi wa Uhariri: Ryan Carr
Msaidizi wa Uchapishaji: Lisa Carolina López
Kuandika na kuhariri: Brittany Beattie, David Dickson, David A. Edwards, Matthew D. Flitton, Lori Fuller, Garrett H. Garff, LaRene Porter Gaunt, Mindy Anne Leavitt, Michael R. Morris, Sally Johnson Odekirk, Joshua J. Perkey, Jan Pinborough, Richard M. Romney, Paul VanDenBerghe, Marissa Widdison

Mkurugenzi Mtendaji Sanaa : J. Scott Knudsen
Mkurugenzi wa Sanaa: Tadd R. Peterson
Usanifu: Jeanette Andrews, Fay P. Andrus, Mandie M. Bentley, C. Kimball Bott, Thomas Child, Nate Gines, Colleen Hinckley, Eric P. Johnsen, Susan Lofgren, Scott M. Mooy, Mark W. Robison, Brad Teare, K. Nicole Walkenhorst
Mratibu wa Haki Miliki: Collette Nebeker Aune
Meneja wa Uzalishaji: Jane Ann Peters
Uzalishaji: Connie Bowthorpe Bridge, Julie Burdett, Katie Duncan, Bryan W. Gygi, Denise Kirby, Ginny J. Nilson, Gayle Tate Rafferty
Kabla ya Chapa: Jeff L. Martin

Mkurugenzi wa Uchapishaji: Craig K. Sedgwick
Mkurugenzi wa Usambasaji: Stephen R. Christiansen

Kwa manunuzi na bei nje ya Marekani na Kanada, nenda store.lds.org au wasiliana na kituo cha usambazaji cha Kanisa ama kiongozi wa kata au tawi.

Wasilisha miswaada na maswali katika mtandao liahona.lds.org; kwa barua pepe liahona@ldschurch.org ama barua *Liahona,* Rm. 2420, 50 E. North Temple St., Salt Lake City, UT 84150-0024, Marekani.

Liahona (neno katika Kitabu cha Mormoni linalomaanisha "dira" ama "kielekezo") imechapishwa katika Kialbeni, Kiarmeni, Bislama, Kibulgaria, Kikambodia, Kisebuano, Kichina, Kichina (kilichorahisishwa), Kikroeshia, Kicheki, Kidenishi, Kiholanzi, Kiingereza, Kiestoni, Kifiji, Kifinishi, Kifaransa, Kijerumani, Kigiriki, Kiangaria, Kiaislandi, Kiindonesiia, Kiitaliano, Kijapani , Kikiribati, Kikorea, Kilatvia, Kilithuania, Kimalagasi, Kimarshalizi, Kimongolia, Kinorwei, Kipolishi, Kireno, Kiromania, Kirusi, Kisamoa, Kislovenia, Kihispania, Kiswahili, Kiswidi, Kitagalogi, Kitahiti, Kithai, Kitonga, Kiukreni, Kiurdu, na Kivietinamu. (Masafa hutofautiana kwa lugha.)

© 2015 na Intellectual Reserve, Inc. Haki zote zimehifadhiwa Imechapishwa Marekani.

Nakala na nyenzo za picha katika *Liahona* zinaweza kunakiliwa kimuafaka, kwa matumizi yasiyo ya kibiashara ya kanisa au nyumbani Nyenzo za picha haziwezi kunakiliwa kama vikwazo vimeelezwa katika laini ya sifa na mchoro. Maswali a haki ya kunakili yanapaswa kuelekezwa ofisi ya Intellectual Property, 50 E. North Temple St., Salt Lake City, UT 84150, USA; barua pepe: cor-intellectualproperty@ldschurch.org.

For Readers in the United States and Canada: April 2015 Vol. 2 No. 1. LIAHONA (USPS 311-480) Swahili (ISSN 2326-3695) is published once a year (April) by The Church of Jesus Christ of Latter-day Saints, 50 E. North Temple St., Salt Lake City, UT 84150. USA subscription price is $1.00 per year; Canada, $1.20 plus applicable taxes. Periodicals Postage Paid at Salt Lake City, Utah. Sixty days' notice required for change of address. Include address label from a recent issue; old and new address *must* be included. Send USA and Canadian subscriptions to Salt Lake Distribution Center at address below. Subscription help line: 1-800-537-5971. Credit card orders (American Express, Discover, MasterCard, Visa) may be taken by phone or at store.lds.org. (Canada Post Information: Publication Agreement #40017431)

POSTMASTER: Send all UAA to CFS (see DMM 707.4.12.5). NONPOSTAL AND MILITARY FACILITIES: Send address changes to Distribution Services, Church Magazines, P.O. Box 26368, Salt Lake City, UT 84126-0368, USA.

Mawazo ya Jioni ya Familia Nyumbani

Toleo hili lina makala na shughuli ambazo zinaweza kutumika kwa ajili ya jioni ya familia nyumbani. Yafuatayo ni mawazo mawili.

"Nina Haja Nawe Kila Saa," ukurasa wa 30: Kama vile maneno ya wimbo "Nina Haja Nawe Kila Saa" yalivyomsaidia Pak Mi-Jung kuamua kubatizwa, nyimbo zinaweza kuwa na athari kubwa katika maisha yetu. Fikiria juu ya wakati ambao maneno ya wimbo yamebariki maisha yako na uzingatie kuelezea uzoefu huo kwa familia yako. Alika kila mwana familia achague wimbo aupendao na aseme jinsi ambavyo umebariki maisha yake. Kisha imba kila wimbo na familia yako. (Unaweza kuzigawa ili lifanyike kwa wiki kadhaa.)

"Sala na Makanisa Makuu," ukurasa wa 68: Baada ya kusoma hadithi hii, onyesha picha za makanisa tofauti ama taja makanisa tofauti katika mji wako na uongee kuhusu maswali haya na familia yako: Ni mambo gani ambayo unayo, yanafanana na ya dini zingine? Je Baba wa Mbinguni anahisi vipi kuhusu watoto Wake wote? Tunapaswa kuwatendea vipi watu ambao wana imani tofauti? Zingatia kutumia-makala "Weka usawa kati ya Ukweli na Uvumilivu" na Mzee Elder Dallin H. Oaks wa Akidi ya Mitume kumi na Wawili (*Liahona,* Feb. 2013, 28–35) ili kusaidia kujibu maswali haya.

KATIKA LUGHA YAKO

Liahona na maandiko mengine ya Kanisa yanapatikana katika lugha nyingi katika **languages.lds.org.**

MADA KATIKA TOLEO HILI

Nambari zinawakilisha ukurasa wa kwanza wa makala.

Agano Jipya, *54, 62, 72, 74*
Amri, *70, 75*
Asili ya kiungu, *58*
Dhambi, *20, 34*
Familia, *10, 50*
Haki ya Kujiamulia, *4, 20, 44*
Hatia, *20, 34*
Huduma, *26, 42*
Huzuni, *30, 41*
Imani, *8, 20, 44*
Jioni ya familia nyumbani, *10, 80*
Joseph Smith, *12, 50*
Kazi ya hekalu, *30, 43*
Kazi ya umisionari, *30, 40*
Kifo, *30, 41*
Kuponya, *8, 72, 74*
Maamuzi, *44, 60, 75*
Manabii, *53*
Mfano, *14, 66*
Mfungo, *30*
Msamaha, *20, 34*
Muziki, *30, 40*
Pornografia, *34*
Roho Mtakatifu, *30, 41, 42, 43, 44, 50, 58*
Sala, *68*
Shetani, *34, 61*
Toba, *34, 64*
Ufufuo, *12, 49*
Ujasiri, *4*
Ukuhani, *50*
Uongofu, *30*
Upatanisho, *20, 34, 49*
Upendo, *76*
Urejesho, *50*
Utiifu, *44, 54, 58*
Viongozi wa Kanisa, *53, 64*
Wanawake, *14*
Yesu Kristo, *7, 8, 12, 20, 26, 34, 49, 54, 62, 66, 72, 74, 76*

Na Rais Thomas S. Monson

Rais Monson Ahimiza

UJASIRI



Hata saa moja haipiti, Rais Thomas S. Monson ameelezea, kwamba tunahimizwa kufanya chaguzi za aina moja ama nyingine.

Ili kufanya chaguzi za hekima, alishauri, tunahitaji ujasiri—"ujasiri wa kusema hapana, ujasiri wa kusema ndio. Maamuzi huamua hatima."[1]

Katika dondoo zifuatazo, Rais Monson anawakumbusha Watakatifu wa Siku za Mwisho kwamba wanahitaji ujasiri kusimama kwa ajili ya ukweli na haki, ili kutetea kile wanachoamini, na kukabiliana na ulimwengu ambao unakataa maadili na kanuni za milele.

"Wito wa ujasiri huja kila mara kwa kila mmoja wetu, alisema. Imekuwa hivyo, na hivyo ndivyo itakavyokuwa milele."[2]

Ujasiri Huleta Idhini ya Mungu

Sote tutakabiliwa na hofu, tutafanyiwa kejeli, na kukutana na upinzani. Sisi,—sisi sote—tuwe na ujasiri wa kwenda kinyume na yanayokubalika, ujasiri wa kusimama kwa ajili ya kanuni. Ujasiri, kuto kubali maovu, huleta tabasamu ya idhini ya Mungu. Ujasiri huwa adili hai na ya kuvutia unapochukuliwa si tu kama kutaka kufa kiume lakini pia kama uamuzi wa kuishi vyema. Tunaposonga mbele, tukijitahidi kuishi kama tunavyopaswa, hakika tutapata usaidizi kutoka kwa Bwana na tunaweza kupata faraja katika maneno Yake."[3]

Shinda kwa Ujasiri

"Nini maana ya kustahimili? Ninapenda maana hii: *kushinda kwa ujasiri.* Ujasiri unaweza kuhitajika kwako katika kuamini; utahitajika wakati mwingine unapotii. Kwa hakika utahitajika zaidi kadiri unavyo stahimili hadi siku ile utakapoondoka katika maisha haya ya duniani."[4]

Kuwa na Ujasiri wa Kusimama kwa ajili ya Ukweli

"[Na] uwe na ujasiri wa kusimama imara kwa ajili ya ukweli na haki. Kwa sababu mwenendo katika jamii ya leo uko mbali na maadili na kanuni ambazo Bwana ametupa, bila shaka utaitwa utetee yale ambayo unayaamini. Isipokuwa mizizi ya ushuhuda wako imepandwa imara, itakuwa vigumu kwako wewe kustahimili kejeli ya wale wanaoijaribu imani yako. Ukiwa umepandwa imara, ushuhuda wako wa injili, wa Mwokozi, na wa Baba yetu wa Mbinguni utashawishi yote unayoyafanya katika maisha yako."[5]

Tunahitaji Ujasiri wa Kiroho na wa Maadili

"Ujumbe unao onyeshwa kwenye televisheni, katika sinema, na katika vyombo vingine vya habari [leo] mara nyingi sana uko kinyume kabisa na ule ambao tunataka watoto wetu waupokee na waushikilie kwa dhati. Ni wajibu wetu, si tu kuwafundisha kuwa imara katika mafundisho na katika roho lakini pia kuwasaidia kukaa hivyo, bila kujali nguvu za nje wanazoweza kupambana nazo. Hii itahitaji muda na juhudi nyingi kwa upande wetu—na ili kuwasaidia wengine, sisi wenyewe tunahitaji ujasiri wa kiroho na kimaadili ili kustahimili mabaya tunayoona kila upande."[6]

Tuweze Daima Kuwa Wajasiri

"Tunapoendelea kuishi siku baada ya siku, ni dhahiri kabisa kwamba imani yetu itapata changamoto. Tunaweza saa zingine kujikuta tumezungukwa na watu wengine na bado tukiwa tumesimama katika wale wachache ama hata kusimama pekee yetu kuhusu kile ambacho kinakubalika na kile ambacho hakikubaliki.

Na tuweze daima kuwa wajasiri na tuliojitayarisha kusimama kwa ajili ya yale tunayoamini, na ikiwa lazima tusimame pekee yetu katika mchakato huu, tuweze kufanya hivyo kwa ujasiri, tukiwa tumeimarishwa na ufahamu kwamba kwa ukweli kamwe hatuko pekee yetu tunaposimama na Baba yetu aliye Mbinguni."[7] ■

KUFUNDISHA KUTOKANA NA UJUMBE HUU

Unaweza kuwauliza wale unaowafundisha kufikiria hali katika wiki ijayo—nyumbani, kazini, shuleni, au kanisani—ambayo itawahitaji wao kutenda kwa ujasiri. Huenda wakakabiliwa na hofu, wakastahmili changamoto fulani, wakasimama kwa ajili ya imani yao, au wakaamua kutii kanuni ya injili kwa kikamilifu zaidi. Waalike watoe mawazo yao au wayaandike.

MUHTASARI

1. Thomas S. Monson, "The Three Rs of Choice", *Liahona,* Nov. 2010, 67, 68.
2. Thomas S. Monson, "Wito wa Ujasiri", *Liahona,* Mei 2004, 55.
3. Thomas S. Monson, "Kuwa Imara na Mwenye Ujasiri Mwema", *Liahona,* Mei 2014, 69.
4. Thomas S. Monson, "Amini, Tii, na Stahmili", *Liahona,* Mei 2012, 129.
5. Thomas S. Monson, "Uweni na Ujasiri", *Liahona,* Mei 2009, 126.
6. Thomas S. Monson, "Malengo Matatu Kukuongoza", *Liahona,* Nov. 2007, 118–19.
7. Thomas S. Monson, "Thubutu Kusimama Peke Yako", *Liahona,* Nov. 2011, 60, 67.

KIELELEZO NA ISTOCK / THINKSTOCK

Sarah wa Mtu Mwingine

Na McKenzie Miller

Nilikuwa ninaona vigumu kutumia imani yangu kama jibu la swali rahisi kama vile "Kwa nini haunywi kahawa"? Katika siku za nyuma nilikuja na visingizio kama vile Ni chungu sana ama sipendi ladha yake.

Je, ni kwa nini nilikuwa naona aibu? Kwa nini nilikuwa na hofu sana kusimama kwa ajili ya kile nilichoamini? Nikitazama nyuma sasa, Sielewi hasa kile nilichohofia. Lakini ninakumbuka hasa wakati nilipokoma kujificha nyuma ya visingizio.

Siku moja katika darasa langu la Kiingereza la shule ya sekondari, mwalimu alitangaza kwamba tungekuwa tunatazama kipindi cha televisheni nilijua sikuwa ninapaswa kukitazama. Wakati wanafunzi wengine wakishangilia kwa furaha, mwana darasa mwenzangu Sarah aliinua mkono wake na kuomba kama angeweza kuondoka.

Wakati mwalimu alipomwuliza ni kwa nini, Sarah alijibu kwa kusema ukweli, "Kwa sababu mini ni Mmormoni na huwa sitazami sinema za lugha chafu."

Ujasiri wake kusimama mbele ya darasa ulikuwa wa ajabu. Shukrani kwa Sarah, mimi pia nilisimama na kusubiri nje kwa dhamiri safi hadi sinema ikaisha.

Nilibadilishwa milele. Nilianza kuelezea imani yangu badala ya kuepuka mada hiyo. Na kwa sababu ya hayo, nilipata kujiamini na nilishiriki zaidi katika shughuli za Kanisa na shuleni.

Sikuwahi kumwaambia Sarah jinsi nilvyouthamini mfano wake, lakini ninajaribu kuiga mfano wake wa ujasiri. Sasa ninatambua kwamba kuwa muumini wa Kanisa la Mungu zuri na takatifu, hakika si jambo la kuonea aibu. Ninatumaini kwamba ninaweza, kupitia mfano wangu, kuwa Sarah wa mtu mwingine.

Mwandishi anaishi Utah, Marekani.

WATOTO

Ujasiri katika Maandiko

Rais Monson anatufundisha kuwa na ujasiri na kusimama kwa ajili ya kile tunachoamini. Kuna mifano mingi katika maandiko ya watu walioonyesha ujasiri. Soma maandiko kando ya kila jina. Watu hawa walionyeshaje ujasiri na kusimama kwa ajili ya kile walichokijua kuwa sahihi? Tumia nafasi kuandika ama kuchora picha ya majibu yako.



PICHA NA ISTOCK/THINKSTOCK

Kwa maombi jifunze maneno haya na utafute kujua kitu cha kueleza. Je ni kwa namna gani kuelewa maisha na nafasi za Mwokozi kunaweza kuongeza imani yako Kwake na kuwabariki wale unaowaongoza kupitia ualimu wa kutembelea? Kwa taarifa zaidi, nenda kwenye ***www.reliefsociety.lds.org****.*

Sifa za Yesu Kristo: Bila Hila ama Unafiki

Hii ni sehemu ya mfululizo wa Ujumbe wa Ualimu wa Kutembelea zinazoonyesha sifa za Mwokozi.

Kuelewa kwamba Yesu Kristo hana hila wala unafiki kutatusaidia sisi kujitahidi kwa uaminifu kufuata mfano wake. Mzee Joseph B. Wirthlin (1917–2008) wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili alisema: "Kulaghai ni kudanganya au kupotosha. Mtu asiye na hila ni mtu asiye na hatia, mwenye dhamira aminifu, na nia safi, ambaye maisha yake yanaonyesha matendo rahisi yanayothibitisha vitendo vyake vya kila siku na kanuni za uadilifu. Naamini umuhimu wa waumini wa Kanisa kuwa bila hila kunaweza kuhitajika zaidi sasa kuliko wakati mwingine kwa sababu wengi katika dunia hii wanaonekana hawaelewi umuhimu wa maadili haya."[1]

Juu ya unafiki, Rais Dieter F. Uchtdorf, Mshauri wa Pili katika Urais wa Kwanza, alisema: "Hakuna yeyote miongoni mwetu ambaye yu kabisa kama Kristo kama tunavyojua tunapaswa kuwa. Lakini tunatamani kwa dhati kushinda makosa yetu na tamaa ya kutenda dhambi. Kwa moyo na nafsi yetu tunatamani kuwa bora zaidi kwa msaada wa Upatanisho wa Yesu Kristo."[2]

"Tunajua tutahukumiwa kulingana na matendo yetu, tamaa za mioyo yetu, na aina ya watu ambao tumekuwa."[3] Hata hivyo tunpojitahidi kutubu, tutakuwa wasafi zaidi—"na heri wenye moyo safi: maana watamwona Mungu" (Mathayo 5:8).

Maandiko ya Ziada

Zaburi 32:2; Yakobo 3:17; 1 Petro 2:1–2, 22

Zingatia Hili

Tunaweza kujifunza nini kutoka kwa watoto wadogo kuhusu kuwa bila hila? (Ona Guide to the Scriptures, Guile.)

MUHTASARI

1. Joseph B. Wirthlin, "Bila Hila," *Ensign,* Mei 1988, 80, 81.
2. Dieter F. Uchtdorf, Njoo, Jiunge Nasi, *Liahona,* Nov. 2013, 23.
3. *Handbook 2: Administering the Church* (2010), 8.1.3.

Imani, Familia, Usaidizi

Kutoka katika Maandiko

Watoto wadogo hawana hila. Yesu Kristo alisema: "Waacheni hao watoto waje kwangu, wala msiwazuie, kwa maana watoto kama hawa ufalme wa Mungu ni wao. Akawakumbatia [watoto] akawaweka mikono yake juu yao, akawabariki" (Marko 10:14, 16).

Kristo pia aliwahudumia watoto katika Amerika baada ya Kusulibiwa Kwake. Aliamuru kwamba watu wawalete watoto wao wadogo Kwake na "kuwaweka chini juu ya ardhi kumzunguka, na Yesu alisimama kati,

[Na] alilia, na umati ulishuhudia hii, na akachukua watoto wao wachanga, mmoja mmoja, na kuwabariki, na kuomba kwa Baba juu yao. . . .

Na walipotazama kuona walielekeza macho yao mbinguni, na wakaona malaika wakiteremka kutoka mbinguni kama wakiwa katikati ya moto; na walikuja chini na kuzunguka wale wachanga, na malaika waliwahudumia" (3 Nefi 17:12, 21, 24).

NGUVU YA IMANI

Na Amber Barlow Dahl

Kama Baba wa Mbinguni angetuondolea changamoto zetu kwa sababu tu tumemwomba, Angekuwa anatunyima sisi kujifunza mambo muhimu sana kwa ajili ya wokovu wetu.

Mwaka mmoja katika chuo, nilikuwa ninafanya mtihani wakati shingo yangu ilianza kuuma. Maumivu hayakupotea wakati wasiwasi wa mtihani ulipopita. Niliwaona madaktari na wataalamu wa matibabu na kujaribu aina mbali mbali za tiba, lakini bado maumivu yaliendelea. Mwaka uliofuata, nilipojitahidi kukabiliana na maumivu haya, nilijitahidi pia kuongeza imani yangu. Nilitumia muda mwingi katika maombi, nilisoma maandiko, na niliomba baraka za ukuhani. Nilihisi kwamba kama tu ningekuwa na imani ya kutosha, ningeponywa.

Yesu Kristo aliwaponya wagonjwa, vipofu, viwete, walio na ukoma—"kulingana na imani [yao]" (Mathayo 9:29). Nilijua alikuwa na nguvu ya kuniponya mimi kama Alivyokuwa amewaponya wengine wengi wakati wa maisha yake duniani. Nilihitimisha, kwa hiyo, kwamba ukosefu wangu wa imani tu ndio ulionizuia kuponywa, hivyo basi niliongeza juhudi zangu. Nilipoendelea na tiba ya mwili, nilisali na kufunga na kusoma na kuamini. Hata hivyo maumivu yangu yaliendelea.

Maandiko yanatufundisha kuwa kwa imani tunaweza kufanya miujiza (ona Mathayo 17:20), lakini bado sikuweza kuondolewa mateso haya madogo. Je, nguvu katika imani yangu ilikuwa wapi? Hatimaye, kimya kimya nilikubali hali yangu, nikapata njia za kukabiliana na maumivu yangu, na nikawa nimetoshelezwa kwa kuweka ufahamu kamili wa imani na uponyaji kwa wakati ujao.

Miaka mingi baadaye nilikuwa ninazungumza na rafiki ambaye alikuwa ameteseka na kichefuchefu kibaya kilichokuwa kimempelekaa hospitalini zaidi ya mara moja wakati wa ujauzito wake wa kwanza. Erin alitaka kuwa na mtoto mwingine, lakini alitishwa na hofu kwamba huenda angepitia maumivu yale yale aliyokuwa amepitia wakati wa ujauzito wake wa kwanza. Aliniambia kuwa alikuwa akifunga na kusali na kwamba aliamini kwamba kweli Baba wa Mbinguni hangemwomba apitie tena kwa mara ya pili.

Tulipokuwa tunazungumza, nilikumbuka maandiko, "Tulia, na ujue kuwa Mimi ni Mungu" (Zaburi 46:10). Nilifikiria kuhusu uzoefu wangu mwenyewe katika kujifunza kutulia katkati ya mateso na nikamuhimiza Erin aendelee kuwa na imani lakini asiifanye imani hiyo itegemee kuwapo ama kutokuwapo kwa kichefuchefu wakati wa ujauzito wake ujao.

Nilipokuwa nikieendelea kujifunza kanuni ya imani, nilifungua hotuba ya Alma juu ya imani ambapo anafundisha kwamba "kama mkiwa na imani mna tumaini katika mambo ambayo hayaonekani, ambayo ni ya kweli" (Alma 32:21).

Nikitafakari maandiko, niligundua kwamba imani haikuwa kile nilichofikiri ilikuwa. Imani, Alma anatufundisha, ni matumaini katika kanuni ya kweli. Kuwa na imani haimaanishi

KUSHINDA MAJARIBIO

"Je, hakuna hekima katika [Baba wa Mbinguni] kutupa sisi majaribio ili tuweze kuyashinda, majukumu ili tupate kuyafikia, kazi ili tushupaze misuli yetu, huzuni ili kuzijaribu nafsi zetu? Je! Hatujaachwa kukabili majaribu ili kupima uwezo wetu, magonjwa ili tujifunze uvumilivu, kifo ili tuweze kuwa na maisha ya milele na walio tukuka?

"Kama wagonjwa wote ambao tunawaombea wangeponywa, kama wenye haki wote wangelindwa na waovu kuangamizwa, mpango mzima wa Baba ungepotea bure, na kanuni ya msingi ya injili, haki ya kujiamulia, ungemalizika. Hakuna mtu angelazimika kuishi kwa imani."

Raisi Spencer W. Kimball (1895–1985), *Teachings of Presidents of the Church: Spencer W. Kimball* (2006), 15.

kwamba tunaamini Baba yetu wa Mbinguni daima atatupatia kile tunachoomba wakati tunapokiomba. Kuwa na imani kwamba Kristo angeniponya shingo yangu au Yeye angempa Erin wakati wa ujauzito usio na kichefuchefu si kuwa na imani katika kanuni ya kweli. Hata hivyo, tunaweza kuwa na imani kwamba Kristo ana nguvu za kuponya, kwamba anatujali, kwamba atatuimarisha, na kwamba tukistahimili vyema, tutaweza kustahili uzima wa milele.

Bwana aliahidi, "Chochote utakachoomba kwa imani, ukiamini kwamba utapokea kwa jina la Kristo, utakipokea" (Enoshi 1:15). Naamini nguvu katika ahadi hii ipo katika ushauri wa kuamini "katika jina la Kristo". Kidahizo katika Kamusi ya Biblia hutufundisha: "Tunasali kwa jina la Kristo wakati mawazo yetu ni mawazo ya Kristo, na matakwa yetu ni matakwa ya Kristo—ikiwa maneno yake yanakaa ndani yetu (Yohana 15:7). Ndipo sisi tunapoomba vitu ambavyo Mungu anaweza kutupatia. Mara nyingi hubaki bila kujibiwa kwa sababu hayako katika jina la Kristo hata kidogo; hayawakilishi kwa njia yoyote mawazo Yake, lakini yanatokana na uchoyo wa moyo wa binadamu."

Tunapoomba kwa imani kitu ambacho kinalingana na mapenzi ya Mungu, Atatupatia kulingana na hamu zetu. Baba wa Mbinguni anatujua, anatupenda, na anataka kila kitu muhimu kwa ajili yetu ili kurudi katika uwepo wake. Na wakati mwingine hiyo hujumuisha majaribu, matatizo na changamoto (ona 1 Petro 1:7). Kama Baba wa Mbinguni angetuondolea changamoto zetu kwa sababu tu tumemwomba, angekuwa anatunyima sisi kujifunza mambo yaliyo muhimu sana kwa ajili ya wokovu wetu. Sharti tujifunze kuamini katika mpango wa Mungu kwa ajili yetu na kuyaweka mapenzi yetu chini ya mapenzi Yake. Tunapoweka matakwa yetu sambamba na matakwa Yake na kukiri utegemezi wetu kamili juu Yake, tunaweza kustahili kupokea "mwisho wa imani [yetu], hata wokovu wa roho [zetu]" (1 Petro 1:9). ■

Mwandishi anaishi Oregon, Marekani.

JIONI YA FAMILIA NYUMBANI—MNAWEZA KUIFANYA!

Haidhuru familia yako ikoje, jioni ya familia nyumbani inaweza kuwabariki na kuwaimarisha.

Baba anafika nyumbani akiwa amechoka baada ya siku ndefu kazini na huwakuta wengine katika familia yake wakihangaika na hisia hizo za uchovu. Ni Jumatatu usiku, na kufanya jioni ya familia nyumbani kunaonekana kutowezekana. Baada ya kusema sala kwa ajili ya msaada, baba na mama wanaamua kufanya mambo kwa urahisi. Wanaita familia yao pamoja, wanaimba wimbo, na kusali pamoja. Wanampa kila mwana familia mshumaa mdogo kuwasha huku wakielezea kuhusu jambo lililowavutia hivi karibuni. Katika chumba kilicho na giza, mwanga wa mishumaa unawakilisha uvuvio na unalenga usikivu wa watoto. Shuhuda zinapokuwa zikitolewa, hisia ya amani tamu na upendo zinaingia nyumbani. Familia inakamilisha usiku kwa shukurani kwamba wamefanya jioni ya familia.

Je, unajua kwamba jioni ya familia nyumbani imekuwa mpango wa Kanisa kwa miaka 100? Mnamo Aprili 1915, Urais wa Kwanza uliwaagiza waumini watenge usiku mmoja kila wiki kwa ajili ya sala ya familia, muziki, kujifunz injili, hadithi, na shughuli nyinginezo. (Ona ukurasa 80 kwa dondoo kutoka barua ya Urais wa Kwanza.) Manabii wanaendelea kutukumbusha umuhimu wa jioni ya familia nyumbani. "Hatuwezi kumudu kupuuza mpango huu wa maongozi kutoka mbinguni, Rais Thomas S. Monson alisema. Unaweza kuleta ukuaji wa kiroho kwa kila mwana familia, kumsaidia kuhimili vishawishi ambavyo vipi kila mahali."[1]

Hapa ni baadhi ya fikra za kukumbuka unapoifanya jioni ya familia nyumbani kuwa sehemu yako ya wiki:

Hii inahusika na mimi. "Jioni ya familia nyumbani ni kwa kila mtu," alisema Mzee L. Tom Perry wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili.[2] "Sisi sote—tuliooa ama bado, tulio na watoto au la—tunaweza kutoa muda kuimarisha familia na kujifunza injili".

Naweza kupata muda. Kanisa linaweka mfano kwa kuacha Jumatatu usiku kuwa bila shughuli za Kanisa. Unaweza kumwoonyesha Bwana na familia yako kuwa uko tayari kutenga muda kwa kile kilicho cha muhimu zaidi.

Naweza kupata kile kinachowezekana kwa familia yangu. Kama familia yako imetengwa kijiografia, jaribu jioni ya familia kupitia intaneti na zungumza na wanafamilia kupitia intaneti au kwenye simu. Je, kuna mtu anayelazimika kufanya kazi hadi usiku sana? Fanya jioni ya familia nyumbani kwenye bustani" iliyo karibu na kazini wakati wa mapumziko. Baba aliyekuwa ameachwa na mke alifanya jioni ya familia kupitia barua kila Jumatatu, akiwaandikia watoto wake ambao waliishi mbali.[3] Fanya vikwazo viwe kichocheo kwa ajili ya ubunifu zaidi.

Naweza kuanza wiki hii. Jioni ya familia nyumbani inaweza kupangwa kulingana na mahitaji na hali ya nyumba yako. Hapa kuna baadhi ya mapendekezo kwa ujumla:

- Anza na umalize kwa sala.
- Tumia muziki, ikiwa ni pamoja na nyimbo za kanisa na nyimbo za Watoto.
- Jifunze kutoka katika maandiko na manabii wa kisasa.
- Jumuisha aina mbali mbali ya michezo, miradi ya huduma, na shughuli zilizojengeka katika misingi ya injili wiki baada ya wiki.
- Pateni Burudani! Cheza mchezo au tayarisha viburudisho.
- Fanyeni mfululizo. Kama huwezi kufanya Jumatatu, tafuteni siku nyingine ambayo inawezekana.

Nataka baraka. Manabii wameahidi kwamba endapo tukishiriki katika jioni ya familia nyumbani, baraka kubwa itatokea: Upendo na

PICHA YA KIHISTORIA KWA HISANI YA CHUO KIKUU CHA BRIGHAM YOUNG, PICHA YA RANGI NA ISTOCK / THINKSTOCK

utiifu nyumbani utaongezeka. Imani itakua katika mioyo ya vijana. Familia "itapata nguvu ya kupambana na athari mbaya na majaribu yanayo wazingira" wao.[4]

Huku jioni zako za familia nyumbani inawezekana zisiwe matukio safi kila wakati, familia yako itaimarishwa na kubarikiwa kwa sababu ya juhudi zako. "Kila jioni ya familia nyumbani ni alama kwenye turubai la roho zetu", Mzee David A. Bednar wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili alifundisha. "Hakuna tukio moja linaloweza kuonekana kuwa la kuvutia sana au kukumbukwa. Lakini kama vile tu alama za rangi zinavyo kamilishana vyema na kuzalisha picha inayovutia, hivyo pia msimamo wetu wa kufanya mambo yanayoonekana kuwa madogo kunavyoweza kusababisha matokeo muhimu ya kiroho."[5] ■

MUHTASARI

1. Thomas S. Monson, "Constant Truths for Changing Times, *Liahona,* Mei 2005, 19.
2. L. Tom Perry, "Therefore I Was Taught, *Ensign,* Mei 1994, 38.
3. "Family Home Evening: Any Size, Any Situation," *Ensign,* Dec. 2001, 42.
4. First Presidency, katika James R. Clark, comp., *Messages of the First Presidency of The Church of Jesus Christ of Latter-day Saints,* 6 vols. (1965–75), 4:339.
5. David A. Bednar, "More Diligent and Concerned at Home", *Liahona,* Nov. 2009, 19–20.

TOA KIPAUMBELE CHA JUU

"Tunawashauri wazazi na watoto kuvipa kipaumbele sala ya familia, jioni ya familia nyumbani, kujifunza injili na maelekezo yake, na burudani nzuri za kifamilia. Licha ya ustahili na usahihi wa mahitaji na shughuli zingine zilivyo, zisiruhusiwe kubadilisha majukumu ya kiungu yaliyotolewa ambayo wazazi na familia pekee ndio wanaoweza kufanya vyema."

Barua ya Urais wa Kwanza, Feb. 11, 1999.

AMEFUFUKA

Imani thabiti katika Kristo ndiyo haja muhimu zaidi ya dunia ya leo.

Na Rais David O. McKay (1873–1970)
Rais wa Tisa wa Kanisa

David O. McKay alizaliwa Septemba 8, 1873. Alitawazwa kuwa Mtume mnamo Aprili 9, 1906, akiwa na umri wa miaka 32, na Aprili 9, 1951, alikubaliwa kama Rais wa Tisa wa Kanisa. Ifuatayo ni dondoo kutoka katika hotuba aliyoitoa katika mkutano mkuu wa Aprili 1966. Kwa hotuba kamili, ona Conference Report, Apr. 1966, 55–59.

Ikiwa muujiza ni tukio lisilo la kawaida ambalo nguvu iliyosababisha ina shinda hekima iliyo na kipimo cha binadamu, basi Ufufuko wa Yesu Kristo ni muujiza mkuu zaidi kwa wakati wote. Ndani yake kunafunuliwa ukuu wa Mungu na kutokufa kwa binasdamu.

Ufufuo ni muujiza, hata hivyo, katika maana tu kwamba upo nje ya ufahamu na uelewa wa binadamu. Kwa wale wote ambao wanaukubali kama kweli, ni ishara tu ya sheria sare ya maisha. . . .

Ithibitishe kama ukweli kwamba Kristo hakika aliuchukua mwili wake na kuonekana kama kiumbe aliyetukuzwa, aliyefufuliwa, na unajibu swali la wakati wote: "Kama mtu akifa, je, ataishi tena" (Ayubu 14:14).

Mashahidi wa Ufufuo

Kwamba ufufuo halisi wa Kristo kutoka kaburini ulikuwa hakikisho kwa wanafunzi ambao walimjua Yeye kwa undani kwamba ni uhakika. Katika mawazo yao hapakuwa na shaka kabisa. Walikuwa mashahidi wa ukweli; walijua maana macho yao yaliona, masikio yao yalisikia, mikono yao iligusa uwepo wa mwili wa Mkombozi aliyefufuka.

Petro, Mtume mkuu, katika tukio wakati wale kumi na mmoja walipokutana ili kumchagua mmoja kuchukua nafasi ya Yuda Iskarioti, alisema, "Basi katika watu hawa lazima mmoja awe shahidi pamoja nasi juu ya kufufuka kwake" (Matendo 1:21–22).

Katika tukio jingine Petro alitangaza mbele ya adui zao, watu wale wale ambao walikuwa wamemuua Yesu msalabani; "Enyi waume wa Israeli, sikilizeni maneno haya! Yesu huyo Mungu alimfufua, na sisi sote tu mashahidi wake" (Matendo 2:22, 32).

Mashahidi wa Ziada

Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho linasimama na Petro, na Paulo, na Yakobo, na pamoja na Mitume wale wengine wote wa awali waliokubali Ufufuo si tu kama kuwa hakika kweli, lakini kama ukamilifu wa ujumbe mtukufu wa Kristo duniani.

Miaka elfu moja mia nane baada ya Yesu kufa msalabani, Nabii Joseph Smith alitangaza kwamba Bwana aliyefufuka alimtokea yeye, akisema: "Niliwaona Viumbe Wawili, ambao uangavu na utukufu wao ulishinda maelezo yote, wamesimama juu yangu angani. Mmoja wao akaniambia, akiniita mimi kwa jina na kusema, huku akimwonyesha yule mwingine—"*Huyu ni Mwanangu Mpendwa. Msikize Yeye!*" (Joseph Smith—Historia 1:17). . . .

Ikiwa ushuhuda wa Joseph Smith ulisimama peke yake, ungekuwa, kama vile Kristo alivyosema kuhusu ushahuda wake wakati alipojisemea Mwenyewe, hauna maana yoyote, lakini Yesu alishuhudiwa na Mungu na Mitume. Na Joseph Smith alikuwa na mashahidi wengine [ambao] walithibitisha ushuhuda [wake], ukweli ambao ulijulikana kwao kutokana na malaika Moroni kujitokeza kwao. . . .

Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho [pia] linatangaza ono tukufu la Nabii Joseph Smith:

"Na sasa, baada ya ushuhuda

KRISTO ALIYE HAI

Soma ushuhuda wa Yesu Kristo ulisotolewa na mitume na manabii wa kisasa katika *Liahona,* Apr. 2000, 2–3.

KUSHOTO: PICHA NA DAVID STOKER, *BEHOLD MY HANDS*, NA JEFF WARD

mwingi uliokwisha kutolewa juu yake, huu ni ushuhuda, wa mwisho wa zote, ambao tunautoa juu yake: Kwamba yu hai!" M&M 76:22).

Katika mwanga wa shuhuda kama hizi zisizoweza kukanushwa kama zilivyotolewa na Mitume wa kale—shuhuda zinazoanza miaka michache baada ya tukio lenyewe—katika mwanga wa ufunuo wa ajabu zaidi katika wakati huu wa Kristo aliye hai, inaonekana vigumu kweli kuelewa jinsi watu bado wanaweza kumkataa Yeye na wanaweza kuwa na shaka kuhusu kutokufa kwa mwanadamu.

Ni nini Tunachohitaji Leo

Imani thabiti katika Kristo ndiyo haja muhimu zaidi ya dunia ya leo. Ni zaidi ya hisia tu. Ni nguvu inayosababisha kutenda, na inapaswa iwe katika maisha ya binadamu nguvu ya kushawishi ya msingi zaidi ya zote. . . .

Ikiwa watu wangetenda tu mapenzi Yake, badala ya kutazamia bila tumaini katika kaburi iliyo giza na huzuni, wangegeuza macho yao yatazame mbinguni na kujua kwamba "Kristo amefufuka!" . . .

Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho linatangaza kwa ulimwengu wote kwamba Kristo ni Mwana wa Mungu, Mkombozi wa ulimwengu! Hakuna mfuasi wa kweli anayeridhika na kumkubali Yeye kama tu mleta mabadiliko mkubwa, mwalimu bora, au hata kama mtu mmoja mkamilifu. Mtu wa Galilaya—si kwa kuashiria, lakini *hahika ni*—Mwana wa Mungu aliye hai.

Hakika Kuzaliwa Upya

Hakuna mtu anayeweza kwa dhati kutumia katika maisha yake ya kila siku mafundisho ya Yesu wa Nazareti bila kuhisi mabadiliko katika maisha yake yote. Kifungu kuzaliwa tena kina maana ya ndani zaidi kuliko kile ambacho watu wengi hudhania kuwa. Ana furaha mtu yule ambaye kwa kweli amehisi nguvu yenye kuinua, kubadilisha inayokuja kutokana na ukaribu huu kwa Mwokozi, ujamaa huu kwa Kristo aliye hai. Ninashukuru kwamba ninajua ya kuwa Kristo ni Mkombozi wangu. . . .

Ujumbe wa Ufufuko ni wa faraja sana, wa utukufu zaidi ambao kamwe haujawahi kutolewa kwa mwanadamu, kwani wakati kifo kinapomchukua mpendwa mmoja kutoka kwetu, mioyo yetu inayohuzunika huinuliwa na tumaini na uhakika wa kiungu unaoelezwa katika maneno haya: "*Hayuko hapa; kwani amefufuka!*" [ona Mathayo 28:6; Marko 16:6].

Kwa moyo wangu wote najua kwamba Yesu ameshinda mauti, na kwa sababu Mkombozi wetu anaishi, ndivyo sisi pia. ■

Vichwa vidogo vimebadilishwa; herufi kubwa na vituo vya uandishi vimesawazishwa.

USHAWISHI WA KIROHO WA

"Tunawaita wanawake wa Kanisa ili kusimama pamoja kwa haki. Ninaona hii kama tumaini moja linalong'ara katika dunia." —President Gordon B. Hinckley (1910–2008)

WANAWAKE

MABINTI WA MUNGU, NA KATHLEEN PETERSON, ISINAKILIWE

Je, tunajua uwezo wa nguvu zetu za kiroho?

Na Starla Awerkamp Butler

Wanawake wengi, wanyenyekevu katika Kanisa hutoa huduma ya kujitolea bila kutambua athari ya kina ambayo hutokana na maisha yao kuwa—kama mifano ya huduma ya kidunia, lakini pia kama urithi wa nguvu za kiroho. Mmoja wa wanawake hao ni bibi yangu, Cherie Petersen. Amehudumu kwa uaminifu katika miito ya kimya kimya katika maisha yake yote. Ukimuuliza, angedai kwamba hana vipaji vingi vya kutoa kwa dunia. Hata hivyo, nilivyoanza kujifunza kuhusu maisha yake, niligundua kiwango ambacho nguvu yake ya kiroho ilivyoathiri maisha yangu.

Wazazi wa Cherie waliacha kuhudhuria kanisa na wakatalikiana wakati alipokuwa bado mdogo sana, hivyo basi alilelewa na mama, Florence, ambaye alikuwa daima anafanya kazi. Florence alikuwa hata ametelekezwa zaidi akiwa mtoto, kwani alilelewa katika shule za bweni wakati mama yake, Georgia, akiishi maisha ya kilimwengu. Licha ya changamoto katika malezi yake, Cherie alibakia akijishughulisha na injili, kwa uaminifu akihudhuria kanisa na marafiki wa bibi yake mkongwe Elizabeth au na marafiki wengine. Aliona katika familia zao kile alichokitaka kwa familia yake mwenyewe. Hakujua hasa jinsi familia inavyopaswa kuwa, lakini alijua jinsi iisivyopaswa kuwa, na alidhamiria kuwa familia yake ya siku za usoni iwe tofauti.

Mumewe Cherie—babu yangu Dell—wakati mmoja aliniambia, "Ili kuwa na ushuhuda lazima uutake. Cherie daima aliutaka ushuhuda." Ingawa miaka yao ya awali ya ndoa ilijawa na shida, walidhamiria kubaki imara kama familia. Walikuwa hawahudhurii kanisa kila mara katika mwaka wa kwanza wa ndoa yao kwa sababu ya ratiba ya kazi ya Dell, lakini wito kuhudumu kwa Watoto ulisababisha Cherie kuanza kuhudhuria, na Dell punde alijiunga naye kanisani kama mshauri wa akidi ya washemasi.

Wote wamehudhuria kanisani na kuwa imara katika Kanisa tangu wakati huo. Kutaka kwa Cherie kuhudumu na uamuzi wa kujenga familia imara kulimsaidia mamangu kuwa mwanamke mwenye nguvu, na mfano wa mamangu umesaidia kuongoza maisha yangu, hasa ninapoanzisha familia yangu mwenyewe sasa.

Kama wanawake tunaweza kuwa na ushawishi wa kina wa kiroho katika maisha ya wale wanaotuzunguka. Hakika, Joseph Smith alifundisha kwamba jukumu letu "siyo tu kuwasaidia maskini, lakini kuokoa".[1] Yesu Kristo ametoa wito kwa wanawake wa Kanisa Lake kuwa wafuasi wake na kuwa na nguvu kiroho. Nguvu na ushawishi wetu wa kiroho ni muhimu katika maendeleo ya kazi ya wokovu, na tunapaswa tutafute fursa za kuwaimarisha kiroho wanaotuzunguka. Tunapofanya hivyo, ushawishi wa imani na wema wetu utadumu zaidi kupita kile tunachoweza kuona.

Vizazi vinne: Elizabeth (kushoto), akimbeba mjukuu wake Florence. Annie (katikati) alikuja Utah na wazazi wake na ni mama wa Elizabeth. Georgia (kulia) ni bintiye Elizabeth, lakini Georgia na binti yake Florence waliacha Kanisa. Ilikuwa mwaminifu Elizabeth ambaye alisaidia kitukuu chake Cherie na ukoo wa Cherie kurudi katika injili.

Kuitwa Kuwa Wafuasi

Mzee James E. Talmage (1862–1933) wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili aliandika, "shujaa mkuu duniani wa mwanamke na umama ni Yesu Kristo".[2] Fikiria, kwa mfano, juu ya kile alichowafundisha wafuasi Wake wawili wa kike katika Agano Jipya, kina dada Mariamu na Martha. Kitabu *Daughters in My Kingdom* kinaelezea: "Luka 10 kina taarifa ya Martha akifungua nyumba yake kwa Yesu. Alimhudumia Bwana kwa kutekeleza mahitaji yake ya kimwili, na Mariamu alikaa miguuni pa Mwalimu na kupokea mafundisho yake.

Katika umri ambapo wanawake walitarajiwa kwa ujumla kutoa huduma ya kimwili tu, Mwokozi alimfundisha Martha na Mariamu kuwa wanawake pia wangeweza kushiriki kiroho katika kazi Yake. Aliwaalika wawe wanafunzi Wake na kushiriki wokovu, sehemu ile nzuri' ambayo kamwe haitachukuliwa kutoka kwao."[3]

Kama Martha, wakati mwingine sisi hukosea kufikiri kwamba jukumu la msingi la wanawake ni kutoa huduma ya kimwili, kama vile kutoa milo, kushona, na kuwasafishia wengine. Huduma hii ni muhimu na bora kabisa; Hata hivyo, hata zaidi ya anavyo wahitaji kina dada ambao wanaweza kushona na kupika, Bwana anawahitaji wanawake walio na nguvu za kiroho ambao imani, wema na hisani vinang'aa katika maisha yao. Anajua kwamba sote tuna mengi ya kutoa. Yesu Kristo anamwita *kila mmoja* wetu kukuza nguvu zetu za kiroho na uwezo wa kupokea na kutenda juu ya ufunuo wa kusaidia kusogeza kazi Yake mbele. Linda K. Burton, Rais mkuu wa Muungano wa Usaidizi wa Akina Mama, alisema kwa akina dada, "Mmetumwa duniani katika kipindi hiki cha nyakati kwa sababu ya asili yetu na kile mlichoandaliwa kufanya! Bila kujali nini Shetani angejaribu kutushawishi kufikiri kuhusu asili yetu, utambulisho wetu wa kweli ni ule wa mfuasi wa Yesu Kristo!"[4]

Bwana anatujua na hali zetu, na Anayo kazi kwa kila mmoja wetu kufanya katika dunia hii. Hakuna dada anayejua kidogo sana au aliye na vipaji vichache kuwa nguvu ya kiroho kwa ajili ya wema na kuwaleta wengine kwa Kristo. Kwa uwezo huu wa kiungu tuna wajibu wa kuwa viongozi wa kiroho katika nyumba zetu na jumuiya zetu. Mzee M. Russell Ballard wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili alitangaza, "Kila dada katika Kanisa ambaye amefanya maagano na Bwana ana jukumu takatifu la kusaidia kuokoa nafsi, na kuongoza wanawake wa ulimwengu, kuimarisha nyumba za Sayuni, na kujenga ufalme wa Mungu."[5]

Si lazima tuwe katika nafasi za juu au kufanya mambo yasiyo ya kawaida ili kusaidia wale wanaotuzunguka wafanye maamuzi ambayo yatawaelekeza kuwa karibu na Yesu Kristo—ambao ni wajibu wetu muhimu sana. Yote mambo madogo na makubwa tunayofanya katika maisha ya mtu mmoja au wawilii, hata ndani tu ya familia zetu wenyewe, yanaweza kuwa na athari kubwa.

Wanawake katika Kazi ya Wokovu

Wimbo tunaoupenda unaeleza, "Kazi za malaika wamepewa wanawake; Na hii ni zawadi ambayo, kama akina dada, tunaidai."[6] Tuna mengi ya kutoa katika maisha ya

YESU NA MARIA NA MARTHA, NA KATHLEEN PETERSON, PCHA KWA HESHIMA YA MTUNZI DESERET BOOK; PICHA KWA HISANI YA MTUNZI

wale tunaowapenda. Mzee Richard G. Scott wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili amesimulia hadithi ya jinsi nguvu ya kiroho ya wanawake wawili ilivyoathiri maisha yake:

"Nilipokuwa mtoto mdogo, baba yangu hakuwa muumini wa Kanisa na mama yangu alikuwa hahudhurii kanisani. Miezi kadhaa baada ya sikukuu yangu ya nane ya kuzaliwa, Bibi Whittle alikuja kutoka upande wa pili wa nchi kututembelea. Bibi alikuwa na wasiwasi kwamba, mimi na kaka yangu tulikuwa hatujabatizwa. Sijui aliwaambia nini wazazi wangu kuhusu haya, lakini najua kwamba asubuhi moja alimchukua ndugu yangu pamoja na mimi kwenye bustani na kushirikiana nasi hisia zake kuhusu umuhimu wa kubatizwa na kuhudhuria mikutano ya Kanisa kila mara. Sikumbuki yale yote aliyoyasema, lakini maneno yake yalichochea kitu katika moyo wangu, na punde baadaye ndugu yangu pamoja na mimi tulibatizwa. . . .

Mwokozi aliwafundisha Martha na Maria kwamba wanawake wangeweza kushiriki kiroho katika kazi yake. Aliwaalika kuwa wanafuasi wake na kupokea wokovu.

Bibi alitumia kiasi sahihi cha ujasiri na heshima ili kumsaidia baba yetu kutambua umuhimu wake kwa kutuendesha kwenda kanisani kwa ajili ya mikutano yetu. Katika kila njia sahihi, alitusaidia sisi kuona umuhimu wa injili katika maisha yetu".[7]

Chanzo cha pili cha nguvu za kiroho alikuwa mke wa Mzee Scott, Jeanene. Walipokuwa katika matembezi ya kirafiki walianza kuzungumza kuhusu siku zijazo. Jeanene, ambaye alikuwa amelelewa katika nyumba imara ya kimisionari,

MTOTO, NA KATHLEEN PETERSON, ISINAKILIWE

alionyesha hamu yake kuolewa katika hekalu na mmisionari aliyerejea nyumbani. Mzee Scott, ambaye hakuwa amefikiria kuhusu kuhudumu misheni kabla, aliguswa kwa nguvu sana. "Nilienda nyumbani, na sikuweza kufikiria kuhusu kitu chochote kingine. Nilikuwa macho usiku mzima. Baada ya sala nyingi nilifanya uamuzi wa kukutana na Askofu wangu na kuanza maombi yangu ya umisionari".[8] Ingawa Jeanene alimpa uongozi na ushawishi aliohitaji, Mzee Scott alisema, "Jeanene kamwe hakuniomba nihudumu misheni *kwa ajili yake*. Alinipenda vya kutosha kushirikiana nami ushuhuda wake na kisha alinipa fursa ya kuelekeza mwelekeo wa maisha yangu menyewe. Sisi sote tulihudumu misheni na baadaye tuliunganishwa katika hekalu. Ujasiri na msimamo wa Jeanene kwa imani yake ulifanya tofauti yote katika maisha yetu kwa pamoja. Nina uhakika hatungepata furaha tunayoifurahia bila imani yake imara katika kanuni ya kumtumikia Bwana kwanza. Yeye ni mfano wa ajabu, mfano wema!"[9]

Wimbo tunaoupenda unasema, kazi za malaika wamepewa wanawake; Na hii ni zawadi ambayo, sisi kama akina dada tunaidai. Tuna mengi ya kutoa katika maisha ya wale tunaowapenda.

Ilikuwa ushawishi wa kiroho wa hawa malaika wanawake katika maisha yake kwamba walisaidia tu kijana mmoja—Mzee Scott—kufanya baadhi ya maamuzi muhimu katika maisha yake: kubatizwa, kutumikia misheni, na kuoa katika hekalu.

Tunaweza kuwasaidia wengine kufanya maamuzi mazuri kutokana na mfano wetu, matendo, maneno, na wema wetu binafsi. Dada Carole M. Stephens, mshauri wa kwanza katika urais mkuu wa Muungano wa Usaidizi wa Akina Mama, anatangaza, "Sisi ni mabinti wa agano katika ufalme wa Bwana, na tuna fursa ya kuwa vyombo katika mikono yake. Tunashiriki katika kazi ya

wokovu ya kila siku kwa njia ndogo na zilizo rahisi—"kulinda, kuimarisha na kufundishana sisi kwa sisi."[10] Tunapotegemea Roho na kusonga mbele katika juhudi za dhati na nyenyekevu kuwasaidia wale walio karibu nasi kuja karibu na Kristo, tutaongozwa katika kile tunachoweza kufanya na kupatiwa nguvu ya kukifanya, na tutasikia furaha ya kuwaleta watoto wa Bwana Kwake.

Kuwa Ushawishi wa Kiroho

Kujua jukumu letu, tunaweza kuuliza kama wanafunzi wa zamani, "Tutendeje" (Matendo 2:37) ili kuwa na ushawishi wa kiroho? Katika mkutano mkuu wa hivi karibuni, Dada Burton aliwaalika akina dada kufikiria "baadhi ya misaada ya kiroho inayoweza kuwa 'msaada unahitajika' ishara zinazohusiana na kazi ya wokovu:

- Msaada unahitajika: wazazi kulea watoto wao katika mwanga na ukweli
- Msaada unahitajika: binti . . . , akina dada. shangazi . . . , binamu, mababu, na marafiki wa kweli kutumika kama washauri na kutoa mikono ya usaidizi kwenye njia ya agano
- Msaada unahitajika: wale wanaosikiliza ushawishi wa Roho Mtakatifu na kuyatendea kazi mawazo wanayopokea
- Msaada unahitajika: wale wanaoishi injili kila siku kwa njia zilizo ndogo na rahisi
- Msaada unahitajika: wafanyikazi wa historia ya familia na hekalu ili kuunganisha familia milele
- Msaada unahitajika: wamisionari na waumini kueneza habari njema—"injili ya Yesu Kristo"
- Msaada unahitajika: waokozi kuwatafuta wale ambao wamepotea njia yao
- Msaada unahitajika: wanaoshika maagano kusimama imara kwa ajili ya ukweli na haki
- Msaada unahitajika: wafuasi wa kweli wa Bwana Yesu Kristo".[11]

Haya si mambo mapya, lakini wakati tunapotafuta fursa ya kushiriki katika kazi ya wokovu, tutaboresha uwezo wetu wa kuwasaidia wale wanaotuzungukai. Mzee Ballard alisema, "Hakuna kitu katika dunia cha kibinafsi, kama kuwalea, au kama kubadilisha maisha kama ushawishi wa mwanamke mwema."[12] Tunapokuza nguvu zetu za kiroho kwa njia ya sala binafsi na mafunzo ya maandiko, utii imara, na kushika maagano yetu kwa uaminifu, tutakuwa ushawishi huo.

Zaidi ya Kile Tunachoweza Kuona

Rais Brigham Young (1801–1877) alisema, "Je, unaweza kuona kiasi cha wema ambao kina mama na mabinti katika Israeli wanaoweza kufanya? Hapana, haiwezekani. Na wema watakaofanya utawafuata milele."[13]

Maamuzi ya haki ya bibi yangu yameathiri vizazi vya familia yake kupita kile ambacho yeye kama msichana angeweza kukiona. Hata hivyo, ushawishi wa kiroho wa wanawake katika familia yangu unapanuka hata mbali zaidi kurudi nyuma. Cherie alipata sehemu kubwa ya nguvu zake mwenyewe za kiroho kwa kumtazama bibi yake (bibi yangu wa kizazi cha tatu nyuma) Elizabeth. Mfano wa Elizabeth wa imani na ushuhuda ulifika kupita vizazi viwili vya kutohudhuria kanisa ili kumsaidia kitukuu wake Cherie kubadili mwelekeo wa familia zilizovunjika na kurudi katika Kanisa.

Tunapokuwa nguvu ya kiroho kwa wale wanaotuzunguka, ushawishi wetu utafika mbali zaidi ya kile tunachoweza kukiona. Rais Gordon B. Hinckley (1910–2008) alisema, "Tunawaomba wanawake wa Kanisa wasimame pamoja kwa ajili ya wema. Ni lazima waanze katika nyumba zao wenyewe. Wanaweza kufundisha katika madarasa yao. Wanaweza kutoa sauti katika jumuiya zao. . . .

"Ninaona hii kama tumaini moja linalong'aa katika dunia inayoelekea katika kujiangamiza yenyewe."[14]

Tunapotimiza amri hii, kazi ya Bwana itasonga mbele kote katika dunia inayotuzunguka na, muhimu zaidi, katika familia zetu na maisha ya wale tunaowapenda. ■

Mwandishi anaishi Utah, Marekani.

MUHTASARI

1. *Teachings of Presidents of the Church: Joseph Smith* (2007), 453.
2. James E. Talmage, *Jesus the Christ,* 3rd ed. (1916), 475.
3. *Daughters in My Kingdom: The History and Work of Relief Society* (2011), 3–4.
4. Linda K. Burton, "Inahitajika: Mikono na Mioyo ili Kuharakisha Kazi," *Liahona,* Mei 2014, 122–123.
5. M. Russell Ballard, "Wanawake wa Haki," *Ensign,* Apr. 2002, 70.
6. "As Sisters in Zion," *Hymns,* no. 309.
7. Richard G. Scott, "Nimewapa Kielelezo," *Liahona,* Mei 2014, 32.
8. Richard G. Scott, "Nimewapa Kielelezo," 33.
9. Richard G. Scott, "Nimewapa Kielelezo," 33.
10. Carole M. Stephens, "Tuna Sababu Kuu ya Kufurahia," *Liahona,* Nov. 2013, 117.
11. Linda K. Burton, "Inahitajika: Mikono na Mioyo Kuharakisha Kazi," 124.
12. M. Russell Ballard, "Mothers and Daughters," *Liahona,* Mei 2010, 18.
13. *Discourses of Brigham Young,* sel. John A. Widtsoe (1954), 216.
14. Gordon B. Hinckley, "Standing Strong and Immovable," *Worldwide Leadership Training Meeting,* Jan. 10, 2004, 20.

Si DHAMBI KUWA MDHAIFU

JUU: PICHA NA ISTOCK/THINKSTOCK; CHINI: PICHA NA PHOTODISC/THINKSTOCK

Na Wendy Ulrich

"Je ni kweli ninastahili kuingia katika nyumba ya Mungu? Je ninawezaje kuwa kama mimi si mkamilifu?"

"Je, Mungu anaweza kufanya udhaifu wangu kuwa nguvu? Nimefunga na kusali kwa siku nyingi ili tatizo hili liondolewe kutoka kwangu, lakini hakuna dalili ya mabadiliko."

"Katika uwanja wa misheni niliishi injili kwa msimamo zaidi kuliko wakati wowote katika maisha yangu, lakini sijawahi kuwa na ufahamu wa mapungufu yangu. Kwa nini, wakati nilikuwa mzuri sana, nilikuwa najisikia vibaya wakati mwingine?"

Tukitafakari maswali kam hayo, ni muhimu kuelewa kwamba wakati *dhambi* ni dhahiri inatuongoza mbali na Mungu, *udhaifu,* kinyume chake unaweza kutuongoza kuelekea Kwake.

Kutofautisha kati ya dhambi na Udhaifu

Kwa kawaida tunafikiria dhambi na udhaifu kama tu alama nyeusi zenye ukubwa tofauti kwenye kitambaa cha roho zetu, uvunjaji sheria wenye uzito tofauti. Lakini maandiko yanasema kwamba dhambi na udhaifu ni urithi ulio tofauti, vinahitaji tiba tofauti, na vina uwezo wa kuzalisha matokeo tofauti.

Wengi wetu tuna uzoefu na dhambi kuliko tunavyojali kukubali, lakini hebu tupitie upya: Dhambi ni uchaguzi wa kutotii amri za Mungu au uasi dhidi ya Mwanga wa Kristo ndani yetu. Dhambi ni uchaguzi wa kumwamini Shetani zaidi kuliko Mungu, hutuweka katika uadui na Baba yetu. Tofauti na sisi, Yesu Kristo alikuwa hana dhambi kabisa na aliweza kulipia dhambi zetu. Wakati tunapotubu

Udhaifu na mapungufu si dhambi na hayawezi kutuzuia kuwa safi na wenye kustahili kuwa na Roho wa Mungu.

Wakati ni dhahiri dhambi hutuongoza mbali na Mungu, udhaifu, unaweza kutuongoza kuelekea kwake.

kwa dhati—pamoja na kubadilisha akili , moyo na tabia zetu; na kuomba msamaha sahihi au maungamo, tufanye malipo pale inapowezekana, na kutorudia dhambi hiyo siku zijazo—tunaweza kupata Upatanisho wa Yesu Kristo, kusamehewa na Mungu, na kuwa safi tena.

Kuwa safi ni muhimu kwa sababu hakuna kichafu kinachoweza kukaa katika uwepo wa Mungu. Lakini kama lengo letu tu ni kuwa bila hatia kama tulivyokuwa wakati tulipokuwa tunatoka katika uwepo wa Mungu, itakuwa bora zaidi kwetu sote kulala raha musterehe katika hori zetu kwa ajili ya mapumziko maisha yetu yote yaliyosalia. Badala yake, tulikuja duniani kujifunza kwa uzoefu ili kutofautisha mema na mabaya, kukua katika hekima na ujuzi, kuishi maadili ya maisha ambayo tunayajali, na kupata sifa ya utauwa—maendeleo ambayo hatuwezi kuyafanya kutokana na mipaka ya tenga la mtoto.

AHADI YA UPATANISHO

"Kurejesha kile ambacho huwezi kurejesha, uponyaji wa jeraha ambalo huwezi kuponya, kutengeneza kile ambacho ulikivunja na hakiwezi kutengenezeka ndio lengo hasa la upatanisho wa Kristo. . . .

Narudia, isipokuwa kwa wale wachache sana ambao hutorokea kwenye upotevu, hakuna tabia, hakuna madawa ya kulevya, hakuna uasi, hakuna uvunjaji wa sheria, hakuna ukengeufu, hakuna uhalifu, ambao umesamehewa kutokana na ahadi ya msamaha mkamilifiu. Hiyo ni ahadi ya upatanisho wa Kristo."

Rais Boyd K. Packer, Rais wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili, "The Brilliant Morning of Forgiveness," *Ensign*, Nov. 1995, 19–20.

Udhaifu wa kibinadamu una jukumu muhimu katika madhumuni haya muhimu ya hapa duniani. Wakati Moroni alipokuwa na wasiwasi kwamba udhaifu wake wa maandishi ungesababisha watu wa mataifa mengine kudhihaki mambo matakatifu, Bwana alimhakikishia kwa maneno haya:

"Na ikiwa watu watakuja kwangu nitawaonyesha udhaifu wao. Nitawapatia watu udhaifu ili katika udhaifu wao wawe wanyenyekevu, na neema yangu inawatosha watu wote ambao hujinyenyekeza mbele yangu, kwa maana wakijinyenyekeza mbele yangu, na kuwa na imani ndani yangu, ndipo, nitafanya vitu dhaifu kuwa vya nguvu kwao" (Etheri 12:27; ona pia 1 Wakorintho 15:42–44; 2 Wakorintho 12:7–10; 2 Nefi 3:21; na Yakobo 4:7).

Maana ya andiko hili inajulikana ni muhimu sana na hutualika sisi kutofautisha dhambi (inayohimizwa na Shetani) na udhaifu (ilivyoelezwa hapa kama hali "tuliyopewa" na Mungu).

Tunaweza kuelezea udhaifu kama kikwazo kwa hekima yetu, nguvu na utakatifu ambayo inakuja kwa kuwa binadamu. Kama binadamu tunazaliwa wanyonge na tegemezi, tukiwa na dosari mbalimbali za kimwili na kimaelekezo. Tumelelewa na kuzungukwa na binadamu wengine dhaifu, na mafundisho yao, mifano, na wanayotutendea yana dosari na hutuharibu wakati mwingine. Katika udhaifu wetu, hali yetu ya kibinadamu tunapatwa na magonjwa ya kimwili na hisia, njaa, na uchovu. Tunajifunza hisia za binadamu kama hasira, huzuni na hofu. Tumekosa hekima, ujuzi, uthabiti, na nguvu. Na tuko chini ya majaribu ya aina nyingi.

Ingawa alikuwa bila dhambi, Yesu Kristo alijiunga pamoja nasi kikamilifu katika hali dhaifu ya mauti (ona

KUTOFAUTISHA KATI YA DHAMBI NA UDHAIFU

	Dhambi	Udhaifu
Ufafanuzi?	Kutomtii Mungu kwa Makusudi	Upungufu wa kibinadamu, udhaifu
Chanzo?	Himizwa na Shetani	Sehemu ya asili ya mwili wetu wenye kufa
Mifano?	Kuvunja amri za Mungu kwa kujua, kumwamini shetani zaidi ya Mungu	Kuhisi majaribu, hisia, uchovu, ugonjwa wa kimwili au kiakili, ujinga, maelekezo, majeraha, kifo
Je, Yesu alikuwa na?	La	Ndiyo
Jibu letu linapaswa kuwa?	Toba	Unyenyekevu, imani katika Kristo, na jitihada za kushinda
Jibu la Mungu kwa upande?	Msamaha	Neema—nguvu ya kuwezesha
Ambayo ina matokeo katika?	Kusafishwa kutokana na dhambi	Kupata utakatifu, nguvu

2 Wakorintho 13:4). Alizaliwa kama mtoto mchanga mnyonge katika mwili unaoweza kufa na kulelewa na walezi ambao si wakamilifu. Alikuwa ajifunze jinsi ya kutembea, kuzungumza, kufanya kazi, na kupatana vyema na watu wengine. Alipata njaa na uchovu, alihisi hisia za kibinadamu, na angeweza kuwa mgonjwa, kuteseka, kutokwa na damu, na kufa. Alikuwa "katika kila hali mwenye kujaribiwa kama sisi, bado hakuwa na dhambi," alijikabidhi mwenyewe kwenye umauti ili aweze "kuguswa na hisia ya upungufu wetu" na kutusaidia katika upungufu *wetu* au udhaifu wetu (Hebrews 4:15; ona pia Alma 7:11–12).

Hatuwezi tu kutubu kwa kuwa ni wadhaifu—wala udhaifu wenyewe hautufanyi sisi kuwa wachafu. Hatuwezi kukua kiroho isipokuwa *tukatae* dhambi, lakini pia hatuwezi kukua kiroho isipokuwa *tukubali* hali yetu ya udhaifu wa kibinadamu, kujibu kwa unyenyekevu na kwa imani, na kujifunza kupitia udhaifu wetu kumwamini Mungu. Wakati Moroni alipokuwa na wasi wasi kuhusu udhaifu wa maandishi yake, Mungu hakumuambia atubu. Badala yake, Bwana alimfundisha kuwa mnyenyekevu na kuwa na imani katika Kristo. Tunapokuwa wapole na waaminifu, Mungu hutoa neema—si msamaha—kama dawa ya udhaifu. Kamusi ya Biblia inaeleza neema kama nguvu yenye kutuwezesha itokayo kwa Mungu ili tuweze kufanya kile ambacho hatuwezi kujifanyia wenyewe (tazama kamusi ya Bibilia, "Neema")—tiba sahihi ya kiungu ambayo kwayo anaweza kufanya "vitu dhaifu kuwa vyenye nguvu."

Kutumia Unyenyekevu na Imani

Kutoka mapema katika uzoefu wetu Kanisani, tunafundishwa mambo muhimu ya toba, lakini jinsi gani hasa tunaweza kuendeleza unyenyekevu na imani? Zingatia yafuatayo:

- **Tafakari na kusali.** Kwa sababu sisi ni wadhaifu, inawezakana tukakosa kutambua kama tunashughulika na *dhambi* (wito wa haraka ni kuenea kwa mabadiliko ya mawazo, moyo, na tabia) au *udhaifu* (wito wa unyenyekevu, juhudi endelevu, kujifunza, na kuboresha). Jinsi gani tunavyoangalia mambo haya inaweza kutegemea malezi na ukomavu wetu. Kunaweza hata kuwa na mambo yote mawili ya dhambi na udhaifu katika tabia moja. Kusema dhambi hakika kuwa ni udhaifu hutuongoza kwenye urazinishaji badala ya kutubu. Kusema udhaifu ni dhambi inaweza kusababisha aibu, lawama, kukata tamaa, na kukata tamaa katika ahadi za Mungu. Kutafakari na kusali kunatusaidia kubainisha tofauti hizi.
- **Weka kipaumbele.** Kwa sababu sisi ni wadhaifu, hatuwezi kufanya mabadiliko yote mara moja. Tunaponyenyekea na kuamini kukabiliana na udhaifu wetu wa kibinadamu masuala machache kwa wakati mmoja, tunaweza kupunguza ujinga hatua kwa hatua, kuunda sampuli nzuri ya mazoea, kuongeza afya yetu ya kimwili na kihisia na uthabiti, na kuimarisha imani

PICHA NA ISTOCK/THINKSTOCK

yetu katika Bwana. Mungu anaweza kutusaidia kujua wapi pa kuanzia.

- **Mpango.** Kwa sababu sisi ni wadhaifu, kuimarika kutahitaji zaidi ya hamu ya haki na nidhamu nyingi. Sisi pia tuna haja ya kupanga, kujifunza kutokana na makosa, kuendeleza mikakati madhubuti zaidi, kurekebisha mipango yetu, na kujaribu tena. Tunahitaji msaada kutoka katika maandiko matakatifu, vitabu muhimu, na watu wengine. Tunaanzia kidogo, kufurahi katika kuboresha, na kuchukua tahadhari (hata ingawa kunatufanya kujihisi tunaweza kuathirika na wadhaifu). Tunahitaji msaada ili kutusaidia kufanya maamuzi mazuri hata wakati tunapokuwa na uchovu au tumekata tamaa na mipango ya kuturudisha katika njia sahihi tunapokuwa tumeteleza.
- **Tumia subira.** Kwa sababu ya udhaidfu wetu, mabadiliko yanaweza kuchukua muda. Hatuachi tu udhaifu wetu kwa njia ile tunavyoacha dhambi. Wanafunzi wanyenyekevu hufanya kinachohitajika kwa hiari, kujifunza ujasiri, kuendelea kujaribu, na hawakati tamaa. Unyenyekevu unatusaidia kuwa na subira na sisi wenyewe na wengine ambao ni wadhaifu pia. Subira ni dhihirisho la imani yetu katika Bwana, shukrani kwa uaminifu Wake kwetu, na imani katika ahadi Zake.

Hata tunapotubu dhambi zetu kwa dhati, kupata msamaha, na kuwa wasafi tena, bado tunabaki wadhaifu. Bado tuko chini ya magonjwa, hisia, ujinga, maelekezo, uchovu, na vishawishi. *Lakini udhaifu na mapungufu si dhambi na haviwezi kutuzuia kuwa wasafi na wenye kustahili kuwa na Roho wa Mungu.*

Udhaifu kuwa Nguvu

Wakati Shetani ana nia ya kutumia udhaifu wetu kutushawishi katika dhambi, Mungu anaweza kutumia udhaifu

KUTOFAUTISHA KATI YA HATIA YENYE KUJENGA (HUZUNI YA KIMUNGU) NA UNYENYEKEVU KUTOKANA NA AIBU BANDIA ISIYO NA MSAADA

Hatia yenye kujenga—Huzuni ya Kiungu kwa ajili ya Dhambi	Imani & Unyenyekevu—Upole kama wa Kristo katika Udhaifu	Aibu ya Kuharibu—Bandia Isiyo na Msaada
Tunaelekea: • Kuhisi majuto kwa kukiuka kanuni za maadili yetu. • Kutubu, kukibadilisha mawazo yetu, moyo, tabia. • Kuwa wazi, kukiri makosa yetu, tufanye marekebisho. • Kua na kujifunza. • Tujione kama asili nzuri, ya thamani. • Kuwa na hamu ya kuwianisha tabia zetu na picha chanya ya ubinafsi wetu. • Kuwa na matumaini kamilifu katika nguvu ya ukombozi ya Upatanisho wa Kristo.	Tunaelekea: • Kuhisi utulivu wa uhakika na kujikubali wewe mwenyewe, viungo na vyote. • Thubutu kukua na kuchangia. • Wajibika kwa makosa, tamani kuwa bora zaidi. • Jifunze kutokana na makosa na jaribu tena. • Kuza hisia ya ucheshi na furahia maisha na wengine. • Ona udhaifu wetu kama kitu kitupacho sehemu sawa na watu wengine • Kuwa na subira kwa udhaifu na dosari za wengine. • Ongeza kujiamini katika upendo na msaada wa Mungu.	Tunaelekea: • Kuhisi kutokuwa na thamani, kukata tamaa. • Kujaribu kuwaficha wengine udhaifu wetu. • Kuhofia kufichuliwa. • Kuwalaumu wengine kwa matatizo yako. • Epuka kujiingiza katika hatari, kuona kushindwa kama dhalilisho. • Kushindana na kujilinganisha na wengine. • Kujitetea na ukaidi au dufu. • Kuwa mwenye kejeli au kuwa mkali sana. • Kujishughulisha sana na kushindwa kwetu au ukuu wetu. • Ogopa kukataliwa na kuchukiwa na Mungu.

wa binadamu ili kufundisha, kuimarisha, na kutubariki. Kinyume na kile tunachoweza kutarajia au kutumaini, hata hivyo, Mungu si daima, "hufanya vitu dhaifu kuwa imara" kwetu kwa kuondoa udhaifu wetu. Wakati Mtume Paulo alipoomba kwa Mungu mara kadhaa kuwa amuondolee "mwiba katika mwili" Shetani alitumia kipigo chake, Mungu alimwambia Paulo, "Neema yangu inakutosha wewe; maana uwezo wangu hukamilishwa zaidi katika udhaifu" (2 Wakorintho 12:7, 9).

Kuna njia nyingi Bwana hufanya "vitu dhaifu kuwa vyenye nguvu." Wakati Yeye anaweza kuondoa udhaifu kupitia tiba ya kiajabu tunayotumaini, lakin katika uzoefu wangu binafsi hii kwa kiasi fulani ni nadra. Kwa mfano, naona hakuna ushahidi kwamba Mungu alimwondolea Moroni udhaifu wake wa kuandika baada ya aya maarufu katika Etheri 12. Mungu anaweza pia kufanya vitu dhaifu kuwa na nguvu na kutusaidia kufanya kazi licha ya udhaifu wetu, kupata hisia sahihi ya ucheshi au mtazamo juu ya hilo, na kuboresha hatua kwa hatua baada ya muda. Pia, uwezo na udhaifu mara nyingi huhusiana (kama nguvu ya uvumilivu na udhaifu wa ukakamavu), na tunaweza kujifunza kuthamini nguvu na udhaifu wa hasira ambao huendana nayo.

Kuna njia nyingine ambayo ina nguvu zaidi ambayo Mungu hufanya mambo dhaifu kuwa na nguvu kwetu. Bwana anasema na Moroni katika Etheri 12:37, "Kwa sababu umeuona udhaifu wako, utafanywa kuwa mwenye nguvu, hata kukaa mahali nimepatayarisha katika nyumba ya Baba yangu."

Hapa Mungu haahidi kubadili udhaifu wa Moroni, lakini kumbadili Moroni. Kwa kukabiliana na changamoto ya udhaifu wa kibinadamu, Moroni—pamoja na sisi—tunaweza kujifunza wema, huruma, upole, uvumilivu, ujasiri, kutokata tamaa, hekima, uthabiti, msamaha, ukakamavu, shukrani, ubunifu, na mengineyo ambayo hutufanya kuwa zaidi kama Baba yetu wa Mbinguni. Hizi ndio sifa hasa tulizokuja duniani kujifunza, sifa za Kikristo ambazo zinatuandaa ili turudi nyumbani hapo juu.

Hakuna mahali popote upendo wa Mungu, hekima, na nguvu ya ukombozi ni dhahiri zaidi kuliko uwezo Wake wa kubadilisha shida zetu na udhaifu wa binadamu katika fadhila za kiungu na uwezo wa kutufanya kuwa zaidi kama Yeye. ■

Mwandishi anaishi Utah, Marekani.

PICHA YA KIELELEZO NA COLIN LIGERTWOOD

Na Mzee W. Christopher Waddell
Wa wale Sabini

Dini SAFI

Huduma isiyo na uchoyo—kujisahau wenyewe, kutatua na shida za wengine, na kuweka chini maisha yetu katika huduma yao—imekuwa tabia ya wafuasi wa Yesu Kristo.

Katika Mathayo sura ya 11 Mwokozi anatufundisha somo muhimu kwa kile alichokifanya *si* kusema katika jibu la swali lililoulizwa na wafuasi wa Yohana Mbatizaji:

"Sasa wakati Yohana aliposikia akiwa gerezani habari ya matendo ya Kristo, aliwatuma wanafunzi wake wawili,

Na akamwambia, wewe ni yule anayekuja, au tumngoje mwingine?

Yesu akajibu na akawaambia, Nendeni na umwonyeshe tena Yohana yale ambayo mumesikia na kuyaona:

Vipofu wanapata kuona, viwete watembea, wenye ukoma wanatakaswa, na viziwi wasikia, wafu wafufuliwa, na maskini wanahubiriwa Habari Njema" (Mathayo 11:2–5).

Badala ya kutoa mafundisho mafupi ya maelezo na kuelezea kwamba Yeye alikuwa, kwa kweli, "ndiwe yule ajaye," Mwokozi alijibu kwa njia ya yale anayofanya—mfano Wake wa huduma.

Katika mkutano mkuu wa Aprili, 2014 Mzee Richard G. Scott wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili alitukumbusha: "Tunamtumikia Baba yetu wa Mbinguni kwa haki kwa kushawishi wengine na kuwahudumia. Mfano mkubwa wa aliyewahi kutembea ulimwenguni ni Mwokozi wetu, Yesu Kristo."[1]

Huduma isiyo na uchoyo—kujisahau wenyewe, kuta tua na shida za wengine, na kuweka chini maisha yetu katika kuwahudumia wao—daima ni tabia ya wanafunzi wa Yesu Kristo. Kama Mfalme Benjamin alivyofundisha zaidi ya miaka 100 kabla ya kuzaliwa kwa Mwokozi, "Na tazama nawaambia vitu hivi ili mpate hekima ili mjifunze kwamba mnapowatumikia wanadamu wenzenu mnamtumikia tu Mungu wenu" (Mosia 2:17).

Yakobo anatukumbusha kipengele muhimu cha "dini safi" hupatikana katika huduma yetu kwa wengine kama "kuwatembelea yatima na wajane katika shida zao" (Yakobo 1:27). "Dini safi" ni zaidi ya tamko la imani; ni maonyesho ya imani.

Wapende wasafiri wenzako

Katikati ya Julai 1984, wiki kadhaa tu baada ya mke wangu, Carol, na mimi kufunga ndoa katika Hekalu la Los Angeles California, tulikuwa njiani tukielekea Utah, mahali ambapo ningeeanza kazi yangu na Carol angemaliza masomo yake katika chuo kikuu. Tulikuwa tunaendesha magari tofauti. Kati ya magari haya mawili, tulikuwa tukisafirisha kila kitu tulichomiliki.

Kama nusu ya safari yetu, Carol alisogea kando ya gari langu na kuniashiria nisimame. Hii ilikuwa katika siku zile kabla ya simu za mkononi na smartfoni, ujumbe mfupi wa simu na Twita. Baada ya kuona ishara katika uso yake kupitia dirisha la gari lake, niliweza kutambua hakuwa anajisikia vizuri. Aliwasiliana nami kwamba anaweza kuendelea

VIELELEZO NA ANNIE HENRIE

kuendesha gari, lakini nilikuwa na wasiwasi kwa ajili ya mke wangu tuliyefunga ndoaa hivi karibuni.

Tulipokaribia mji mdogo wa Beaver, Utah, alisogea kando ya gari langu tena, na nilijua kwamba alihitaji kusimama. Alikuwa mgonjwa na hakuweza kuendelea. Tulikuwa na magari mawili yaliyojaa nguo na zawadi za harusi, lakini kwa bahati mbaya tulikuwa na fedha kidogo. Chumba cha hoteli kilikuwa nje ya bajeti yetu. Sikuwa na uhakika na cha kufanya.

Hakuna aliyewahi kufika Beaver kati yetu, na sikuwa na uhakika nilikuwa natafuta nini, tuliendesha tukizunguka kwa dakika chache hadi nikaona bustani. Tuliingia ndani ya bustani hiyo na tuliona mti ulio na kivuli kidogo, ambapo nilitandika blanketi ili Carol aweze kupumzika.

Dakika chache baadaye gari nyingine iliingia katika bustani hiyo na kuegesha gari hilo karibu na magari yetu mawili. Mwanamke, wa umri wa mama zetu, alitoka nje ya gari yake na kutuuliza kama kulikuwa na shida na kama angeweza kutusaidia. Alisema alikuwa ametutambua alipokuwa akitupita na alihisi kuwa alipaswa kusimama. Wakati tulipomwelezea hali yetu, mara hiyo alitualika nyumbani kwake, ambapo tungepumzika kwa muda tuliotaka.

Punde tulijikuta juu ya kitanda kizuri katika chumba chake cha kulala kilichokuwa chini ya nyumba yake na chenye baridi kidogo. Punde tulipotulia, dada huyu mzuri alitueleza kuwa alikuwa na shughuli kadhaa za kufanya na kwamba tungeachwa pekee yetu kwa saa chache. Alituambia kwamba kama tutasikia njaa, tulikuwa tumekaribishwa kwa kitu chochote tulichoweza kupata jikoni, na kama tungeoondoka kabla ya yeye kurudi nyumbani, tafadhali tungemfungia mlango wa mbele.

Baada ya kupata usingizi wa kutosha, Carol aliona ilikuwa vyema tuendelee na safari yetu bila kuenda jikoni. Wakati tulipoondoka, huyo mwanamke mkarimu hakuwa amerudi nyumbani kwake. Kulingana na kumbukumbu yetu, hatukuandika anwani na kamwe hatukumshukuru huyo msamaria mwema, ambaye alisimama njiani na kuwafungulia nyumba yake wageni walio kuwa na shida.

Nikitafakari juu ya tukio hilo, maneno ya Rais Thomas S. Monson, ambaye anajumuisha mawaidha ya Mwokozi na "enenda zako nawe ukafanye vivyo hivyo" (ona Luka 10:37) kama vile binadamu katika akili yake: "Hatuwezi kwa kweli kumpenda Mungu kama hatuwezi kupenda wasafiri wenzetu katika safari hii ya mauti."[2]

Popote tunapokutana na "wasafiri wenzetu"—kwenye barabara au kwenye nyumba zetu, kwenye uwanja wa michezo au katika shule zetu, kazini au kanisani—tunapotafuta, kuona, na kutenda, tutakuwa kama Mwokozi, tukibariki na kuhudumia njiani.

Tafuta

Mzee Neal A. Maxwell (1926–2004) wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili alifunza:

"Tofauti na Mwokozi wetu, hakika sisi hatuwezi kufidia dhambi za wanadamu! Aidha, kwa hakika hatuwezi kubeba magonjwa yote ya binadamu, udhaifu, na masikitiko (ona Alma 7:11–12).

"Hata hivyo, kwa kipimo chetu kidogo, kama vile Yesu alivyotualika, tunaweza kujitahidi kuwa 'hata kama [vile Yeye alivyo]' (3 Nefi 27:27)."[3]

Tunapotafuta kuwa kama Yeye, tukiwa na hamu ya dhati ya kubariki "wasafiri wenzetu," tutapatiwa fursa kusahau ubinafsi wetu na kuwainua wengine. Fursa hizi mara nyingi huwa si rahisi, kupima hamu yetu ya kweli ya kuwa kama Bwana, ambaye huduma yake ndio kubwa ya zote, Upatanisho Wake usio na mipaka, ni kitu chochote bali rahisi. Hata hivyo, Yeye anasema, "utukufu na uwe kwa Baba, na Mimi nikachukua na kukamilisha maandalizi yangu kwa wanadamu" (M&M 19:19).

Kutafuta kwa dhati kuwa kama Mwokozi itaturuhusu kuona kile ambacho hatungeweza kukiona vingenevyo. Msamaria wetu mwema aliishi karibu sana na Roho Mtakatifu na hivyo kumwezesha kujibu maongozi ya Mungu na kuweza kumkaribia mgeni aliyekuwa na shida.

Ona

Kuona kwa macho ya kiroho ni kuona vitu kama vile vilivyo kweli na kutambua shida ambazo vinginevyo hatungeweza kuzitambua. Katika fumbo la kondoo na mbuzi, si wale waliokuwa wamebarikiwa wala wale waliokuwa wamelaaniwa walikuwa wamemtambua Mwokozi katika wale walio kuwa na njaa, kiu, uchi, au gerezani. Waliyapo kea malipo yao kwa kuuliza, "Ni lini tulikuona ukiwa"? (Ona Mathayo 25:34–44).

Ni wale tu ambao walikuwa wameona kwa macho ya kiroho, na kutambua shida, walitenda na kuwabariki wale watesekao. Msamaria mwema wetu alitambua vile alivyoona kwa macho ya kiroho.

Tendo

Tunaweza kuona shida karibu nasi lakini tunaweza kuhisi kuwa duni kuitikia, tukidhania kwamba kile ambacho tunacho kitoa hakitoshelezi. Tunapotafuta kuwa hata kama Yeye na tunapoona mahitaji kwa wasafiri wenzetu kupitia macho ya kiroho, ni lazima tuamini kwamba Bwana anaweza kufanya kazi kupitia kwetu, na kisha ni lazima tuchukue hatua.

Walipokuwa wanaingia hekaluni, Petro na Yohana walikutana na mtu "kiwete tangu tumboni mwa mama yake" ambaye aliwaomba wampe sadaka (ona Matendo ya Mitume 3:1–3). Jibu la Petro ni mfano na mwaliko kwa kila mmoja wetu:

"Mimi sina fedha, wala dhahabu, lakini nilicho nacho ndicho nikupacho. Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama uende".

Akamshika mkono wa kuume, akamwinua" (Matendo ya Mitume 3:6–7).

Tunaweza kutenda kwa kutoa wakati wetu na vipaji vyetu, neno la ukarimu, au mgongo imara. Tunapotafuta na kuona, tutawekwa katika mazingira na hali ambayo tunaweza kutenda na kubariki. Msamaria mwema alitenda. Alituchukua nyumbani kwake na kutupa kile alichokuwa nacho. Kimsingi yeye alisema, "Kile nilicho nacho ndicho nakupa." Ilikuwa ndicho tulichohitaji hasa.

Rais Monson amefundisha kanuni sawa na hizo:

"Kila mmoja wetu, katika safari ya maisha ya duniani, atasafiri kwenye barabara yake ya Jericho mwenyewe. Je uzoefu wako utakuwa nini? Je wangu utakuwa nini? Je, nitashindwa kumtambua yule aliyeanguka miongoni mwa wezi na anahitaji msaada wangu? Je, wewe?

Je nitakuwa mmoja wa wale wenye kumtazama aliyejeruhiwa na kusikia ombi lake, lakini navuka upande mwingine? Je, wewe?

Au nitakuwa yule ambaye anaona, anasikia, anasimama, na kusaidia? Je wewe?

Yesu alitupa msemo wetu, 'Nenda, nawe ukafanye vivyo hivyo.' Tunapotii tamko hili, kunafunguka kwa maoni yetu ya milele ono la furaha ambalo ni nadra kulingana na kamwe kuzidiwa."[4]

Tunapokuwa zaidi kama Mwokozi kwa kutafuta, kuona, na kutenda, tutakuja kujua ukweli wa maneno haya ya Mfalme Benjamin: "Kwamba mnapowatumikia wanadamu wenzenu mnamtumikia tu Mungu wenu" (Mosia 2:17). ■

MUHTASARI

1. Richard G. Scott, "Nimewapa Mfano," *Liahona,* Mei 2014, 35.
2. Thomas S. Monson, "Upendo—Kiini cha Injili," *Liahona,* Mei 2014, 91.
3. Neal A. Maxwell, "Apply the Atoning Blood of Christ," *Ensign,* Nov. 1997, 22.
4. Thomas S. Monson, "Your Jericho Road," *Ensign,* Mei 1977, 71.

TAFUTA KWA DHATI

TAZAMA KWA MACHO YA KIROHO

TENDA NA UBARIKI

함소서
Need Thee Every Hour

"Nina Haja Nawe KILA SAA"

Wakati tulipokuwa hatujui nini zaidi tunachoweza kufundisha, mwenzangu alipendekeza tuimbe wimbo huu.

Na Jonathan H. Westover

Jumapili moja mchana katika misheni yangu huko Balsan, Korea, mmisionari mwenzangu na mimi tulikuwa tunasema kwaheri kwa waumini baada ya kanisa na tulikuwa karibu kuondoka kwenda kufundisha wakati kiongozi wa misheni wa kata alipotutambulisha kwa kijana mwenye umri wa miaka 12, Kong Sung-Gyun. Alikuwa amehudhuria kanisa siku hiyo na alitaka kujifunza zaidi kuhusu injili.

Bila shaka tulikuwa na furaha kuhusu matarajio ya kumfundisha, lakini pia nilikuwa na woga kuhusu kufundisha kijana mdogo vile. Tuliamua kuhakikisha tunapata na ruhusa ya wazazi wake, hivyo basi nilipiga simu nyumbani kwa Kong Sung-Gyun na kuongea kwa kifupi na mama yake, Pak Mi-Jung. Nilishangazwa wakati aliposema alifurahi mwanawe alikuwa anafikiria kuhudhuria kanisa na kwamba angefurahia afundishwe nasi.

Wachunguzi Wasiotarajiwa

Jioni ya pili tulifika nyumbani kwa kijana yule, tayari kufundisha. Tulishangaa kujua kwamba Pak Mi-Jung pia alitaka tumfundishe na binti yake, Kong Su-Jin. Na kwa kuwa tulikuwa wageni katika nyumba yake, Pak Mi-Jung alitaka kukaa katika mafundisho. Bila shaka tulikuwa na furaha kufundisha wengi wa waliotaka kusikiliza.

Baada ya kutupa vinywaji, tuliketi pamoja na kuanza kuzungumza. Badala ya kuanza moja kwa moja na somo, Pak Mi-Jung alitaka kutujua vyema zaidi na kutuelezea kuhusu hali ya familia yake. Alituambia kuhusu majaribu ya hivi karibuni na matatizo waliyokuwa wamepitia, ikiwa ni pamoja vita vya mwanawe vya hivi karibuni na saratani. Alikuwa amepitia mafanikio ya matibabu ya mionzi, na saratani ilikuwa kwa sasa katika hali ya kuondoka, lakini madaktari waliwaonya ingerudi wakati wowote. Huu ulikuwa mzigo mkubwa kwa familia. Walikuwa famila ya kipato cha kawaida, na baba alilazimika kufanya kazi kwa nguvu sana ili kuweza kuwa na nyumba na chakula.

Nilishangazwa na kuhuzunishwa na majaribu katika maisha yao. Maisha hayakuwa rahisi kwao, lakini ukaribu ndani ya familia ulikuwa dhahiri zaidi kuliko nilivyokuwa nimeona katika familia nyingine yo yote ambayo nilikuwa nimekutana nayo Korea, ambayo inasema mengi katika jamii ya kifamilia za Korea. Sisi tuliondoka nyumbani kwao jioni hiyo baada ya kujuana vyema na familia hii maalum na baada ya kuwafundisha ujumbe wa injili.

Mwenzi wangu na mimi tulirudi kufundisha mara kadhaa zaidi wiki hiyo, kila wakati tukipata ukujufu na

VIELELEZO NA JULIA YELLOW; BAMBOO ART BY ISTOCK/THINKSTOCK

ukarimu sawa na ule tuliopata katika matambezi yetu ya kwanza. Wakati mada ya ubatizo ilipokuja, watoto wawili walikuwa na hamu sana kujiunga na Kanisa. Hata hivyo, mama yao hakushiriki katika msisimko wao. Ingawa mafundisho yetu yalimwingia na alitumaini kuwa ni ya kweli, yeye hakuona kama angeweza kufanya na kuwa na aina ya msimamo ambao Kanisa linataka unapojiunga nalo. Yeye pia hakuona kwamba ingekuwa sahihi kwake yeye kubatizwa bila mumewe, ambaye tulikuwa bado kukutana naye. Hata hivyo, yeye alikuwa na nia ya kuendelea kukutana na sisi na pia alitaka kujiunga na watoto wake katika kuhudhuria kanisa.

Karibu na mwisho wa wiki ya pili, tulipokuwa tukiendelea kufundisha katika nyumba yake, tulikutana na mume wake, Kong Kuk-Won—mnyenyekevu, mwenye subira, na mtu mkarimu. Yeye alijiunga na sisi kwa majadiliano machache ya kumalizia na papo hapo aliamini kila kitu tulichowafundisha, ikiwa ni pamoja na mafundisho ambayo mara nyingi wengine waliyaona vigumu kama vile zaka na Neno la Hekima. Pamoja na hali zao kuwa duni ki fedha, walianza kulipa zaka. Kikwazo pekee kwa baba kilikuwa kufanya kazi kila siku ya Jumapili. Yeye alifanya kazi katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Seoul kila Jumapili, hivyo hakuweza kuhudhuria kanisa na wengine wa familia yake. Pamoja na ratiba ya kazi yake, yeye na mke wake walipanga kuhudhuria ubatizo ya watoto wao Jumapili iliyofuata.

Kufuatia ubatizo wa watoto wao, tuliendelea kukutana mara kwa mara katika nyumba ya familia. Tulikuwa na jioni ya familia nyumbani, tulishiriki maandiko na matukio ya kuvutia, na kuwatambulisha kwa waumini wa kata. Hata hivyo, licha ya uzoefu wa kuendelea wa injili, wazazi hawakuwa karibu kubatizwa.

Wakati huo huo mwenzi wangu mmisionari alihamishwa, na mwenzi mpya alikuwa mmisionari aliyetoka punde kutoka kituo cha mafunzo cha umisionari. Alijawa na imani, nguvu, na hamu, na kwa kweli nilikuwa na wakati mgumu kuafikiana naye. Baada ya kukutana na Kong Kuk-Won na Pak Mi-Jung mara chache, mwenzi wangu alinijia na kuuliza kama mwenzangu wa awali pamoja nami tulikuwa tumefunga pamoja nao. Hatukuwa tumefunga nao Kwa kweli, wazo hilo halikuwa limewahi kunijia. Hivyo tulikutana na familia na kupendekeza

Roho mwenye nguvu alikuwa katika chumba tulipomaliza mstari wa mwisho. Pak Mi-Jung aliniangalia machoni na kusema, "Ninahitaji kubatizwa."

kufunga. Nilishtuka kugundua kuwa walikuwa mara kwa mara wakifunga peke yao, kwa ajili ya afya ya mtoto wao na kwa ajili ya mabadiliko katika ratiba ya kazi ambayo ingeweza kuruhusu Kong Kuk-Won kuhudhuria kanisa. Baada ya mwenzi wangu na mimi kuungana nao katika kufunga, maombi yetu yalijibiwa na ratiba ya kazi ya Kong Kuk-Won ikabadilika. Lakini Pak Mi-Jung alikuwa bado mgumu kuhusu kubatizwa.

Wazo lenye Maongozi

Mwenzi wangu basi alikuwa na wazo jingine zuri. Yeye alitoa nje kitabu chake cha nyimbo cha mfukoni na kuuliza

kama tunaweza kuimba pamoja nao. Ingawa sisi tuliwahi kuimba pamoja kwenye hafla ya awali, sijawahi kuona Pak Mi-Jung akiimba na nilidhania tu kwamba yeye hakuwa akipenda kuimba au alikuwa na wasiwasi kwa sababu wimbo ulikuwa mpya kwake. Mwenzangu alimuuliza kama alikuwa na wimbo alioupenda, na kwa kushtuka kwangu, alipaliwa na mate na kujibu kwamba tangu alipokuwa msichana mdogo, wimbo alioupenda ulikuwa "Nina Haja Nawe Kila Saa" (*Hymns,* no. 98). Tulianza kuimba kwa sauti nne kwa mpangilio, na baba akiimba melodi, mama akiimba alto, na mwenzangu akiimba tena, na mimi nikiimba bezi.

Roho alikuwa na nguvu katika chumba hicho. Tulipoimba aya ya tatu, hisia ilimshinda, na sauti yake ilipungua tulipoendelea:

Nina Haja Nawe Kila Saa,
Kila Hali.
Maisha ni bure,
Usipokuwepo.
Yesu Nakuhitaji;
Viwyo kila saa!
Nibariki, Mwokozi
Nakujia!

Tulipomaliza ubeti wa nne na wa mwisho, yeye alikuwa analia. Mumewe alikuwa anajaribu kumfariji, hatimaye aliweza kujimudu mwenyewe. Yeye alinitazama moja kwa moja machoni na akasema, "Nina haja ya kubatizwa."

Ibada hii ya ubatizo wa Kong Kuk-Won na Pak Mi-Jung Jumapili ile mchana ilikuwa moja ya ibada za kiroho zaidi katika kazi yangu. Watoto wao walishiriki katika mpango, na waumini mbalimbali wenyeji walihudhuria ili kuonyesha kuunga mkono familia hii mpya iliyoongoka katika kata yao. Mwenzi wangu na mimi tuliimba muziki maalum: "Nina Haja Nawe Kila Saa."

Hatimaye mimi nilimaliza misheni yangu na kurudi nyumbani. Baada ya mwaka mmoja katika chuo, mimi nikarudi Korea kwa ajili ya kazi ya kupata ujuzi ya majira ya kiangazi, na kila mwisho wa wiki mimi nilichukua hatua ya kuwatembelea marafiki wengi maalum na familia nilizokuwa nimekutana nazo katika misheni yangu. Baada ya wiki chache mimi nilirejea tena Balsan na nilikutana na familia hii maalumu. Baada ya kuwasili katika nyumba yao, mimi niliona kuwa kuna mtu alikuwa amekosekana—mwana wao. Pamoja na machozi katika macho yake, Pak Mi-Jung aliniarifu: saratani ya mwana wao ilirudi na, katika umri wa miaka 14, alikuwa amepoteza pambano.

Nilipokuwa nikijaribu kutoa rambirambi zangu na pia kukabiliana na uchungu niliokuwa nikiusikia, Kong Kuk-Won alinihakikishia mimi kwamba kila kitu kitakuwa SAWA. Waliipenda injili, walihudhuria kanisa kwa uaminifu wakiitazamia siku ile familia yao itakapopata kuunganishwa milele katika Hekalu la Seoul Korea. Licha ya maumivu ya moyoni ambayo wao waliyasikia, familia ilijua kuwa wangeweza tena kuonana na Kong Sung-Gyun na kuwa pamoja tena. Pak Mi-Jung pia aliniambia kuwa kuimba nyimbo za kila siku kulimsadia yeye kupata nguvu ya kuendelea kuishi na kusikia amani inayoambatana nayo ambayo Roho huileta.

Nilipokuwa nikiondoka nyumbani kwao jioni ile, nilitafakari juu ya maneno ya wimbo wa Pak Mi-Jung. Ninashukuru kwamba Baba wa Mbinguni aliibariki familia kwa amani baada ya kufariki kwa Kong Sung-Gyun, na mimi hasa nashukuru kwa nafasi ya Roho Mtakatifu katika kuongoka kwa Pak Mi-Jung, ambako kumeiwezesha familia kufuzu kupata baraka za milele za hekaluni. ■

Mwandishi anaishi Utah, Marekani.

NYIMBO ZA DINI HUWAFARIJI WAOMBOLEZAJI

"Baadhi ya mahubiri makuu yanahubiriwa kwa kuimba nyimbo. Nyimbo hutuelekeza kwenye toba na matendo mema, kujenga ushuhuda na imani, kufariji wachovu, kufariji wenye huzuni, na kutuhamasisha kustahimili hadi mwisho."

"First Presidency Preface," *Hymns,* ix.

Na Rais
Boyd K. Packer
Rais wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

Dhabihu ya Mwokozi Isiyo na Ubinafsi

Bwana yupo daima. Aliteseka na kulipa deni kama uko tayari kumkubali yeye kama Mkombozi wako.

Sote tunaishi kwa deni la kiroho. Kwa njia moja au nyingine, akaunti ukua na kukua. Kama unalipa unavyosonga mbele, utakuwa na machache ya kuhofia. Punde unapoanza kujifunza nidhamu na kujua kwamba kuna siku ya kiama mbele. Jifunze kulipa akaunti ya kiroho kwa wakati ufaao badala ya kungojea hadi riba inakusanywa na adhabu.

Kwa sababu mnajaribiwa, mnatarajiwa kufanya makosa fulani. Nadhania kwamba mmefanya mambo maishani mwenu ambayo mnajutia, mambo ambayo hamwezi hata kuomba msamaha hata kurekebisha; kwa hivyo, mnabeba mzigo. Ni wakati wa kutumia neno *hatia* ambayo inaweza kututia dosari kama wino usioweza kufutika kwa urahisi. Mtoto wa kambo wa hatia ni kuvunjika moyo, kujutia baraka na fursa zilizopotezwa.

Kama unahangaika na hatia, hauna tofauti na watu wa Kitabu cha Mormoni ambao nabii aliwaongelea, "Kwa sababu ya dhambi zao kanisa lilianza kufifia; na wakaanza kutokuamini katika roho wa unabii na roho wa ufunuo; na hukumu za Mungu zikawatazama wao nyusoni" (Helamani 4:23).

Mara nyingi tunajaribu kutatua shida za

KUSHOTO: PICHA KUTOKA PHOTOS.COM/THINKSTOCK, KULIA: *KRISTO KATIKA GETHSEMANE*, NA ARY SCHEFFER, KWA HESHIMA YA MAKUMBUSHO YA DORDRECHTS, DORDRECHTS, UHOLANZI, ISINAKILIWE; SEHEMU YA NYUMA YA PICHA KUTOKA ISTOCK/STOCK



hatia kwa kumwambia mtu mwengine na kujiambia sisi wenyewe kwamba haidhuru Lakini kwa kiasi fulani, ndani yetu, hatuamini hivyo. Wala hatuamini sisi wenyewe kama tunasema hivyo. Tunajua vyema ni muhimu!

Manabii daima wamefunza toba. Alma alisema, "Tazama, anakuja kukomboa wale watakaobatizwa kutokana na toba, kupitia imani katika jina lake" (Alma 9:27).

Alma alimwambia mwanawe mpotovu wazi wazi, "Sasa, toba haiwezi kuja kwa watu isipokuwa kuwe na adhabu, kama ilivyo pia ya milele kama vile maisha yanapaswa kuwa, ilivyo kinyume na mpango wa furaha" (Alma 42:16).

Kuna madhumuni mawili ya kimsingi kwa maisha ya duniani. Kwanza ni kupokea mwili, ambao unaweza, kama tutapendelea, ukatakaswa na kuinuliwa na kuishi milele. Madhumuni ya pili ni kujaribiwa. Katika majaribio, kwa kweli tutafanya makosa. Lakini kama tutapendelea, tunaweza kujifunza kutokana na makosa yetu. Kama tunasema kwamba sisi hatujatenda dhambi, tunamfanya yeye kuwa mwongo, na neno hatunalo sisi" (1 Yohana 1:10).

Wewe labda unaweza kuhisi upungufu katika akili na mwili na unafadhaika au kulemewa na mzigo wa akaunti ya kiroho ambayo imetiwa alama "wakati umepita." Unapokumbana ana kwa ana na wewe mwenyewe katika nyakati kama hizo za tafakari za kimya (ambazo wengi wetu wanajaribu kukwepa), kuna mambo ambayo hayajasuluhishwa ambayo yanakusumbua? Una chochote katika dhamiri yako? Bado wewe, kwa kiwango kimoja au kingine, una hatia ya chochote kidogo au kikubwa?

Mara nyingi sana, tunapokea barua kutoka kwa wale ambao wamefanya makosa makubwa au wamelemewa na mzigo. Wanaomba kujua, Je naweza kusamehewa? Naweza kabisa kubadilika? Jibu ni ndio!

Paulo aliwafunza Wakorintho, Hayajaondolewa kwenu majaribu bali kama ilivyo kawaida kwa mwanadamu: Lakini Mungu ni mwaminifu, hatakubali ujaribiwe zaidi ya uwezo wako; bali kwa majaribu pia atafanya njia ya kuponyokea, kwamba uweze kuyastahimili (1 Wakorintho 10:13).

Injili inatufunza kwamba ahueni kutokana na mateso na hatia inaweza kupatikana kupitia toba. Isipokuwa kwa wachache—wale wachache tu—wanaoasi hata jahamamu baada ya kujua utimilifu, hamna tabia, hamna ulevi, hamna uasi, hamna dhambi, hamna kosa, dogo au kubwa, ambalo limesamehewa kutokana na ahadi ya msamaha kamili. Licha ya kilichofanyika katika maisha yako, Bwana ametayarisha njia ya kurudi kama utasikia maongozi ya Roho Mtakatifu.

Wengine wamejawa na mvuto wa nguvu sana, majaribu ambayo hujirudia tena na tena mawazoni mwao, pengine hata kuwa tabia, na kisha ulevi. Tu wadhaifu kwa baadhi ya makosa na dhambi na pia kusema kwamba hatuna hatia kwa sababu tumezaliwa hivyo. Tunaingia katika mtego, na kisha uchungu na mateso yakaja ambayo Mwokozi tu ndiye anayeweza kuponya. Una uwezo wa kuacha na kukombolewa.

Shetani Hushambulia Familia

Rais Marion G. Romney (1897–1988) aliniambia wakati mmoja, "Usiwaambie tu ili waweze kukuelewa; waambie ili kwamba wasiweze kukosa kukuelewa."

Nefi alisema, "Kwani roho hufurahia uwazi; kwani kwa jinsi hii Bwana Mungu hutenda kazi miongoni mwa watoto wa watu. Kwani Bwana Mungu hutoa nuru hata tupate ufahamu" (2 Nefi 31:3).

Kwa hivyo sikilizeni! Nitaongea wazi wazi kama mtu aliyeitwa na aliye chini ya sharti la kufanya hivyo.

Mnajua kwamba kuna adui. Maandiko yanamwita kwa maneno haya: "Yule nyoka mzee, ambaye ni shetani . . . baba wa uongo wote." (2 Nefi 2:18). Alitupwa nje mwanzoni (ona M&M 29:36–38) na kunyimwa mwili wenye kufa. Yeye sasa ameapa kudhoofisha "mpango mkuu wa furaha" (Alma 42:8) na kuwa adui wa wema wote. Yeye analenga mashambulizi yake kwenye familia.

Mnaishi katika siku ambapo janga la picha za ponografia zimezagaa kote ulimwenguni. Ni vigumu kiziepuka. Ponografia inalenga sehemu ya uhalisi wako ambao kwayo kuna uwezo wa kuumba uhai.

Kujiingiza katika ponografia kunakupeleka kwenye shida, kuvunjika kwa ndoa, magonjwa, na taabu za aina nyingi. Hamna sehemu yake ambayo haina hatia. Kuzikusanya, kuzitazama au kuzibeba kwa jinsi yoyote ni kama kumweka nyota hatari kwenye mkoba wako. Kunakuweka kwenye mfano wa kuumwa na nyoka mwenye sumu kali. Mtu anaweza kuelewa kwa urahisi, na ulimwengu ukiwa kama ulivyo, unaweza bila kujua kujingiza ndani yake, kuzisoma au kuzitazama bila kujua matokeo yake mabaya. Kama haya yanaelezea juu yako, nakuonya uache. Koma sasa!

Kitabu cha Mormoni hufunza kwamba wanadamu wote wamefunzwa vyema ili "wajue kati ya mema na maovu" (2 Nefi 2:5). Hiyo inakujumuisha na wewe. Unajua kile kilicho sahihi na kile kilicho kosa. Kuwa makini sana usivuke mstari huo.

Kumekuwa na Mmoja tu katika historia zote za binadamu ambaye alikuwa hana dhambi kabisa, na alifuzu kujibu matakwa ya dhambi na uvunjaji sheria kwa wanadamu wote.

Ingawaje makosa mengi yanaweza kuungamwa kwa faragha kwa Bwana, kuna makosa mengine ambayo yanahitaji zaidi ya hayo ili kuleta msamaha. Kama makosa yako ni makubwa sana, mwone askofu wako. Vinginevyo, kuungama kwa kawaida, kwa faragha na kibinafsi, kutatosha. Lakini kumbuka, ile asubuhi kuu ya msamaha yawezekana isije yote mara moja. Kama mwanzo utajikwaa, usife moyo. Kushinda kuvunjika moyo ni sehemu ya majaribu. Usife moyo. Na kama nilivyoshauri awali, mara unapotubu na kuziacha dhambi zako, usitazame nyuma.

Mwokozi Aliteseka kwa Ajili ya Dhambi Zetu

Bwana yupo daima. Yeye ameteseka na kulipa adhabu ikiwa uko tayari kumpokea Yeye kama Mkombozi wako.

Kama wanadamu, sisi hatuwezi, kwa kweli hatuwezi, kufahamu kikamilifu *jinsi* Mwokozi alivyotimiza dhabihu Yake ya kulipia dhambi. Lakini kwa sasa *jinsi gani* si muhimu kama *kwa nini* ya kuteseka Kwake. Kwa nini alifanya hivyo kwa sababu yako, yangu, wanadamu wote? Yeye alifanya hivyo kwa sababu ya upendo wake kwa Mungu Baba na wanadamu wote. "Hakuna mtu aliye na upendo kumshida huyu, kwamba autoe uhai wake kwa sababu ya marafiki zake" (Yohana 15:13).

Katika Gethsemane, Kristo alienda kando mbali kidogo na Mitume Wake ili kuomba. Kile kilichotokea ni zaidi ya uwezo wetu kuelewa! Lakini tunajua kwamba alikamilisha Upatanisho. Yeye alikuwa tayari kujichukulia juu Yake makosa, dhambi na hatia, hofu na uonga wa ulimwengu wote. Aliteseka kwa sababu yetu ili

THE CROWN OF THORNS, NA GUSTAVE DORÉ; MAELEZO KUTOKA *THE CRUCIFIXION OF CHRIST*, KWA HESHIMA YA CHURCH HISTORY MUSEUM

kwamba sisi tusipate kuteseka. Watu wamepata mateso na kufa kifo cha maumivu makali, kifo kibaya. Lakini kuteseka Kwake kunapita mateso yote.

Katika umri wangu, nimepata kujua maumivu ya kimwili ni nini, na siyo mzaha! Hakuna mtu yeyote aepukae katika maisha haya bila kujifunza kitu kimoja au viwili kuhusu mateso. Lakini kuteseka kwake yeye binafsi ambako siwezi kustahamili ndipo ninapokuja kujua kwamba mimi nimesababisha mtu mwingine ateseke. Ndipo basi ninapopata kuona kidogo tu kuteseka kwa Mwokozi alikopata katika Gethsemane.

Kuteseka Kwake ni tofauti na kule kwingine kote kabla au tangu kwa sababu Yeye alijichukulia juu Yake adhabu zote ambazo ziliwekwa kwa ajili ya familia ya mwanadamu. Tafakari haya! Yeye hakuwa na deni la kulipa. Hakutenda kosa lolote. Hata hivyo, jumla ya hatia zote, huzuni na hofu, maumivu na kufedheheshwa, mateso yote ya kiakili, mhemko, na ya kimwili yanayojulikana na mwanadamu—Yeye aliyapata yote. Kumekuwa na Mmoja tu katika historia ya mwanadamu ambaye alikuwa bila dhambi, aliyefuzu kujibu kwa ajili ya dhambi na makosa ya wanadamu wote na kupona uchungu ambao unaambatana na kuzilipia.

Aliutoa uhai Wake na kimsingi alisema, "Ni mimi nichukuae juu yangu dhambi za ulimwengu" (Mosia 26:23). Alisulubiwa; Akafa. Hawangeweza kuuchukua uhai Wake kutoka Kwake. Yeye alikuwa radhi kufa.

Msamaha Kamili Unawezekana

Kama ulijikwaa au hata kupotoka kwa muda, kama utahisi kwamba adui amekukamata mateka, unaweza kusonga mbele kwa imani na usihangaike kule na huko katika ulimwengu tena. Kuna wale waliosimama tayari kukuongoza tena kwenye amani na usalama. Hata neema ya Mungu, kama ilivyoahidiwa katika maandiko, huja "baada ya yote tunayoweza kufanya" (2 Nefi 25:23). Uwezekano wa haya, kwangu, ni ukweli wenye kustahili kuujua.

Naahidi kwamba asubuhi angavu ya msamaha yaweza kuja. Kisha "amani ya Mungu, inayoshinda uelewa wote" (Wafilipi 4:7) itakuja katika maisha yako tena, kitu kama vile machweo, na wewe, kama vile Yeye "hamtakumbuka dhambi zenu tena kabisa" (Yeremia 31:34). Je! Utajuaje? Utajua! (Ona Mosia 4:1–3.)

Hayo ndiyo niliyokuja kuwafundisha ninyi mnaofadhaika. Yeye ataingilia kati na kutatua matatizo ambayo wewe hauwezi kutatua, lakini wewe utahitajika kulipia gharama. Haiwezekani kufanyika bila kutenda hivyo. Yeye ni mtawala mkarimu sana kwa hivyo Yeye daima atalipa gharama inayohitajika, lakini Yeye anakutaka wewe ufanye kile uwezacho kufanya, hata kama ni uchungu.

Mimi nampenda Bwana, na nampenda Baba ambaye alimtuma Yeye. Mizigo yetu ya kufa moyo, dhambi na hatia inaweza kuwekwa mbele Zake, na kwa masharti Yake ya ukarimu, kila kitu katika akaunti kinaweza kutiwa alama "kimelipwa kabisa."

"Njoo sasa, natushauriane pamoja, asema Bwana: ijapokuwa dhambi zako ni nyekundu sana, zitafanywa nyeupe kama theluji; ijapokuwa ni nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu." Hivi ndiyo, Isaya aliendelea, "kama u tayari na ni mtiifu" (Isaya 1:18–19).

Njoo Kwake

Maandiko "Jifunze hekima katika ujana wako; naam, jifunze katika ujana wako kuzishika amri za Mungu" (Alma 37:35) ni mwaliko unaoambatana na ahadi ya amani na ulinzi dhidi ya adui. "Na mtu asipuuze ujana wako; bali uwe mfano kwa waaminio, katika maneno, katika mazungumzo, katika hisani, katika roho, katika imani, katika utakaso" (1 Timotheo 4:12).

Usitarajie kwamba mambo yote yataenda sambamba maisha yako yote. Hata wale wanaoishi kama wanavyostahili, mara nyingine huwa ni kinyume. Kabiliana na kila changamoto ya maisha kwa mtazamo na uhakika, na utakuwa na amani na imani ya kukuhimili sasa na siku zijazo.

Kwa wale ambao hawajapata bado baraka zote mnazohisi mnataka na ambazo mnahitaji kuwa nazo, naamini kwa dhati kwamba hakuna uzoefu au nafasi muhimu ya ukombozi na uokovu watakayo nyimwa wale ambao wanaishi kwa uaminifu. Bakini kuwa wenye kustahiki; kuweni na matumaini, subira, na wenye kusali. Mambo yana njia ya kurekebika. Kipawa cha Roho Mtakatifu kitakuongoza na kitayaelekeza matendo yako.

Kama wewe ni mmoja wa wale wanokabiliwa na hatia, tamaa, au huzuni kama matokeo ya makosa uliyofanya au Baraka ambazo bado hazijaja, soma mafundisho yanayotuliza yanayopatikana katika wimbo "Njoo kwa Yesu":

Njooni kwake Yesu, ninyi muliolemewa na mizigo,
Mliochoshwa na kuzirai, na dhambi kudhulumiwa.
Atakuongoza salama hadi huko mbinguni
Ambapo wote wanaomwamini wanaweza kupata pumziko.



Mizigo yetu ya kuvunjika moyo, dhambi, na hatia inaweza kuwekwa mbele Zake, na kwa masharti Yake ya ukarimu, kila kitu katika akaunti kinaweza kutiwa alama "kimelipwa kabisa."

Njooni kwake Yesu, Yeye milele atakusikiliza,
Ingawa katika giza umepotea.
Upendo wake utakukuta na kwa upole kukuongoza
Kutoka giza la usiku hadi katika mwangaza.

Njoo kwake Yesu, hakika atakusilikiza,
Kama wewe kwa upole utaomba upendo wake.
Oh, haujui kwamba malaika wako karibu nawe
Kutoka makao mema juu?[1]

Mimi nadai, pamoja na Ndugu zangu Mitume, kuwa ni shahidi maalum wa Bwana Yesu Kristo. Ushuhuda huu unaimarishwa kila mara ninapohisi ndani yangu au kwa wengine athari ya utakaso wa dhabihu Yake takatifu Ushuhuda wangu na ule wa Ndugu zangu, ni wa kweli. Tunamjua Bwana. Yeye si mgeni kwa manabii, waonaji, na wafunuzi Wake.

Ninaelewa kwamba wewe si mkamilifu, lakini unasonga mbele kwenye barabara hiyo. Kuweni na ujasiri. Mjue kwamba yeyote aliye na mwili ana uwezo juu ya yule asiye nao.[2] Shetani alinyimwa mwili; kwa hivyo ukikabiliwa na majaribu, jua kwamba wewe unayashinda majaribu hayo yote kama utatumia haki ya kujiamulia aliyopewa Adamu na Hawa katika bustani na kurithishwa kwa kizazi hiki.

Na kama mtatazama mbele kwa tumaini na hamu ya kutenda kile ambacho Bwana angependa mfanye—hayo ndio yote yanayotarajiwa. ■

Kutoka katika hotuba ya mkutano wa ibada, "Truths Most Worth Knowing," delivered kule Chuo Kikuu cha Brigham Young mnamo Nov. 6, 2011. Kwa nakala nzima katika Kingereza, nenda speeches.byu.edu.

MUHTASARI

1. Ona "Come unto Jesus," *Hymns,* no. 117.
2. Ona *Teachings of Presidents of the Church: Joseph Smith* (2007), 211.

KUSHOTO: PICHA KUTOKA PHOTOS.COM/THINKSTOCK; RIGHT: MAELEZO KUTOKA *THOUGH YOUR SINS BE AS SCARLET,* NA HOWARD LYON, HAIPASWI KUNUKULIWA

IMBA WIMBO WAKO UNAOUPENDA

Nilikuwa nimejifungua binti yetu, Rebeka. Uchungu wa kujifungua kwangu ulikuwa mkali, na nilikuwa nimechoka.

Wakati Rebeka akiwekwa katika mikono yangu, nilijawa na hisia kwamba nilipaswa niimbe wimbo wangu ninaoupendao, "Mimi Mwana wa Mungu" (*Nyimbo,* nambari 301). Jibu langu la awali lilikuwa, "Hapana, nimechoka sana. Nitamwimbia baadaye." Lakini wazo likaja tena. Hivyo, ingawa nilikuwa nimechoka, nilianza kuimba mstari wa kwanza. Mume wangu na mama yangu walijiunga nami.

Tulipomaliza wimbo, nilihisi hisia mzuri katika chumba hicho. Hata daktari, ambaye hadi hatua hiyo alikuwa ametenda kitaaluma zaidi na kuwa katika dunia yake, machozi yalimwagika usoni mwake. Alitushukuru kwa kuimba wimbo mzuri kama huo. Alisema kuwa katika miaka yote yeye akiwa anazalisha watoto, hakuwahi kujisikia kama ilivyokuwa kwa wakati huo.

Niliwazia tukio hilo na kufikiria kama nilipaswa kutafuta rekodi ya wimbo huo na kumpa. Kwa bahati mbaya, nilishughulika sana na maisha na nikasahau juu ya jambo hilo.

Kisha siku ikaja ya kutazamwa kwangu baada ya kujifungua. Daktari alipoingia chumbani, uso wake uking'aa, na kunikumbatia. Alisema hakuweza kuutoa wimbo huo akilini mwake na alikuwa hata amejaribu kupata muziki huo katika mtandao ili aweze kuuimbia familia yake. Hapo ndipo Roho Mtakatifu aliponikumbusha kwamba nilipaswa nipate nakala ya muziki kwa ajili yake. Nilimuahidi kwamba wiki hiyo ningerudi na muziki huo.

Usiku huo niliomba msaada ili kupata mpangilio wa wimbo ambao ungekuwa bora zaidi kwake. Alasiri iliyofuata nilinunua CD iliyokuwa na wimbo huo. Ilipofika katika sanduku la posta siku chache baadaye, sikuweza kungojea kumpa.

Alikuwa na furaha kubwa kuupokea na akanishukuru kwa zawadi. Aliniambia kuwa hakuwa na uhakika ni kwa nini, lakini wimbo huu ulikuwa muhimu sana kwake kushirikiana na familia yake. Tulipoendelea kuzungumza, nilimwelezea si tu upendo wangu wa wimbo huo lakini pia ushuhuda wangu wa ukweli rahisi unaofundisha.

Nilipoendesha gari kwenda nyumbani siku hiyo, nilihisi upendo wa Baba yetu wa Mbinguni kwa mmoja wa binti zake—daktari wangu. Anamjua na kumpenda, na anamtaka aelewe kwamba yeye pia anaweza kurudi kuishi Naye tena. ■

Angela Olsen Center, Ohio, Marekani

Tulipomaliza wimbo, daktari, ambaye hadi hatua hiyo alikuwa ametenda kitaalamu na kuwa katika dunia yake, alikuwa na machozi yakimwagika usoni mwake.



Kwanini Baba wa Mbinguni siyo "mara zote" anatulinda na kutuonya?

AHADI ZAKE ZA WAKATI WOTE

Nilipokaa kwenye mkutano wa sakramenti nikitafakari sala ya kubariki mkate, maneno yaliendelea kujirudia yenyewe katika fikra zangu: "kwamba daima Roho wake apate kuwa pamoja nao" (Moroni 4:3; D&C 20:77).

"Daima," ilisema—siyo kwa wakati fulani tu. Kwanini, wakati huo, miezi kadhaa iliyopita, mume wangu na mimi hatukuweza kuongozwa juu ya kumlinda kijana wetu wa miaka 11 kabla hajauawa kwa ajali ya baiskeli kugongwa na gari? Kwanini Baba wa Mbinguni siyo mara zote anatulinda na kutuonya sisi?

Nilifundishwa katika darasa la watoto na niliamini kwamba Roho Mtakatifu angetulinda. Angetumia sauti ndogo nyembaba kutulinda, kutuongoza, na kututahadharisha na hatari. Mawazo haya yamekuwa katika akili yangu toka Ben alipofariki. Nilimkosa sana, na moyo wangu uliuma kwa kutaka kuelewa na amani.

Sauti yangu ya kuonya ilikuwa wapi? Roho Mtakatifu Alikuwa wapi? Nilihisi kwamba tulikuwa tukifanya vyema kuwa wema. Tulilipa zaka yetu, tulihudhuria mikutano, na kutumikia pale tulipotakiwa kutumikia. Tulikuwa mbali na ukamilifu, lakini tulifanya jioni ya familia na kujifunza maandiko. Tulikuwa tunajaribu.

Muda kama huu nilikuwa nimekaa katika darasa la Muungano wa Usaidizi wa Akina Mama wakati mwalimu alipoelezea historia ya ndugu wa karibu. Wakati akisubiria kwenye mataa, ndugu alihisi msukumo wa kubaki pale aliposimama wakati taa za kijani zilipowaka. Aliusikiliza mwongozo ule, na muda mfupi gari kubwa likaja kukatiza kwenye makutano, likipita kwenye taa nyekundu. Kama asingesikiliza na kutii sauti ile, yeye na watoto wake wangeweza kujeruhiwa au hata kuuawa.

Habari hii ilinigusa sana, lakini nilipokaa katika kiti changu nikilia nikijiandaa kusimama na kuondoka, ufariji mkubwa ulinisafisha. Nilihisi amani kwamba Roho Mtakatifu hakika alikuwa pamoja nami. Kwa upande wangu Hakuwepo pale kama sauti ya tahadhali bali kama mfariji.

Tokea wakati wa ajali ya Ben, nimehisi nguvu kuliko zangu mwenyewe na nimefarijiwa kwa upendo wa Baba yangu wa Mbinguni. Nilikosa uelewa wakati fulani wa kwanini baadhi ya vitu hutokea, lakini sijawahi kuwa na wasiwasi wa upendo Wake.

Nina imani kwamba Mungu anaelewa mambo yote na kamwe hatoniacha bila ufariji. Roho Mtakatifu ana nafasi nyingi katika maisha yetu. Anaweza kutulinda, lakini pia Anatuongoza, anatufariji, anatufundisha, na huleta uelewa na baraka nyingine.

Nilijifunza kwamba Baba wa Mbinguni hutimiza ahadi Zake. Mara zote amekuwa pamoja nami. ■

Robyn Casper, Utah, USA

VIELELEZO NA BRADLEY H. CLARK

Nikawaona wavulana wawili wenye umri kama miaka mitano na saba wakikimbia kwenye sehemu ya maegesho ya magari machozi yakiwatiririka chini ya nyuso zao.

ROHO ALININONG'ONEZEA

"Enyi, jamaa! Rudini!" sauti yenye majonzi ikaita.

Nikageuka na kuwaona wavulana wawili wenye umri wa miaka karibu mitano na saba wakikimbia kwenye sehemu ya maegesho ya magari machozi yakiwatiririka chini ya nyuso zao. Muuzaji alikuwa na wasiwasi wakati anawaita.

Nilipogeuka upande wa gari langu, Roho alininong'oneza, "Unaweza kuwa msaada hapa." Mnong'ono ulikuwa wa kimya lakini dhahili kwamba muda mfupi baadaye nilikuwa nikikimbia kwenye maegesho ya magari kuelekea kwa wale wavulana.

Nilimkuta yule mkubwa amesimama karibu na minivani ya kahawia. Nilimsogelea na kupiga magoti pembeni yake.

"Helo. Jina langu ni Christina. Je uko salama?"

Baada ya maneno yangu, alilia zaidi na kuuficha uso wake katika mikono yake. Muuzaji na mvulana mwingine walijumuika nasi.

"Nafikiri wanaongea Kifaransa pekee," muuzaji aliniambia. "Ndiyo kwanza Tuliwaona wakikimbia kupitia dukani, wamepotea."

Nikarudia utambulisho kwa wale watoto kwa Kifaransa. Kifaransa kilikuwa ndiyo lugha yangu ya kwanza, lakini nimekuwa siitumii toka nilipo asiliwa na familia inayoongea-Kiingereza nikiwa mtoto mdogo. Kwa kawaida, Kifaransa changu si-kizuri. Kwa wakati huo, hata hivyo, hakikuwa sio stadi wala rasmi. Maneno yalikuwa wazi katika fikra zangu na sauti yangu wakati nawafariji wale wavulana.

Katikati ya kilio cha kwikwi,kijana mkubwa alieleza kwa mbubujiko wa haraka wa maneno kwamba yeye na ndugu yake hawakuweza kuwaona wazazi wao mahali popote katika duka na ilibidi wakimbie nje ya duka kuwatafuta. Nilipokuwa nasikiliza,niliweza kwa mashaka kutambua kwa jinsi ya kushangaza ilikuwa kwamba sikuwa tu naongea kwa uhuru kifaransa lakini pia bila shida kuelewa na kufariji watoto wawili waliotishika.

"Wamepotezana na wazazi wao na wanataka kuwasubiri hapa kwenye gari lao," nikamwambia muuzaji. Mvulana mdogo alinitajia majina ya wazazi wake, ambayo nilimpa muuzaji ili awaite kwa kipaza sauti. Dakika chache baadaye mvulana akamwona baba yake akitoka nje ya duka na kukimbia ili kumlaki.

Nilipokuwa namfuata yule mvulana kwa baba yake, nikagumdua kwamba nilishindwa hata kusema kwaheri kwa Kifaransa. Nilijaribu kuongea chochote ambacho wale wavulana wangenielewa, lakini nilishindwa kusema chochote zaidi ya maneno mchanganyiko. Mwishowe, nikarudi kwenye Kiingereza, nikimwambia yule mvulana, "Kwaheri. Ilikuwa vizuri kukutana nawe."

Nilipowaacha wale wavulana na wazazi wao, nilijawa na shukrani. Baba wa Mbinguni alifanyakazi kupitia mimi ili kuwafariji watoto Wake wawili. Nilikuwa na unyenyekevu kwamba Bwana alikuwa ameongeza uwezo wangu mdogo ili kutimiza nia Yake. Nilikuwa na shukurani kushuhudia nini kinaweza kutokea tunapojitoa wenyewe Kwake pale tunapoitwa, hata sehemu isiyowezekana. ■

Christina Albrecht Earhart,
Washington, USA

LAZIMA TWENDE HEKALUNI SASA!

Jumapili moja asubuhi muumini aliye batizwa hivi karibuni alitambulishwa kwenye kata. Jina lake lilikuwa Lydia. Alikuwa amezikonga nyoyo zetu mara moja.

Lydia alikuwa mzee na kipofu kutokana na miaka mingi ya kupambana na kisukari. Kwa haraka aliwajua waumini wa kata kwa sauti zao na vishindo vya hatua zao. Aliyataja majina yetu na kutushika mikono, na hatukudokezwa hata kidogo kwamba alikuwa kipofu.

Baada ya subira ya mwaka mmoja kama inavyotakiwa, Lydia alikutana na askofu na raisi wa kigingi kupokea kibali chake cha hekaluni. Katika Muungano wa Usaidizi wa Kina mama Jumapili moja, alinivuta karibu naye na kuniambia, "Raisi wa kigingi aliniambia lazima niende hekaluni haraka iwezekanavyo. Utanipeleka?"

Ilikuwa ni wiki ya kwanza ya Desemba—wakati wa shughuli nyingi ulikuwa umetukaribia. Nilijaribu kutoa sababu za kawaida na kusema, "Hatuwezi kusubiri hadi Januari?"

"Hapana, lazima tuende sasa!"

Kundi la wanawake toka kwenye kata yetu walikwenda hekaluni kila mwezi, hivyo nikawaendea ili waende pamoja na Lydia. Nao pia walikuwa na shughuli nyingi. Lakini Lydia, akiwa na machozi machoni mwake, akatuambia tena raisi wa kigingi amemwambia aenda haraka iwezekanavyo.

Kwa hilo wote tulikubaliana kusafiri maili 150 (241 km) wiki iliyofuata. Tukiwa njiani, gari lilijaa wanawake wanane wenye kubwabwaja na urafiki. Lydia alikuwa na furaha isiyo na kifani kwa tukio lake la kwenda hekaluni na baraka ya kupokea endaumenti yake.

Wiki ya kwanza ya Januari, hali ya Lydia ikazidi kuwa mbaya na akapelekwa hospitali kwa ajili ya uangalizi wa dharura. Wiki moja baadaye akafariki. Lakini Lydia alikwenda na baraka za milele alizozipokea katika hekalu wiki chache zilizopita.

Baadaye nikaielezea ile habari kwa raisi wa kigingi juu ya safari yetu na nikamwambia jinsi nilivyo furahishwa kwa jinsi alivyoongozwa kumwambia Lydia lazima aende hekaluni mara moja.

"Hakika sikuwa na maana lazima aende sasa," alijibu. "Mara nyingi nawaambia wanaothibitishwa kwenda hekaluni haraka. Roho aliongea na Lydia, siyo mimi!"

Lydia alitufundisha sisi wote kumsikiliza Roho na kutenda hayo mara moja. Nina shukuru kwa kukumbuka kwake kuisikiliza sauti ndogo, nyororo. ■

Mary Holmes Ewen, California, USA

"Raisi wa kigingi aliniambia lazima niende hekaluni haraka iwezekanavyo," Alisema Lydia. "Utanipeleka?"

Na Mzee
Anthony D. Perkins
Wa Sabini

ENDELEENI KWA Imani

Ninyi vijana sasa mnaishi katika kile kinachoitwa "Muongo wa Maamuzi." Mnafanya maamuzi mengi ya chaguzi muhimu za maisha yenu, kama vile "kwenda hekaluni, kutumikia misheni, kupata elimu, kuchagua taaluma, na kumchagua mwenza na kuunganishwa kwa maisha haya na kwa milele yote katika hekalu takatifu."[1]

Ninaongea mahususi kwa wale wanaosumbuka na chaguzi muhimu moja au zaidi ya hizi ya chaguzi muhimu—wengine huenda wanapooza kwa woga wa kufanya maamuzi mabaya au kutaka kuimarishwa kuendelea kuwa na imani kwa uamuzi uliofanywa hapo awali.

Masomo manne ya kutukuka ya kufanya uamuzi na Nefi, kama yanafuatwa, yanaweza kupunguza woga wako na kuongeza kujiamini kwako kusonga mbele.

1. Tii Amri

Mstari wa mwisho wa kumbukumbu tukufu za Nefi zilifumbua maisha yake: "Kwani Bwana ameniamuru hivi, na ni lazima nitii" (2 Nephi 33:15).

Imani ya Nefi na upendo kwaajili ya Mwokozi inajionyesha kwenye utii wake katika amri za Mungu. Aliomba (ona 1 Nephi 2:16). Alisoma maandiko (ona 1 Nephi 22:1). Alitafuta na kufuata mwongozo toka kwa nabii aliye hai (ona 1 Nephi 16:23–24). Utii kama huo ulimruhusu Roho Mtakatifu kuwa na Nefi kwa nguvu katika maisha yake yote na kufuata ufunuo binafsi uliokuwa unaendelea.

Wewe pia lazima ukae karibu na Bwana kwa kutii amri za Mungu. Ninashuhudia kwamba utii endelevu katika mambo madogo kama ya kusoma maandiko, kusali daima, kuhudhuria ibada Kanisani, kufuata ushauri wa manabii walio hai, na kuwatumikia wengine kutakusaidia wewe kuwa na Roho—na ufunuo unaopatikana.

Ukamilifu siyo sharti kwa ufunuo binafsi. Sharti ni toba ya kila siku (ona Warumi 3:23). Kama toba yako ni ya kweli na kamilifu (ona M&M 58:42–43), nguvu ya utakaso ya Upatanisho itamleta Roho akuongoze katika maamuzi magumu ya maisha.

Masomo manne ya kutukuka ya kufanya uamuzi na Nefi yanaweza kupunguza hofu yako na kukuongezea kujiamini ili kusonga mbele.

2. Songa Mbele katika Imani

Jiweke mwenyewe kwenye kandambili za Nefi. Baba yako anakuambia Bwana ameiamuru familia yako kuuacha utajiri na kuondoka kwenda

UFAFANUZI KUTOKA *ROHO YA MAOMBI,* NA CLAUDIO ROBERTO AQUIARRAMIRES

Imani ya Nefi na upendo wake kwa Mwokozi vinajidhihirisha katika utii wake wa amri za Mungu.

nyikani. Hutopenda kujua juu ya safari yako na huko uendako?

Nafikiri Nefi angekuwa amesisimka kama Bwana angekuwa amefunua yale yajayo. Lakini hivyo sivyo Mungu alivyofanya kazi na Nefi, na sivyo atakavyofanya kazi na wewe.

Wakati familia ya Nefi ilipokuwa ikisafiri nyikani, miongozo ilikuja kwake pekee "kila mara" (1 Nefi 16:29; 18:1). Akiitafakari safari ya maisha yake kwa uhakika asingeweza kupewa nafsi iliyonyooka na uzoefu wa imani iliyojengeka ambayo ilimsaidia kuwa mtu mwenye tabia ya Kristo.

Kama unasubiri Mungu kukufunulia ni taaluma gani uisomee, nani wa kumuoa, kazi gani uikubali, wapi kwa kuishi, au kuendelea na masomo ya juu, na uzae watoto wangapi, huenda usingeweza kuondoka kwenye nyumba yako. Ninashuhudia kwamba ufunuo utakuja tu "Wakati fulani fulani."

Baba yetu wa mbinguni anataka sisi tukue, na hiyo inajumuisha kukuza uwezo wetu wa kujua mambo, kutoa hukumu, na kufanya maamuzi. Lakini pia anatualika kuleta maamuzi yetu Kwake kwa njia ya sala (ona M&M 9:7–9). Mzee Richard G. Scott wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili amefundisha kwamba majibu ya maombi yetu yanakuja "katika moja wapo ya *njia* tatu."[2]

Kuthibitisha Imani

"Kwanza," Mzee Scott alisema, "unaweza kuhisi amani, ufariji, na uhakika ambao unathibitisha kwamba uamuzi wako ni sahihi."[3] Mke wangu, Christy, na mimi tumegundua kwamba uthibitisho kwa maamuzi yanayo athiri maisha yanaweza kuwasilishwa kupitia maandiko, mara nyingi baada ya ibada ya hekaluni.

Kwa mfano, baada ya kutafakari kwingi na kuomba, tuliamua kuiacha nyumba ya ndoto yetu huko Texas, tukakubali uhamisho wa kikazi, na kuhama na watoto sita kwenda Beijing, China. Lakini kwa kukata tamaa tulitamani uthibitisho wa kiroho kwa uhamisho kama huu. Uhakikisho mtakatifu ulikuja kwetu—katika hekalu—tukiwa tunasoma maneno haya katika Mafundisho na Maagano: "Ni mapenzi yangu kwamba unatakiwa usikawie siku nyingi katika sehemu hii; usifikirie mali yako. Nenda katika nchi za mashariki" (M&M 66:5–7).

Sauti ya Yesu Kristo katika maandiko, ikiambatana na hisia zenye nguvu toka kwa Roho Mtakatifu, ilithibitisha kwamba uamuzi wetu wa kuhamia kwenda China ulikuwa sahihi.

KUPUNGUZA WOGA NA KUONGEZA KUJIAMINI

1. Tii amri.
2. Songa mbele katika imani.
3. Ishi maisha ya sasa.
4. Sogea karibu na nguvu za wengine.

FURAHA YAO ILIJAA TELE NA WALTER RANE, HESHIMA YA MAKUMBUSHO YA HISTORIA YA KANISA

Nefi angekuwa amesisimka kama Bwana angekuwa ameweka wazi mambo yake ya baadaye. Lakini hivyo sivyo Mungu alivyofanya kazi na Nefi, na si hivyo atakavyofanya kazi na wewe.

Mawazo yasiyotulia

Njia ya pili Baba wa Mbinguni anavyo jibu sala ni kupitia "hisia zisizotulia, mzubao wa mawazo, ikionyesha kwamba uchaguzi wako si sahihi."[4]

Baada ya misheni yangu huko Taiwan, nilifikiri uanasheria wa kimataifa ungekuwa chaguo zuri la kazi. Wakati Christy na mimi tulivyofikiria kwamba uwezekano wa baadaye, tulielewa kwamba miaka mitano zaidi ya elimu ya gharama ilikuwa mbele yetu.

Uchumi wa Marekani ulikuwa umeshuka sana na akiba zetu za pesa zilikuwa kidogo, hivyo tukafikiria kwamba kujiunga na Jeshi la Anga ROTC litakuwa ni chaguo la busara ili kujilipia shule. Lakini nilipofanya mitihani iliyotakiwa na kujaza fomu, hakika hatukujisikia vizuri kufanya yale maamuzi. Hakuna mzubao wa mawazo au hisia zenye giza—ni ukosefu wa amani.

Kile kilicho jifanya maamuzi yasiyo na mantiki kifedha yalihuishwa, katika sehemu ndogo, kwa sababu ningekuwa mwanasheria mbaya!

Uaminifu Mtakatifu

Mungu anajibu maombi kwa njia ya tatu: hakuna jibu. "Wakati unapoishi kwa haki na uchaguzi wako unabaki vilevile katika mafundisho ya Mwokozi na unahitaji kutenda," Mzee Scott alisema, "endelea kwa kuamini."[5]

Jaribio la mwisho la Nefi la kupata mabamba ya shaba linaonyesha ni jinsi gani tunatakiwa kuendelea katika kuamini. Alirekodi:

"Na nikaongozwa na Roho, wala sikujua toka mwanzo vitu ambavyo ningefanya.

Hata hivyo nikaenda mbele" (1 Nephi 4:6–7).

Wakati utawadia kipindi cha muongo wako wa maamuzi wakati ambao huwezi kuahirisha zaidi na lazima kutenda. Nimejifunza kwanza, kama Mzee Dallin H. Oaks wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili amefundisha, "tutapata mwongozo wa Roho pale tutakapofanya kila kitu tunachoweza, pale tutakapokuwa nje juani tukifanya kazi badala ya kukaa kivulini tukiomba kwa ajili ya mwongozo wa hatua ya kwanza ya kuchukua."[6]

Kama ilivyokuwa kwa Nefi, Roho katika muda muafaka atathibitisha au kukuonya njia uliyochagua.

3. Ishi Kisasa

Kujitoa kwa Nefi kwenda nchi ya ahadi kunasimama kama kizuizi cha kaka zake Lamani na Lemueli. Walifanya uamuzi wa kwenda, lakini mioyo yao haikuondoka Yerusalemu. Nefi alikuwa akitengeneza upinde wake uliovunjika ili awinde kwa ajili ya chakula na kupasua mbao ili kutengeneza meli wakati kaka zake wakiwa wakicheka kwenye hema.

Leo ulimwengu una akina Lamani na Lemueli wengi. Lakini Mungu anahitaji wanaume na wanawake waliojidhatiti kama Nefi. Utapata uzoefu mkubwa kimaendeleo katika maisha unapojitoa kabisa katika maamuzi yako na kujitahidi kufanya vizuri zaidi katika hali yako ya sasa hata wakati una jicho linaloangalia baadae.

Nefi anaonesha kwa mfano ushauri wa busara wa Rais Thomas S. Monson: "Ndoto za mchana zilizopita na kutamani ya baadae inaweza kutoa faraja lakini haiwezi kuchukua nafasi ya kuishi katika maisha ya sasa. Hii ni siku ya nafasi yetu, na lazima tuishike."[7]

4. Kuwa karibu na Nguvu za Wengine

Hata baada ya kutaka kuwa na Roho, tusonge mbele na uamuzi wetu, na tuwe tumejitoa kabisa, shaka zaweza kuendelea kujitokeza na kusababisha sisi kujiuliza uamuzi wetu. Katika hali kama hiyo familia iliyoaminika au rafiki anaweza kutoa ushauri na nguvu ya kuendelea kubaki kwenye njia. Ninashauri kwamba katika safari yake, mke wa Nefi akawa nanga yake ya kuaminika.

Shukrani kwa mke wa Nefi zikaja kwangu wakati nikitembelea Kumbukumbu za Historia ya Kanisa. Nilishangazwa na picha ya kuchorwa ya Nefi aliyokuwa amefungwa kwa nguvu kwenye mlingoti wa boti, akiwa amelowa sana kwa dhoruba kali.[8]

HELPMEET, NA K. SEAN SULLIVAN

Kwenye upande wa Nefi walikuwa mke wake na mmoja wa watoto wake. Alikuwa anapitia tukio hilo hilo la dhoruba na changamoto kama Nefi, lakini macho yake yalikuwa na ujasiri na mikono yake ilikuwa inamlinda imezungushwa mabegani mwake. Katika wakati huo nilitambua kwamba nami pia nilikuwa nimebarikiwa kuwa na mwenza mwaminifu anayenipa nguvu wakati wa majaribu. Nilitumaini kwamba nami nilikuwa ni nguvu kwake.

Ndugu, kutunza na kuongeza nguvu za kiroho ulizozianzisha (au ambazo mtazianzisha) kama mmisionari au katika huduma nyingine za haki ni rasilimali nzuri kwako katika kuwa mume na baba mwema. Akina dada, kiwango cha kuhisi cha kiroho, imani, na ujasiri wa kumfuata Yesu Kristo ni miongoni mwa tabia zenu bora kama mke na mama.

Ninakualika kuwa aina ya mtu ambaye mwenza wako wa sasa au baadaye anaweza kutoa ushauri wenye busara na nguvu. Mwanamume muadilifu na mwanamke mstahiki, waliounganishwa katika milele yote kwenye hekalu, wanaweza kufanya mambo magumu kama wenza sawa.

Ninaahidi kwamba kama mtayatumia mafundisho mliyojifunza toka kwa Nefi na manabii wa sasa kuhusu kufanya maamuzi, mtaongozwa na ufunuo binafsi "kila mara." Unapoendelea katika muongo wa uamuzi, ninaomba, kama alivyokuwa Nefi, kuwa na imani ya kusema:

"Na nikaongozwa na Roho, wala sikujua mapema vitu ambavyo ningefanya.

Hata hivyo niliendelea mbele" (1 Nefi 4:6–7). ■

Toka katika mkutano wa mafundisho, "Hatahivyo niliendelea ," yaliyotolewa kwenye Chuo Kikuu cha Brigham Young tarehe 4 Februari, 2014. Kwa nakala nzima katika Kingereza, nenda speeches.byu.edu.

Mwana familia aliyeaminika au rafiki anaweza kutoa ushauri na nguvu kubaki katika njia.

MUHTASARI

1. Robert D. Hales, "Kwa Wenye Ukuhani wa Haruni: Kujiandaa kwa ajili ya Muongo wa Uamuzi," *Liahona,* Mei 2007, 48.
2. Richard G. Scott, "KutumiaKipawa cha Maombi Kutoka Juu," *Liahona,* Mei 2007, 10; emphasis in original.
3. Richard G. Scott, "Kutumia Kipawa cha Maombi Kutoka Juu," 10.
4. Richard G. Scott, "Kutumia Kipawa cha Maombi Kutoka Juu," 10.
5. Richard G. Scott, "Kutumia Kipawa cha Maombi Kutoka Juu," 10.
6. Dallin H. Oaks, "Katika Wakati Wake Mwenyewe, katika njia Zake Mwenyewe," *Liahona,* Aug. 2013, 26.
7. Thomas S. Monson, "Katika kutafuta Hazina," *Liahona,* May 2003, 20.
8. Ona *Helpmeet,* by K. Sean Sullivan, in "Kitabu cha Mormoni: A Worldwide View," *Liahona,* Dec. 2000, 37.

MTAFUTE YEYE

"Kwa nini mnamtafuta aliye hai katika wafu?
Hayupo hapa, bali amefufuka."
(Luka 24:5-6.)

HAYUPO HAPA, NA WALTER RANE

MASOMO YA JUMAPILI

Mada ya Mwezi Huu:
Ukengeufu na Urejesho

KWA SABABU YA JOSEPH

Tambua njia sita za maisha yako yalivyo (au yanaweza kuwa) tofauti kwa sababu ya Nabii Joseph Smith.

Na Ted Barnes
Idara ya Ukuhani

Joseph Smith alikufa zaidi ya miaka 170 iliyopita. Aliishi miaka 38 tu, akitumia zaidi ya muda huo katika sehemu za kujificha ambazo huenda wewe pengine huwezi kuzipata popote isipokuwa kwenye ramani yenye maelekezo ya kina. Na huenda pengine una mazoea na vitu vingi alivyovifanya katika maisha yake. Lakini umewahi kufikiria jinsi yanavyo kuathiri wewe binafsi? Wakati njia hizo ni nyingi kuzihesabu, unaweza kuanza na hizi sita.

Kwa sababu ya Joseph Smith:

1. Unaelewa Mungu na Yesu Kristo ni nani haswa.

Hata kama haingekuwa kwa Joseph Smith, bado ungeamini katika Mungu Baba na katika Yesu Kristo. Ungekuwa na ushuhuda wa Biblia. Lakini fikiria kiasi gani kwa undani na ametajirisha zaidi uelewa wako ni kwa sababu ya kile Joseph Smith alirejesha—ujasiri, ushuhuda uliokubalika wa Kitabu cha Mormoni, Mafundisho na Maagano, na Lulu ya Thamani Kuu. Kwa mfano, unajua kitu ambacho watu wengi wa ulimwengu hawakijui: kwamba Mwokozi mfufuka alijidhihirisha huko Marekani—akithibitisha, kwa maneno Yake, kwamba Yeye si tu "Mungu wa Israeli, [bali pia] ni Mungu wa ulimwengu wote" (3 Nephi 11:14).

Fikiria jinsi ushuhuda wako wa Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo unavyo imarishwa kwa ushahidi wa nguvu wa manabii kama Nefi, Alma, na Moroni—bila kumsahau Joseph Smith mwenyewe, aliyetangaza: "Anaishi! Kwani tulimwona yeye, hata katika mkono wa kuume wa Mungu" (M&M 76:22–23). Katika siku ambayo imani kwa Mungu na Yesu Kristo inapingwa na mara nyingi kutelekezwa, ni baraka za aina gani ya kuwa na mwanga huu wa ziada!



3. Familia yako yaweza kuwa ya milele.

Kwa nini watu wengi wanachanganyikiwa kuhusu umuhimu wa ndoa na familia? Huenda ni kwa sababu hawajui mafundisho, yaliyo rejeshwa kupitia Joseph Smith, kwamba ndoa na familia vimetawazwa na Mungu na vimepangwa kuwa vya milele (ona M&M 49:15; 132:7). Hizi siyo desturi zilizotengenezwa na mwanadamu ambazo jamii yetu imekuwa nazo—ni sehemu ya mpango wa milele wa mbinguni. Na asante kwa funguo za ukuhani na ibada za hekalu ambazo zilirejeshwa kupitia Joseph Smith, familia yako ya milele inaweza kuanzia hapa duniani.

2. Unajua kwamba wewe ni mwana wa Mungu—na hivyo ndivyo kila mmoja.

Pengine ukweli muhimu sana aliorejesha Joseph Smith kilikuwa ni ukweli kuhusu uhusiano wetu na Mungu.[1] Yeye ni Baba yetu halisi. Umeshawahi kuacha kufikiria kuhusu vitu ambavyo vinatokana na ukweli ule? Inabadilisha jinsi unavyojiona mwenyewe: bila kujali ulimwengu unafikiria nini juu yako, unajua kwamba wewe ni mtoto mpendwa wa Mungu, ukiwa na sifa zake ndani yako. Inabadilisha jinsi unavyo waona wengine: ghafla kila mmoja—*kila mmoja*—ni kaka au dada yako. Inabadilisha jinsi unavyo yaona maisha yenyewe: furaha zake zote na majaribu ni sehemu ya mpango wa Baba wa Mbinguni kukusaidia wewe kuwa kama Yeye alivyo. Hakuna kitu kibaya kwenye nyimbo unazoimba kwenye darasa la watoto![2]

4. Unayo njia ya kufikia ukuhani na baraka zake.

Kwa sababu Mungu alirejesha ukuhani Wake kupitia Joseph Smith, unaweza kubatizwa, na kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Unaweza kutafuta baraka za ukuhani wa uponywaji, faraja, na mwongozo. Unaweza kufanya maagano matakatifu ambayo yanakuunganisha na Mungu. Na unaweza kuyarudia maagano upya kila wiki wakati unapokula sakramenti. Kupitia ibada za ukuhani, nguvu za Mungu zinaingia katika maisha yako (ona M&M 84:20–21). Hakuna kati ya hili linalowezekana bila ya kazi iliyokamilishwa kupitia Joseph Smith.

KUSHOTO: *MATAMANIO YA MOYO WANGU (ONO LA KWANZA)*, NA WALTER RANE; JUU: HEKALU LA ASUNCIÓN PARAGUAY

5. Upo huru kutokana na matumizi mabaya ya madawa ya kulevya.

Au angalau unaweza kuwa kama unatii ufunuo wa Joseph uliopokelewa huko nyuma mwaka 1833—zamani kabla tumbaku haijagundulika kitabibu kuwa inasababisha saratani ya mapafu na pombe ilihusishwa na ugonjwa wa ini. Wakati unapokuwa na nabii akifunua hekima za Mungu, kwa nini usubiri hekima za ulimwengu zikufikie? Neno la Busara linaonyesha kwamba Mungu hazijali roho zetu pekee bali pia kuhusu miili yetu (ona M&M 89). Baada ya yote, kama vile ufunuo kwa Joseph Smith ulivyoelezea, kuwa na mwili kunatufanya sisi zaidi—siyo kidogo—kuwa kama Baba yetu wa Mbinguni, ambaye pia ana mwili wa nyama na mifupa (ona M&M 130:22).

JIUNGE NA MAZUNGUMZO

MAMBO YA KUTAFAKARI KWA AJILI YA JUMAPILI

- Ninawezaje kuimarisha ushuhuda wangu kwa Nabii Joseph Smith?
- Jinsi gani ninaweza kuonyesha vyema shukrani kwa nabii aliye hai kupitia maneno na matendo yangu?

VITU UNAVYOWEZA KUVIFANYA

- Katika Kanisa, ukiwa na familia yako na marafiki, au vyombo vya habari vya kijamii, shiriki jinsi Nabii Joseph Smith alivyovutia maisha yako.
- Kama alivyofanya Joseph Smith, muulize Baba wa Mbinguni maswali yako. Chukua muda wa kupiga magoti katika sala na muombe mwongozo. Baadaye, subiri na usikilize mawazo au hisia. Andika mawazo yako katika shajara yako.
- Soma mafundisho "Joseph Smith" na Mzee Neil L. Andersen wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili toka mkutano mkuu wa Octoba 2014. Weka mpango wa kuyatumia mawazo mawili anayoyatoa katika kujenga na kushiriki ushuhuda wako kwa Joseph Smith.

6. Unaweza kujua ukweli wewe mwenyewe kupitia Roho Mtakatifu.

Wakati kijana Joseph alipokwenda kwenye Kichaka Kitakatifu mwaka 1820, imani ya kawaida miongoni mwa makanisa mengi ilikuwa kwamba ufunuo ulikuwa ni kitu cha kale. Ono la Kwanza la Joseph linathibitisha kuwa si kweli. Mbingu ziko wazi—na si kwa manabii pekee. Yeyote mwenye swali anaweza kupata jibu kupitia unyenyekevu, kutafuta kwa dhati (ona M&M 42:61; 88:63). Kwa mfano, unaweza kujua mwenyewe kwamba Joseph Smith alikuwa ni Nabii wa Mungu kwa njia ile ile aliyotumia Joseph: kwa kumwuliza Mungu Mwenyewe.

Orodha hii ni mwanzo tu. Ungeweza kuongeza nini? Maisha yako yanatofauti gani kwa sababu ya Joseph Smith? ■

MUHTASARI

1. Ona *Teachings of Presidents of the Church: Joseph Smith* (2007), 37–44.
2. Ona "Mimi ni Mwana wa Mungu," *Hymns,* no. 301.

“Nabii aliye hai ni muhimu zaidi kwetu kuliko yule aliye kufa. . . .

Ufunuo wa Mungu kwa Adam haukumwelezea Nuhu jinsi ya kujenga Safina. Nuhu alihitaji ufunuo wake mwenyewe. Kwa hiyo, nabii aliye muhimu sana, kadiri mimi na wewe inavyotuhusu , ni yule anayeishi katika siku na zama zetu ambaye Bwana kwa sasa anamfunulia mapenzi yake kwa ajili yetu. Kwa hiyo, somo muhimu sana tunaloweza kufanya ni maneno yoyote ya nabii ambayo yanapatikana kwenye majarida ya Kanisa ya kila mwezi. Mwongozo wetu kwa kila miezi sita unapatikana kwenye mafundisho ya mkutano mkuu, ambayo yanachapishwa kwenye *[Liahona]* jarida.

Kuweni waangalifu kwa wale watakao wadharau manabii waliokufa dhidi ya manabii walio hai, kwani **manabii walio hai mara zote huchukua nafasi ya kwanza.”** ■

Na Rais Ezra Taft Benson (1899–1994), “Misingi na kanuni Kumi na Nne katika Kumfuata Nabii” (Brigham Young University devotional, Feb. 26 1980), 2, speeches.byu.edu.

Shiriki Mawazo Yako
Inamaanisha nini kwako kuwaidhinisha manabii waliohai? Shirikisha mawazo yako pamoja na familia na marafiki au mitandao ya kijamii.

MFANO WA MWOKOZI *wa Utiifu*

Mfano wake uliweka utaratibu kwa ajili yetu wote ili tuufuate.

"Katika masomo yote tunayojifunza kutoka katika maisha ya Mwokozi, hakuna kilicho wazi na chenye nguvu zaidi ya somo la utii," alifundisha Mzee Robert D. Hales wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili katika mkutano mkuu wa Aprili 2014. Mfano wa Mwokozi unatufundisha siyo tu *kwa nini* utiifu kwa Baba wa Mbinguni ni muhimu lakini pia *ni jinsi gani* tunaweza kuwa watiifu. Unapopitia upya mifano ifuatayo toka kwenye utumishi Wake, fikiria jinsi unavyoweza kutengeneza njia kwa ajili ya kuifuata katika maisha yako.

"MIMI **SITAFUTI** MAPENZI YANGU MWENYEWE, LAKINI **MAPENZI YA BABA** AMBAYE AMENITUMA MIMI."

(Yohana 5:30; pia ona Yohana 6:38; 8:28–29; 14:31)

UNAWEZA KUFANYA NINI?

Mzee Hales alisema, "Yesu alifundisha kutii katika lugha rahisi ambayo ni rahisi kuielewa: 'Kama unanipenda, tii amri zangu' [Yohana 14:15], na 'Njoo, unifuate' [Luka 18:22]."

Utafanya nini leo ili kuwa mtiifu zaidi?

1. *Japokuwa Yesu hakuwa na dhambi, alikubali ubatizo "ili kutimiza haki yote"* **(Mathayo 3:13–17; onapia 2 Nefi 31:4–7; Yohana 3:5).**

2. *Akiwa na umri wa miaka 12, wakati Joseph na Mary walipompata Yesu akifundisha hekaluni, Aliwatii wao, "na kwa utiifu alirudi nyumbani pamoja nao"* **(ona Luka 2:42–51).**

3. *Japokuwa Aliomba kama kikombe kingemwepuka, Alijitoa na kuteseka katika Bustani ya Gethsemen* **(ona Mathayo 26:36–44; Luka 22:39–54).**

4. *Aliitii siku ya Sabato na alihudhuria ibada katika sinagogi* **(ona Luke 4:16–44).**

5. *Yesu alijitoa ili ahukumiwe na wanadamu ili kazi ya Bwana na utukufu uweze kukamilika* **(ona Isaya 53:7; Mathayo 26:53; Musa 1:39).**

6. *Alimaliza kazi yake kwa kuruhusu watu waovu kumsulubisha Yeye* **(ona Mathayo 27:35; Yohana 10:17–18; Wagalatia 1:3–5).**

KWA SABABU MWOKOZI WETU ALIKUWA MTIIFU



"Kwa sababu Mwokozi wetu alikuwa mtiifu, Alilipia dhambi zetu, kufanya uwezekano wa ufufuko wetu na kuandaa njia kwaajili yetu kurudi kwa Baba yetu wa Mbinguni, ambaye alijua tungefanya makosa wakati tukijifunza utii katika maisha ya mwili wa kufa. Tunapotii, tunakubali dhabihu Yake, kwani tunaamini kwamba kupitia Upatanishi wa Yesu Kristo, watu wote wanaweza kuokolewa, kwa utiifu wa sheria, ibada, na amri zilizotolewa katika injili."

Mzee Robert D. Hales wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili, "'Kama Unanipenda, Shika Amri Zangu,'" *Liahona*, Mei 2014, 35.

1. *UBATIZO WA KRISTO*, NA JOSEPH BRICKEY; 2. *MTOTO YESU HEKALUNI*, NA GRANT ROMNEY CLAWSON; 7. *YESU AKIWA KATIKATI*, NA JUDITH A. MEHR; 8. *ONDOKA HAPA, SHETANI*, NA CARL HEINRICH BLOCH; 9. *ONO LA KWANZA LA JOSEPH SMITH*, NA GREG K. OLSEN





"KATIKA UTUMISHI WOTE WA [YESU], 'ALITESEKA NA **MAJARIBU** LAKINI **HAKUYASIKILIZA'** [M&M 20:22]."
—Mzee Robert D. Hales

7. *Wakati wote akiwa mtiifu kwa Baba Yake, Yesu alienda kwenye ulimwengu wa roho na kuanzisha kazi ya umisionari kule* **(ona 1 Petro 3:18–20; 4:6).**

8. *Yesu alijaribiwa na Shetani, lakini hakushindwa* **(ona Mathayo 4:1–11; M&M 20:22).**

9. *Aliendelea kufanya mapenzi ya Bwana na kuliongoza Kanisa* **(ona Joseph Smith—Historia 1:16–17; M&M 19:2, 24).**



JESHI LA ZIMAMOTO NA NGAO YA MUNGU

Ilikuwa siku tulivu kazini kwangu nikiwa kama mwana zimamoto wa kujitolea, hivyo nikaamua kusoma Kitabu cha Mormoni. Wakati mmoja wa wafanyakazi wenzangu aliponiona nikisoma, aliuliza kama nilijua jinsi gani tunaweza kuvaa ngao ya Mungu siku hizi. Tulipokuwa tukiongea, king'ora kikalia. Kulikuwa na moto kwenye duka la jirani.

Kwa haraka tukavaa magwanda yetu ya zimamoto na kuelekea huko. Miali ya moto ilikuwa mikubwa, na tulipolikaribia duka, kitu kikalipuka katika upande tuliokuwepo. Miali ya moto ikatuzingira. Mlipuko uliwakanganya wafanya kazi wenzangu na mimi kwa sekunde chache. Lakini asante kwa vyombo vyetu na nguo za kujikinga, hatukuumia.

Tuliporudi kituoni baada ya kupambana na moto, nilimwuliza mfanyakazi mwenzangu kama alikumbuka swali lake juu ya ngao ya Mungu. Alisema alikumbuka, na nikamwelezea kwamba ngao ya Mungu ni kama nguo za kujikinga za zimamoto. Lazima tuzivae mara zote ili tuweze kuhimili mashambulio ya nguvu ya adui. Kama tutatii amri, tutabarikiwa kwa nguvu za kujikinga za ngao ya Mungu, na Roho Mtakatifu atakuwa mwongozi wetu. ■

Fernando de la Rosa Marrón, Mexico

ANDIKO LANGU NILIPENDALO

1 Samweli 16:7. "BWANA HAANGALII KAMA AANGALIAVYO MWANADAMU; KWANI MWANADAMU HUANGALIA MUONEKANO WA NJE, LAKINI BWANA HUANGALIA KWENYE MOYO."

Kabla sijajiunga na Kanisa, mara nyingi nimejiona kama mtu wa kawaida nikiwa na uwezo wa kawaida. Nilijiona kwamba sikuwa na chochote cha thamani ninachoweza kutoa. Nilikuwa naogopa kuwaonyesha watu kuwa mimi ni nani kwasababu ya kuogopa kukataliwa na kuumizwa. Nilifikiri kwamba kila mtu aliyenizunguka alikuwa imara, mwenye akili, na mzuri zaidi yangu,

Lakini haya matarajio yote yalibadirika pale nilipokuwa muumini wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho. Nilijifunza kwamba sisi wote ni watoto wa Mungu na tulirithi tabia takatifu. Sasa ninaelewa kwamba hakuna mashindano ya nani mwenye akili, tajiri, au mwenye sura nzuri. Machoni pa Bwana, sisi wote tupo sawa, na Yeye ndiye anaye hukumu—siyo kwa kuangalia sifa za mwili wetu bali kwa utii wetu na kwa kutamani kwetu kufuata njia Alizoziweka. ■

Joan Azucena, Philippines

KIELELEZO NA JULIA YELLOW

UTAFANYA KAZI JUMAPILI?

Nilipokuwa na miaka 15, nilipata ushuhuda mkubwa wa injili ya Yesu Kristo na nilikuwa na furaha tele kujiunga na Kanisa. Wakati huo, nilikuwa nafanyakazi kuisaidia familia yangu. Si muda mrefu baada ya kubatizwa Hata hivyo, nilipoteza kazi yangu.

Nilitakiwa kutafuta kazi mpya haraka kwa sababu familia yangu ilinitegemea, lakini kila kazi niliyoomba ilihitaji nifanye kazi Jumapili. Nilikataa ofa za kazi nyingi kwasababu nilijua kwamba nilihitaji kuwa kanisani Jumapili (ona M&M 59:9–10).

Baada ya miezi miwili ya kutafuta, bado sikupata. Mama yangu hakuwa muumini wa Kanisa, na japokuwa alimwamini Mungu, alikuwa mwenye hasira sana kwa sababu nilikataa kazi nyingi sana.

Usiku mmoja aliniangalia akiwa na machozi machoni mwake na akauliza, "Kwa nini Mungu anayaacha haya yatokee kwetu wakati wewe ni mwaminifu sana katika kutenda kile kilicho cha haki?"

Nikajibu, "Mama, sijui ni kwanini hili linatokea kwetu, lakini ninajua kwamba ninafanya kitu sahihi, na ninajua kwamba Mungu atatubariki kwa hilo."

Asubuhi iliyofuata mtu mmoja alinipa kiasi kikubwa cha pesa ili nikitumie kwa siku mbili kuhamisha mizigo mizito toka nyumba moja hadi nyingine. Kazi ilikuwa ya kuchosha, lakini nilipopata pesa, nilikwenda moja kwa moja nyumbani na kutoa sala ya shukrani. Mara nikapata kazi nzuri ambayo iliniruhusu kupumzika Jumapili, na sijawahi kukosa kazi toka hapo.

Nina furaha kwamba nilichagua kuifanya takatifu siku ya sabato. Kuna changamoto nyingi katika maisha, lakini ninajua kwamba kama tutajitahidi kuwa imara licha ya changamoto hizo, Bwana atatubariki. ■

Sahil Sharma, India

Na Mzee
Neil L. Anderson
Wa Akidi ya Mitume
Kumi na Wawili

JINSI YA KUWA NA HEKIMA

Katika taarifa za siku hizi za mawimbi, tunahitaji sana hekima—hekima za **kutafakari na kutambua** jinsi ya kuyatumia yale tunayojifunza.

Acha tukumbuke:

1. Lazima tutafute hekima.
2. Hekima ni kubwa na inakuja katika ukubwa na rangi tofauti.
3. Hekima iliyopatikana awali inaleta baraka kuu.
4. Hekima katika upande mmoja haiwezi kuhamishwa kwa mwingine.
5. Hekima ya ulimwengu, katika hali nyingi ni yenye thamani, ni ya thamani kuu inapotumika kuabudu na kumheshimu Mungu.

Maandiko yanaelezea aina mbili za hekima: hekima ya ulimwengu na hekima ya Mungu. Hekima ya ulimwengu ina mambo yote mazuri na mabaya. Katika maelezo ya giza nene, inaweza kuelezewa kama baadhi ya ukweli, uliochanganyika na akili na hila, ili kufanikisha ubinafsi au malengo maovu.

Kuna aina nyingine ya hekima ya ulimwengu ambayo haikaribii uovu. Hakika inawezekana. Hekima hii inapatikana kwa kupitia **kujifunza, kufikiria, kuangalia, na kwa kazi ngumu.** Ni yenye thamani kubwa na inasaidia katika mambo tunayoyafanya. Kwa watu wazuri na wenye heshima, inakuja kama ilivyokuwa kwa mwili wetu wa kufa.

Muhimu zaidi, hekima inayoleta mafanikio katika ulimwengu lazima ikubali kurudi nyuma ya hekima ya Mungu na bila kufikiria kwamba inaweza kubadilishana nayo.

Siyo hekima zote zimeumbwa sawa. Tunahitaji kujifunza kwamba panapokuwepo na mvutano kati ya hekima ya ulimwengu na hekima ya Mungu, lazima **tuelekeze mapenzi yetu kwenye hekima ya Mungu.**

Ninashauri uchukue baadhi ya matatizo yanayo kukabili. Weka mstari katikati ya karatasi. Orodhesha hekima za ulimwengu upande wa kushoto na hekima za Mungu upande wa kulia. Andika vitu vyenye kupingana na vingine.

Ni chaguzi gani unazozifanya?

Katika sehemu ya 45 ya Mafundisho na Maagano, ambayo inaongelea matukio yanayo tuongoza kwenye Ujio wa Pili wa Mwokozi, Bwana tena anaelezea hadithi ya wanawali kumi na kisha akatuacha na maneno haya: "Kwani wale walio na hekima na kupokea ukweli, na kumchukua Roho Mtakatifu kuwa kiongozi wao, na hawajadanganywa—amini ninawaambia, hawatakatiliwa chini na kutupwa katika moto, bali watastahimili siku ile" (ona M&M 45:57).

Acheni **tuitafute hekima ya Mungu.** Kuna mengi tunayoweza kujifunza kwa sasa kuhusu hekima. Ninawaahidi kwamba baraka za Bwana zitawajia pale mtakapotafuta hekima, hekima ya Mungu. Anapenda sana kutoa hekima Zake kwetu. Na kama tutakuwa watiifu na wakuomba na kuhitaji, itakuja. ■

Toka Chuo Kikuu cha Brigham Young–Idaho hotuba ya mahafali yaliyotolewa Aprili 10, 2009.

JE, UMETUMIA VIPI HAYA?

"Mara zote kuna uwezekano wa aina mbili wa kuchagua. Unaweza kuchagua kile unachotaka. Lakini unatakiwa kuamua kwa busara. Ninaweza kusema kwamba kumchagua Bwana kunaweza kukusaidia kila siku kuwa na Roho Mtakatifu upande wako na kunaweza kukusaidia katika kila hali. Kuchagua upande usio sahihi kunaweza kukuongoza katika hisia zisizo za furaha ambazo zitaonekana kama furaha kwa muda mfupi lakini baadaye utaona matokea yake na utajutia vikali uchaguzi ulioufanya. Baki katika njia ya Bwana! Mara nyingi si rahisi, lakini ni vyema kufanya!"

Samuel J., Austria

KWA UFAHAMU

Ni sawa kwenda kwenye **dansi** au **sherehe** ambako ninajua **vitu viovu** vitakuwa vinaendela, itakuwa **mfano mzuri**?

Jiulize mwenyewe: "Ni mfano wa aina gani ambao mimi ninafikiria nitakuwa nauweka katika hali kama hiyo?" Kama unafikiria kwenda sehemu fulani ambayo inaweza kuwa na madawa au pombe, mavazi yasiyo na heshima, muziki wenye maneno ya kutamanisha, au muziki usio wa heshima, utawaonyeshaje watu jinsi gani wanaweza kuwa na furaha nyingi bila ya vitu hivyo? Ni jinsi gani watu wanao kuzunguka wanaweza kufikiria—"Je, huo sio mfano mzuri wa imani na viwango?" au "Kwa nini mtu yule hata akaja?" Mara nyingi, utakuwa mfano mzuri kwa kutokwenda kabisa, kwa sababu hutakuwa umedhamiria na kwa kujua kutojiweka hadharani kwenye majaribu. ■

Ni kiasi gani **ushawishi** unafanya **Shetani** awe na nguvu dhidi ya **mawazo yangu**?

Baba yetu wa mbinguni anahakikisha kwamba tuna uhuru wa kimaadili, uwezo wa kuchagua mema na mabaya. Hata tulazimisha kutenda mema, na ibilisi hata tulazimisha kutenda maovu (ona *Teachings of Presidents of the Church: Joseph Smith* [2007], 214).

Hivyo, wakati inapokuja kwenye mawazo yako, ibilisi ana ushawishi pale tu unapokubali kujiweka kwake. Nabii Joseph Smith alisema, "Shetani hawezi kutupotosha kwa ulaghai wake pengine sisi katika mioyo yetu tukubali na kusalimu amri" (*Mafundisho: Joseph Smith,* 213). Pia alisema, "Ibilisi hana uwezo dhidi yetu ila ni pale tu tunapomruhusu" (214).

Kwa nyongeza, maandiko yanatuambia kwamba "hakuna mwingine yeyote isipokuwa Mungu ambaye anayajua mawazo yako na nia ya moyo wako" (M&M 6:16), Kwa hiyo shetani hawezi kwa hakika kujua nini unachofikiria. Anaweza tu kuleta majaribu na ulaghai. Lakini kama utachagua kuyafuata, anapata nguvu kubwa dhidi yako na majaribu yanakuwa ya nguvu. Kwa ishara ileile, kama unastahimili maovu na kuchagua mazuri, utaimarishwa na kubarikiwa. ■

MAELEZO YA PICHA NA DAVE PETERSON

Kundi Moja *na* MCHUNGAJI MMOJA

Boma la kundi la kondoo hutufundisha kuhusu ulinzi wa Mwokozi kwa watu Wake.

Zizi la Kondoo la Kale

Ni nini: Zizi la kawaida, Boma la kuta.

Dhamira: Kulinda kundi la kondoo kutokana na wauaji, wezi hasa usiku

Vifaa na ujenzi: Mawe, kwa kawaida, na vichaka vyenye miiba mara kwa mara huwekwa juu ya kuta, Matawi makubwa yenye miiba pia yalitumika mara kwa mara kutengeneza ua la zizi la muda mfupi. Mapango wakati mwingine yalitumika kama zizi, na jiwe la wastani dogo au vizuizi vya miiba vikiwekwa mbele yake.



KIELELEZO NA DAVID HABBEN, MAELEZO KUTOKA KWA *CHRIST AND THE RICH YOUNG RULER,* NA HEINRICH HOFMANN

KWELI ZA BIBLIA

- Kondoo walikuwa na thamani sana kwa sababu ya nyama zao, mafuta, ngozi, na pembe na walikuwa kimsingi wanyama wa kutolewa kafara
- Katika Israeli, mbwa mwitu, fisi, chui weusi na mbweha ni baadhi ya wawindaji ambao wangelenga kondoo. Katika nyakati za kale, simba na dubu pia waliishi katika eneo lile (ona 1 Samueli 17:33–37).
- Wachungaji walitumia fimbo kuwaongoza kondoo na fimbo na kombeo kwa kuwalinda.
- Mchungaji aliwaongoza kondoo hadi kwenye malisho na maji wakati wa mchana (Ona Zaburi 23:1–2) na kuwarejesha zizini wakati wa usiku. Mchungaji angewahesabu kondoo waliporejea, akitafuta waliopotoka ikiwa kuna aliyekosekana . Kisha angelala kwenye mlango wa zizi ili kuwalinda.
- Yesu Kristo alijiita Mwenyewe Mchungaji Mwema (ona Yohana 10:11–15) kwa sababu alitoa maisha Yake kwa ajili yetu. Pia alijilinganisha na mlango wa zizi la kondoo (ona Yohana 10:1–9) kwa sababu ni kwa kupitia kwake ndipo tunapopokea malisho ya kiroho, pumziko, amani, wokovu na kuinuliwa.
- Mtume Paulo alilinganisha Kanisa na kundi la kondoo (ona Matendo ya Mitume 20:28).

KONDOO WENGINE

Mwokozi alizungumzia "kondoo wengine . . . ambao si wa zizi hili," (Yohana 10:16), akimaanisha Wanefi na Walamani waliokuwa wameongozwa mbali na nyumba ya Israeli (ona 3 Nefi 15:14–24). Alizungumzia pia ziara yake kwa makabila yaliyopotea ya Israeli (ona 3 Nefi 15:20; 16:1–3).

Kile Tunachoweza Kujifunza

Zizi za kondoo ni:

Pale ambapo kondoo hukusanyika. Kama waumini wa Kanisa, tunashiriki mfungo wa umoja kupitia kwa imani yetu na maagano yetu, na pia kwa kihalisi kukusanyika pamoja. Rais Henry B. Eyring, Mshauri wa Kwanza katika Urais wa Kwanza, amefundisha: "Furaha ya umoja [Baba wa Mbinguni] anataka sana kutupa sisi, sisi si pweke. Ni lazima tuitafute na kustahili pamoja na wengine. Si ajabu basi kuwa Mungu anatuhimiza kukusanyika pamoja ili Yeye aweze kutubariki. Anataka tukusanyike katika familia. Alianzisha madarasa, kata, na matawi na kutuamuru kukutana kila mara. Tunaweza kuomba na kufanyia kazi umoja huo utakaotuletea furaha na kuongeza uwezo wetu wa kuhudumu" ("Our Hearts Knit as One," *Liahona,* Nov. 2008, 69).

Mahali pa usalama na pumziko. Katika Yesu Kristo "tunapata raha nafsini [mwetu]" (Mathayo 11:29). Kanisa Lake ni "ngome, na . . . kimbilio" (M&M 115:6). Na kama vile Boyd K. Packer, Rais wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili alivyofundisha, "Tunapata usalama na ulinzi kwetu wenyewe . . . katika kuheshimu maagano tuliyofanya na kuishi kulingana na matendo ya kawaida ya utiifu yanayohitajika kwa wafuasi wa Kristo" ("These Things I Know," *Liahona,* May 2013, 7).

Kulindwa na Mchungaji. Yesu Kristo ni Mchungaji Mwema anayetuokoa. Aliteseka na kufa ili tuweze kushinda dhambi na kifo na kurejea kwaBaba yetu wa Mbinguni Tunapokuja kwa Kristo na kuwa watiifu kwa amri Zake, Anatubariki, Anatuongoza, na kutulinda sisi binafsi na kama watu wake wa agano. ■

"Ninawezaje kuridhika vya kutosha kuzungumza na askofu wangu kuhusu mambo au mashaka yangu?"

Unaweza kujisikia mwenye wasiwasi kumzungumzia askofu wako kuhusu mambo unayosumbuka nayo, na hiyo ni kawaida. Kila mara tunapata wasiwasi kabla ya matukio mapya au kabla ya kuzungumza na mtu mzima.

Lakini Askofu wako ameitwa na Mungu. Aliitwa kwa sababu ni mfuasi wa dhati wa Yesu Kristo. Atafanya juhudi kuwa mkarimu na muelewa. Dhamira yake ni kukusaidia kuja kwa Mwokozi ili upate amani. Mwanzoni, unaweza kuona soni kumzungumzia kuhusu maswali yako au dhambi, lakini hatakufikiria kuwa wewe ni mpungufu. Kwa hakika, atafurahi kuwa una hamu ya kuwa bora Na atatunza mazungumzo yenu ya siri.

Hupaswi kubeba mizigo yako pekee yako. Askofu wako anaweza kukusaidia kupata majibu ya maswali yako na ikibidi, kukusaidia kutubu na kushinda, kupitia Upatanisho wa Kristo, hisia za hatia, kuvunjika moyo, au kutostahili.

Unapozungumza na askofu wako utahisi upendo wake kwako. Ingawa ana jukumu la kata au tawi lote, lengo lake ni hali njema ya wavulana na wasichana. Humsumbui kwa kumwomba usaidizi.

Unaweza kusali kwa Baba wa Mbinguni akupe nguvu na ujasiri wa kuzungumza na askofu wako. Amemwidhinisha askofu wako kukusaidia na askofu wako ana hamu ya kufanya hivyo. Ukienda na moyo ulio wazi na hamu ya kuwa bora, utaona kwamba unapoondoka katika ofisi yake utakuwa unajisikia vyema zaidi ya ulivyokuwa hapo awali.

Hatakufikiria Kuwa Mpungufu

Askofu wa kata yako amepewa mamlaka kukuongoza kupitia hatua za toba. Mara nyingine kumgeukia askofu wako ni njia ya pekee kwako kutubu kikamilifu kupitia kwa Mwokozi. Nilipohitaji kumzungumza na askofu wangu, alinisaidia kumpata Mwokozi na kushinda kidonda kikuu nilichowahi kuwa nacho. Askofu wako anataka kukuasaidia. Wito wake ni kukulinda, na hatakufikiria kuwa mpungufu kwa sababu ya kitu unachohitaji kumwona.

Madison D., umri 18, Utah, Marekani

Askofu Wako Yu Tayari Kukusaidia

Nilikuwa nahisi vibaya katika mahojiano, lakini hatimaye niligundua kuwa askofu wangu alikuwa tayari kila wakati kunisaidia kutatua matatizo yangu. Mwamini askofu wako, yeye ni mchungaji na kata ni kundi lake.

Jaime R., umri 19, Cochabamba, Bolivia

Hataisaliti Imani Yako

Nimekuja kujua kuwa askofu ni mtu mzima pengine anayeaminika zaidi ambaye kijana anaweza kutafuta usaidizi kutoka kwake. Hataweza kamwe kusaliti imani yako—kila kitu unachomsimulia husalia pale ofisini mwake Wakati mwingine ni vigumu sana kusimulia matatizo yako, lakini kuzungumza ana kwa ana na mtu anayekupenda na kukujali na anayetaka mema zaidi kwako hufanya kuwa rahisi zaidi.

Nicole S., umri 18, Idaho, USA

Majibu yanadhamiriwa kwa msaada na mtazamo, si kama matamko rasmi ya mafundisho ya Kanisa.

Unaweza Kumtegemea

Askofu wako au rais wa tawi ni mtumishi wa kweli wa Bwana. Unaweza kumtegemea kwa maelekezo unapotafuta maongozi kutoka kwa Roho Mtakatifu na maandiko. Ni lazima uelewe kuwa askofu yuko pale ili kusaidia, na kwamba anaongozwa na Mungu.

Stanislav R., umri 19, Donetsk, Ukraine

Kumbuka Kwamba Anakupenda

Ikiwa una kitu unachotaka kweli kujadiliana na askofu, inaweza kuwa rahisi kuzungumza naye kuhusu shule na mambo mengine ya kawaida kwanza. Ikiwa una wasiwasi kwa sababu unahitaji kuzungumza naye mambo ya toba, kumbuka kwamba anakupenda. Huhitaji kuwa na wasi wasi kuhusu kile atakachofikiria juu yako, kwa sababu, kwa nini akubeze kwa kutaka kuwa karibu na Kristo?

Ashley D.,umri 17, Arizona, Marekani

Sali ili Ufahamu

Jiulize kwa nini unasikia vibaya ukizungumza na askofu. Unafikiri hataweza kutatua matatizo yako? Sali ili ujue kuwa askofu anakupenda na ameitwa ili kukusaidia.

Adam H., umri 13, California, USA

Hata Kama Utafanya Makosa

Inaweza kuwa vigumu na aibu kukiri mambo kwa askofu wako lakini unapotoka katika ile ofisi, utahisi kupata nafuu, na utajua kuwa Baba wa Mbinguni anakupenda. Anataka uwe na furaha hata ukifanya kosa.

Amanda W., umri 16, Utah, USA

Yuko Hapa Ili Kusaidia

Askofu ni mchungaji wa kata yako. Kumbuka kwamba atafanya awezalo kukusaidia na ana uwezo wa Bwana uko upande wake. Ukihisi uoga, unaweza kusali kwa ajili ya kuomba nguvu ili kuweza kuzungumza na askofu wako. Hatimaye, utafurahi kuwa ulimwendea—na itakuwa ya kustahili.

Samuel H., umri 14, Idaho, USA

Kwa maelezo zaidi kuhusu mada hii, ona C. Scott Grow, "Kwa nini ninahitaji Kuungama kwa Askofu?," Liahona, *Okt. 2013, 59.*

MWAMINI YEYE

"Tafuta ushauri kutoka kwa viongozi wako wa ukuhani, hasa askofu wako. Anajua viwango, na anajua cha kukufunza. Tafuta fursa za kuwa naye. Unaweza kutarajia akuulize maswali ya moja kwa moja, ya upekuzi. Mwamini. Mwamini yeye. Muombe akusaidie kuelewa kile Bwana anachotarajia kutoka kwako. Dhamiria kuishi kulingana na viwango vya Kanisa vya maadili. Uhusiano wenye maana na mtu mzima kiongozi ni muhimu kukusaidia kuwa msafi kimaadili na mwenye kustahili."

Mzee M. Russell Ballard wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili, "Usafi Huja kabla ya Uwezo," *Ensign*, Nov. 1990, 37.

SWALI LINALOKUJA

"Ninakejeliwa shuleni kwa kuwa MSM. Ninajua ninapaswa kutetea ninachoamini lakini ni vigumu sana! Nitakuwaje jasiri ya kutosha kuwaambia wale watu wakome?

Wasilisha majibu yako, na ukipenda, picha ya ubora wa hali ya juu kabla ya Mei 1, 2015, katika liahona.lds.org, kwa barua pepe liahona@ldschurch.org, au kwa posta (Ona anwani katika ukurasa wa 3).

Taarifa ifuatayo na ruhusa lazima ijumuishwe katika barua pepe yako au barua: (1) jina kamili, (2) tarehe ya kuzaliwa, (3) kata au tawi, (4) kigingi au wilaya, (5) ruhusa yako uliyoandika, na kama u chini ya miaka 18, ruhusa iliyoandikwa na mzazi wako (barua pepe inakubalika) ili kuchapisha majibu yako na picha.

Majibu yanaweza kuhaririwa kwa ajili ya urefu au ufafanuzi.

Ni nani

Ellie alijua shujaa wake ni nani, lakini alikuwa mwoga sana kusema.

Na Charlotte Mae Sheppard
Imetokana na tukio halisi

*"Simama na dhamiri yako, heshima yako, imani yako; simama kama shujaa" (*Children's Songbook, *158).*

Ellie aliuma kucha la dolegumba lake kwa wasiwasi. Binti Fitz alikuwa anafuata safu ya madawati akiuliza kila mwanafunzi swali, mmoja baada ya mwingine.

"Nani shujaa wako?" Binti Fitz akamwuliza Jeremy.

Jeremy hakupoteza muda kujibu. "Baba yangu!" alisema kwa kujivunia.

KIELELEZO NA VALERIO FABBRETTI

shujaa Wako?

Binti Fitz akatabasamu "Na wako Sara?"

Jibu lake likaja haraka vivyo. "Abraham Lincoln."

Ellie alisikia mapigo ya moyo wake wakati Binti Fitz alipoendelea kwenye safu ya wanafunzi. Walikuwa wamezungumza juu ya mashujaa siku nzima na sasa kila mtu alipaswa kusema ni nani alikuwa shujaa wake—mbele ya darasa zima!

Amber na Justin walisema mama zao walikuwa mashujaa wao. Walter alisema wake alikuwa babu yake. Wanafunzi wengine wachache walisema shujaa wao alikuwa mfalme au rais.

Wanafunzi wachache walisalia kabla ya Binti Fitz kumfikia Ellie. Ilimbidi kufikiria shujaa—na kwa haraka.

Ellie alitazama chini kwenye viatu vyake, akiona haya. Kuamua nani alikuwa shujaa haikuwa shida hasa. Tayari alijua shujaa wake ni nani. Ilikuwa Yesu Kristo. Aliwaponya wagonjwa, alifufua wafu, na kulipa gharama ya dhambi ya kila mtu. Alikuwa shujaa mkuu aliyewahi kuishi! Aliogopa sana kusema hivyo.

Ellie aliuma kucha ya dolegumba lake tena na kufikiria kuliambia darasa zima kwamba Yesu Kristo alikuwa shujaa wake. Ingekuwaje kama Jeremy angemcheka? Na ingekuwaje kama Sara na Amber wangemsengenya wakati wa mapumziko?

Bila shaka alijua kuwa Yesu Kristo alikuwa shujaa wake Lakini hilo halikumaanisha kila mtu alihitaji kujua.

Binti Fitz alisimama hasa mbele ya dawati la Ellie na kutabasamu. "Na shujaa wako ni nani Ellie?"

Ellie alitazama kutoka safu ya wanafunzi waliokuwa karibu naye hadi kwa Binti Fitz. "Abraham Lincoln," alinong'ona.

Binti Fitz akafurahi "Vyema" alisema alipoenda kwa mwanafunzi aliyefuata katika safu.

Mara tu alipoondoka, mabega ya Ellie yalitua kwa shime. Shukrani, hilo lilikuwa limepita. Jambo la mwisho alilohitaji ilikuwa ni kila mtu kujua ni nani aliyekuwa shujaa wake—

"Yesu Kristo," sauti ikasema.

Macho ya Ellie yakapanuka alipogeuka pole pole. Pale—chini kidogo ya safu—alikaa mvulana mdogo aliyekuwa na nywele zilizokunjana. Alikuwa mwembamba na mwoga, na kila mara alikaa nyuma ya darasa. Ellie hata hakufahamu jina lake. Hakumkumbuka akisema hata neno moja—hadi sasa.

Wanafunzi wachache waligeuka ili kumkodolea macho yule mvulana lakini hakuwaona. Alimtazama tu Binti Fitz na kuzungumza tena. "Shujaa wangu ni Yesu Kristo."

Binti Fitz alitabasamu sana na kuendelea kwenye safu. Lakini Ellie alimtazama yule mvulana kwa mshangao Alikuwa amekuwa na uoga wa kumwambia kila mtu kuhusu shujaa wake, lakini mvulana huyu hakuwa mwoga. Hata hakuenda katika kanisa lake! Lakini alijua ilivyokuwa muhimu kusimama kama mfano wa Yesu Kristo hata ilipokuwa vigumu.

Ellie alitabasamu kwa yule mvulana. Hangeogopa tena kusema ni nani aliyekuwa shujaa wake. Kwani, alikuwa na wawili sasa. ■

Mwandishi anaishi katika California, Marekani.

Sala na Makanisa Makuu

Na McKelle George
Kutokana na tukio halisi

"Kama mkipendana ninyi kwa ninyi, ninyi ni wanafunzi Wangu" (Yohana 13:35).

Dani alitazama juu lakini bado hakuweza kuona kilele cha kanisa lile kubwa. Watu wa makanisa tofauti walikuja pale. Dani hakuelewa kwa nini familia yake ilikuwa inatembelea kanisa hili siku ya Ijumaa lakini Baba alisema walikuwa wanahudhuria kitu kilichoitwa Wimbo wa Jioni.

"Hiyo ni nini?" Dani akauliza.

"Ni mkutano ambapo watu wanaimba, kusoma maandiko na kusali pamoja" Baba alisema. "Kama familia kubwa mwishoni mwa siku."

Dani alipenda jinsi hilo lilivyosikika. Yeye na familia yake walikuwa wanatembelea Uingereza. Jumapili iliyopita walikwenda katika kata iliyoitwa York. Katika darasa la Watoto, watoto wote waliyajua maandiko yale yale ambayo Dani aliyajua. Alijua kata aliyotembelea ilikuwa sehemu ya Kanisa la Kweli la Kristo, kama kata yake nyumbani.

Lakini hili kanisa kubwa lilikuwa tofauti sana na kile alichokizoea. Aliona meza ndogo iliyojaa mishumaa. Dani alimtazama mvulana akiwasha mshumaa.

"Kwa nini unawasha mishumaa?" Dani akamwuliza.

Yule mvulana akatabasamu. "Ninawasha mshumaa ninapoomba kwa ajili ya mambo maalum. Mradi mwale unaendelea kuwaka,

VIELELEZO NA SCOTT GREER

"Tunapaswa kuwapenda watu wote, kuwa wasikilizaji wema, na kuonyesha kujali imani yao ya dhati."

Mzee Dallin H. Oaks wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili, "Kuwapenda Wengine na Kuishi na Tofauti," *Liahona,* Nov. 2014, 27.

ninatumaini kuwa sala itaendelea kusikilizwa na Mungu."

Ilionekana kama mishumaa ya kawaida kwa Dani Alikanganyikiwa kidogo lakini alitaka kuwa mpole. Alitabasamu kwa yule mvulana.

Dani na familia yake walikaa, na mara Wimbo wa jioni ulianza. Alimwona mvulana yule yule safu chache kutoka alipokuwa. Kisha akagundua kuwa hakujua wimbo wowote kati ya nyimbo ambazo kila mtu alikuwa akiimba. Walipoomba, walisoma kutoka katika kijitabu kidogo. Kila kitu kilionekana tofauti na kile alichozoea.

Lakini muziki ulikuwa mzuri, hata ingawa haukufahamika. Kisha mtu akasimama kusoma maandiko. Alikuwa amevaa kanzu, badala ya suti na tai kama vile askofu wa Dani. Lakini mara alipoanza kusoma, Dani aligundua kuwa aliifahamu hadithi hii! Alikuwa akisoma kuhusu Yesu akiponya wakoma 10.

"Baba." Dani alinong'oneza, "Ninaipenda hadithi hii."

Baba akatabasamu. "Pia mimi."

Kisha mtu aliyekuwa amevaa kanzu akatoa sala. Alimwomba Mungu kuwabariki waliokuwa wagonjwa na waliokuwa na shida. Kama Vile Dani alivyofanya! Aliomba pia baraka maalumu kwa viongozi wa Kanisa lake. Dani akakumbuka jinsi familia yake kila mara ilivyomwomba Baba wa Mbinguni kumbariki Rais Thomas S. Monson na washauri wake.



Hisia ya joto ikaja ndani ya moyo wa Dani. Alijua kwamba Baba wa Mbinguni alikuwa akimwambia kuwa Aliwapenda watoto wake *wote* na Alisikiliza sala zao *zote* hata kama walienda kwenye kanisa tofauti na hawakuwa na utimilifu wa injili

Walipoamka ili kuondoka, Baba aliangalia simu yake. Alionekana kuwa na huzuni alipokuwa akisoma ujumbe wake. "Dada ameaga dunia," alisema.

"La hasha!" Dani akatoa sala ya haraka moyoni mwake kwamba Rais Monson awe SAWA.

"Je u mzima?" mtu akauliza. Ilikuwa yule mvulana wa hapo awali. Alikuwa amemsikiliza Dani na alionekana kuwa na wasiwasi.

"Dada Monson ameaga dunia," Dani akasema. "Ni mke wa nabii wetu, Rais Monson."

"Pole," alisema kwa upole. "Nitawasha mshumaa kwa ajili yake."

Dani akatabasamu na kumshukuru. Alifikiri ilikuwa vyema kwa mvulana yule kutoa sala maalum kwa ajili ya Rais Monson. Alijua kuwa Baba wa Mbinguni angesikiliza ile sala aliyosema moyoni mwake na ile ambayo yule mvulana alitoa. ■

Mwandishi anaishi Utah, Marekani.

SHAHIDI MAALUM



Na Mzee Russell M. Nelson
Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili

Washiriki wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili ni mashahidi maalum wa Yesu Kristo.

Kwa nini kuwa **MTIIFU** ni muhimu sana?



VIELEZO NA APRIL STOTT

Kutoka kwa "Acha Imani Ionekane," Liahona, *Mei 2014, 29–32.*

KIELELEZO NA MATT SMITH

Yesu amponya Mwenye Ukoma

Na Erin Sanderson

Fikiria wakati ulipokuwa mgonjwa. Je! Mtu alifanya jambo lolote la wema ili kukusaidia kujisikia vyema zaidi?

Katika Agano Jipya, tunasoma kuhusu jinsi Yesu alivyoonyesha ukarimu kwa watu waliokuwa wagonjwa. Siku moja mtu aliyekuwa na ugonjwa mkali wa ngozi unaoitwa ukoma alimwendea Yesu. Alijua kuwa Yesu alikuwa na uwezo wa kuponya kila mtu aliyekuwa mgonjwa. Aliamini kuwa Yesu angemponya. Yesu akamgusa mkoma na akamwambia, "Nataka takasika!" (Marko 1:41). Mara Yesu alipokuwa amenena, yule mtu aliponywa.

Tunaweza kufuata nyayo za Yesu kwa kuwa wema na wenye upendo kwa wengine walio wagonjwa au wenye huzuni. ■

Mwandishi anaishi Utah, Marekani.

MAWAZO KWA AJILI YA HOTUBA YA FAMILIA

Unaweza kutumia michoro ya maandiko katika ukurasa wa 74 ili kusimulia hadithi kutoka Marko 1:40–42. Kisha unaweza kusoma Yuda 1:22 na kupanga jinsi ya kufanya kitu kama familia ili kuleta tofauti katika maisha ya mtu fulani. Pengine mnaweza kumhudumia mtu fulani kwa siri!

Wimbo: "Tell Me the Stories of Jesus" (*Children's Songbook,* 57)

Maandiko: Mark 1:40–42

Video: Nenda **Biblevideos.org** ili kutazama "Jesus Heals a Lame Man on the Sabbath" na "Jesus Heals a Man Born Blind."

KUFUATA NYAYO ZA YESU

Pamoja na familia yako, igiza jinsi ambavyo ungeweza kuonyesha upendo kwa wengine katika hali hizi? Tunga baadhi ya hali zako mwenyewe!



Familia moja imehamia katika eneo lenu.

Watoto wengine wanamkejeli mtoto mwingine shuleni.

Mgeni asiyemjua yeyote Kanisani amekuja kwenye masomo ya Watoto.

Kaka au dada yako mdogo hana mtu wa kucheza naye.

Mtoto mchanga analia na mama yako anajaribu kuandaa chakula cha jioni.

Mtu katika kata yako au tawi ni mgonjwa na hawezi kutoka nyumbani.

KUSHOTO: *MKOMA ALIYESEMA 'ASANTE,'* NA JOHN STEEL © PROVIDENCE LITHOGRAPH; KULIA: KIELEZO NA DAVID MALAN; KIELELEZO CHA MALAPA NA MARK ROBISON

JIFUNZE ZAIDI: INJILI

Agano Jipya lina vitabu vinne maalum vinavyoitwa injili ambavyo viliandikwa na baadhi ya wanafunzi wa Yesu. Injili zinasimulia kuhusu wakati Yesu Kristo alipokuwa akiishi duniani. Hadithi kuhusu kuponya mwenye ukoma ipo kwenye injili tatu. Ipo kwenye Marko 1:40–42 na pia kwenye Mathayo 8:2–4 na Luka 5:12–14.

DOKEZO LA MAANDIKO: KUPEKUA NENO

Kwenye Marko 1:41 neno *huruma* limetumiwa. Wakati mwingine kuna maneno makubwa kwenye Biblia ambayo unaweza kushindwa kuyaelewa. Unapopata neno usilolielewa, unaweza kutumia Mwongozo wa Maandiko ili kukusaidia! Kwa mfano unaweza kuangalia "Huruma" ili kujua lina maana gani na kutafuta maandiko mengine yanayolitumia. Ni maneno gani mengine unayoweza kuangalia katika hadithi juu ya Yesu akimponya mwenye ukoma?

Yesu Awaponya Wagonjwa

Marko 1:40–42;
Luka 4:38–40



Gandisha karatasi hii kwenye karatasi nzito au kadibodi. Kisha kata maumbo na kuyanatisha katika vijiti au mifuko ya karatasi. Yatumie kuwasaidia kuigiza hadithi kutoka katika Agano Jipya.

Unaweza kuchapisha nakala zaidi katika liahona.lds.org.

VILELEZO NA BETH M. WHITTAKER

Na Mzee
Claudio D. Zivic
Wa wale Sabini

NJIA Sahihi



"Yasikilizeni maneno ya yule Mungu aliyewaumba ninyi" (M&M 43:23).

Miaka mingi iliyopita familia yangu na mimi tulitembelea Mbuga ya Taifa ya Arches huko Utah, Marekani. Mojawapo ya matao maarufu katika mbuga ni Delicate arch, na tuliamua kukwea mlima ili kuifikia.

Tulianza kwa hamasa, lakini baada ya muda wengine walitaka kupumzika. Nilikuwa nataka kufika huko haraka kwa hivyo nikaenda pekee yangu. Bila kuwa mwangalifu kwa njia niliyopaswa kuchukua, nilianza kumfuata mtu aliyeonekana kama alifahamu aliko kuwa akienda.

Njia ikawa ngumu zaidi kupanda. Nilikuwa na hakika kwamba familia yangu haingeifikia. Mara nikaona Delicate Arch, lakini kwa mshangao wangu nisingeweza kuifikia Njia niliyofuata haikuelekeza kwenye tao.

Nilivunjika moyo na nikarudi nyuma. Nilingoja kwa wasiwasi hadi nilipokutana na kundi langu tena. Waliniambia kuwa walikuwa wamefuata ishara zilizoonyesha njia sahihi, na kwa uangalifu na bidii walikuwa wamefika Delicate Arch. Kwa bahati mbaya, nilikuwa nimechukua njia isiyo sahihi Ni somo lipi nilijifunza!

Usipotoke kutoka katika njia yako ya kuelekea uzima wa milele na Baba yako wa Mbinguni Fuata kanuni za injili na amri unazojifunza, na utakuwa kwenye njia ya kuishi naye milele. ■

Kutoka "Tusipite Kwenye Njia Isiyo sahihi," Liahona, *May 2014, 39–41.*

KIELEZO NA GREG NEWBOLD

Ninajua Kwamba Yesu Ananipenda

Na Jane McBride Choate
Imetokana na tukio halisi

Laney alikuwa anajaribu sana kuwa na staha kanisani. Lakini alikuwa amechoka, miguu yake ilianza kulegea.

Baada ya sakramenti kuisha, Laney alifungua kitabu chake juu ya Yesu. Alipata picha ya Yesu na watoto wadogo. Ilimfanya kusikia amani na furaha ndani yake.

Hadithi inaendea katika ukurasa wa 79.

VIELEZO VYA MISTARI NA PAUL MANN; VIELEZO VYA RANGI NA JESS GOLDEN









1-Kata

Kitabu changu juu ya YESU

1

4-Kata

I Know That My Savior Loves Me
Na Tami Jeppson Creamer na Derena Bell

8

2-Mkunjo



Upendo ambao alihisi kwa wadogo wallo wake
ninajua anahisi vivyo hivyo kwangu.

4

Sikumgusa wala kukaa kwenye gotí lake
lakini Yesu ni halisi kwangu.

5

3-Mkunjo

2

Hapo kale katika mahali pazuri, watoto walikusanyika kumzunguka Yesu.

7

Moyo wangu nautoa Kwake Ninajua kuwa Mwokozi ananipenda.

Mkunjo



3

Alibariki na kufundisha walipohisi upendo wake. Kila mmoja aliona machozi usoni pake.

6

Ninajua anaishi! Nitamfuata kwa uminifu.

Mkunjo

Baada ya mkutano wa sakramenti kumalizika, Laney alimwuliza Mama, “Kwa nini ni rahisi kuwa na staha ninapotazama kitabu changu juu ya Yesu?”

“Ninafikiri ni kwa sababu kinakukumbusha jinsi Yesu anavyokupenda,” Mama akasema.

Laney alikubali kwa kichwa. “Unafikiri Yesu anajua kuwa ninampenda pia?” akauliza.

Mama akamkumbatia Laney. “Ndiyo nina hakika anajua.” ■

Mwandishi anaishi katika Colorado, Marekani.

Mwezi huu unaadhimisha miaka 100 tangu Urais wa Kwanza uwahimize waumini kuwa na jioni ya familia nyumbani. Dondoo zifuatazo zinatoka katika barua ya Urais wa Kwanza ukiitambulisha jioni ya familia nyumbani. Ilitolewa Aprili 1915 na kuchapishwa katika Improvement Era *Juni 1915 (Kurasa 733–34). Herufi kubwa na vituo vmefanywa kuwa vya kisasa.*

MIAKA 100 YA Jioni ya Familia Nyumbani

Wapendwa Kaka na dada zangu: Tunawashauri Watakatifu wa Siku za Mwisho kuzingatia zaidi amri ya Bwana iliyotolewa katika sehemu ya 68 ya Mafundisho na Maagano:

"*Na tena, ili mradi wazazi wanao watoto katika Sayuni, au katika kigingi chake chochote ambacho kimeundwa, ambao hawawafundishi wao kuelewa mafundisho ya toba, imani katika Kristo Mwana wa Mungu aliye hai, na ubatizo na kipawa cha Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono, wafikapo miaka minane, dhambi zao zitakuwa juu ya vichwa vya wazazi ; . . .*

Na pia wawafundishe watoto wao kuomba, na kusimama wima mbele za Bwana" [ona M&M 68:25–28].

Watoto wa Sayuni wanapaswa pia kushika kwa ukamilifu zaidi amri ambayo Bwana alitoa kwa Israeli ya kale na kuirudia kwa Watakatifu wa Siku za Mwisho.

"Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako" [Kutoka 20:12].

Funuo hizi zinatumika kwa nguvu zaidi kwa Watakatifu wa Siku za Mwisho na inahitajika kwa akina baba na akina mama katika Kanisa hili kuwa amri hizi zifundishwe na kutumiwa majumbani mwao.

Kwa hivyo, tunawashauri na kuhimiza uanzishwaji wa "jioni ya familia nyumbani" Kote katika Kanisa ambapo akina baba na mama wanaweza kuwakusanyika wavulana na wasichana wao nyumbani na kuwafundisha neno la Bwana. Wanaweza basi kujifunza kikamilifu zaidi mahitaji na matakwa ya familia zao, wakati huo huo wakifahamiana wao kwa wao na watoto wao kwa undani zaidi pamoja na kanuni za injili ya Yesu Kristo. Jioni hii ya nyumbani inapaswa kutengwa kwa ajili ya sala, kuimba nyimbo za dini, nyimbo, muziki wa vyombo, kusoma maandiko, mada za familia na mafunzo mahususi ya kanuni za injili na matatizo ya kimaadili ya maisha, pamoja na majukumu ya watoto kwa wazazi, nyumba, Kanisa, jamii na taifa. Kwa watoto wadogo, ukariri sahihi wa, nyimbo, hadithi na michezo inaweza kuanzishwa. Viburudisho vyepesi ya aina hiyo kwa kiwango kikubwa vilivyotengenezwa nyumbani vinaweza kuandaliwa.

Urasmi na ugumu unapaswa kuepukwa kabisa na familia nzima inapaswa kushiriki katika mazoezi haya.

Mikusanyiko hii itatoa fursa za maelewano na kuaminiana kati ya wazazi na watoto, kati ya kaka na dada, na pia kutoa nafasi kwa maneno ya kuonya, ushauri na mwongozo kutoka kwa wazazi kwa ajili ya wavulana na wasichana wao. Itatoa fursa kwa wavulana na wasichana kuwaheshimu baba na mama zao na kuonyesha shukrani yao kwa baraka za nyumbani ili ahadi za Bwana kwao ziweze kutimia kihalisi, na maisha yao kurefushwa na kufanywa kuwa ya furaha. . . .

Tunawahimiza vijana kubaki nyumbani jioni hiyo na kutumia nguvu zao katika kuifanya kuwa yenye mafunzo, yenye faida, na ya kuchangamsha.

Ikiwa Watakatifu watatii ushauri huu, tunaahidi kuwa baraka kuu zitatokea. Upendo nyumbani na utiifu kwa wazazi utaongezeka. Imani itajengwa katika mioyo ya vijana wa Israeli, na watapata uwezo wa kupigana na vishawishi viovu na majaribu yanayowazonga.

Ndugu zenu,
JOSEPH F. SMITH
ANTHON H. LUND
CHARLES W. PENROSE
Urais wa Kwanza ■

PICHA KWA HISANI YA CHURCH HISTORY LIBRARY

UMAIZI

Ninawezaje kuipa kipaumbele jioni ya familia?

"Unapofanya kazi kuimarisha familia yako na kujenga amani, kumbuka jioni ya familia nyumbani kila wiki. Tahadhari usifanye jioni yenu ya familia nyumbani kuwa kitu cha ziada baada ya siku yenye shughuli nyingi. Amua kuwa Jumatatu usiku familia yako itakuwa pamoja nyumbani kwa jioni hiyo. Usikubali mahitaji ya kikazi, michezo, starehe, kazi ya ziada shuleni au kitu kingine chochote kuwa muhimu kuliko muda huo mnaotumia pamoja nyumbani na familia yako. Muundo wa jioni yenu si muhimu kama muda uliowekezwa mle. Injili inapaswa kufundishwa kwa njia rasmi na kwa njia isiyo rasmi. Fanya iwe tukio lenye maana kwa kila mwanafamilia."

Mzee Richard G. Scott wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili, "Fanya Matumizi ya Imani kuwa Kipaumbele Chako," *Liahona,* Nov. 2014, 94.

Pia Katika Toleo Hili

KWA VIJANA WAKUBWA

ENENDENI KATIKA Imani

Njia hizi nne za umaizi kutoka katika maisha ya Nefi zinaweza kukupa kujiamini katika uamuzi wako.



p. 44

KWA VIJANA

p. 50

KWA SABABU YA JOSEPH

Ni kwa namna gani maisha yako ni tofauti kwa sababu ya Nabii Joseph Smith? Fikiria njia hizi sita.

KWA WATOTO

NINAJUA KUWA YESU ANANIPENDA

Tengeneza kijitabu chako mwenyewe kukusaidia kuwa na staha kanisani.

p. 76

KANISA LA
YESU KRISTO
LA WATAKATIFU
WA SIKU ZA MWISHO

SWAHILI
4 021256 47743 4